# Maarifa ya Jamii

## Kitabu cha Mwanafunzi

Darasa la **7**



Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Maarifa ya Jamii

## Kitabu cha Mwanafunzi

### Darasa la Saba



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 549

Jina la Chapisho: Maarifa ya Jamii Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Saba

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978-9987-09-338-0

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 12 Julai, 2021 kuwa Kitabu cha Kiada kwa ajili ya Mwanafunzi wa Darasa la Saba katika ngazi ya elimu ya Msingi nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa Mwaka 2019.

**Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa**
Kamishna wa Elimu

Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR ONLINE USE ONLY

MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 1 30/07/2021 11:58

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2020

Toleo la Kwanza 2020
Toleo la Pili 2021

ISBN 978–9987–09–338–0

Taasisi ya Elimu Tanzania
S. L. P 35094
Dar es Salaam

Simu: +255 735 041 170 / +255 735 041 168
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kukitoa kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 2 30/07/2021 11:58

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Yaliyomo

**Shukurani** ...................................................................................v

**Utangulizi** ...................................................................................vi

**Sura ya Kwanza**

**Majanga ya asili** ...................................................................................1

**Sura ya Pili**

**Maendeleo ya binadamu na zana za uzalishaji mali**.......................27

**Sura ya Tatu**

**Tabianchi ya Tanzania**.....................................................................56

**Sura ya Nne**

**Mila na desturi za Watanzania**..........................................................78

**Sura ya Tano**

**Usafirishaji na uhusiano wa Tanzania na nchi nyingine**................88

**Sura ya Sita**

**Athari za njia zilizotumika kudai uhuru Afrika**................................94

**Sura ya Saba**

**Maendeleo nchini Tanzania baada ya uhuru**..................................102

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 3 30/07/2021 11:58

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Sura ya Nane**

Matumizi ya ramani ....................................................................118

**Sura ya Tisa**

Mfumo wa Jua..............................................................................133

**Sura ya Kumi**

Idadi ya watu na makazi.............................................................144

**Sura ya Kumi na Moja**

Shughuli za kiuchumi katika nchi za

Jumuiya ya Afrika Mashariki ......................................................165

**Sura ya Kumi na Mbili**

Ujasiriamali ...................................................................................175

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 4 30/07/2021 11:58

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki waliofanikisha uandishi wa kitabu hiki cha mwanafunzi.

TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wafuatao:

**Waandishi:** Dkt. Joyce Kahembe, Mwl. Ferdnand Lutatenekwa, Mwl. Charles Manyama na Mwl. Sophia Amasi (Historia), Mwl. Beatrice Rulenguka, Mwl. Neema Kashindye, Mwl. Mariam Japhet, Mwl. Emanuel Stanislaus, Mwl. Aristarick Lekule (Jiografia), Dkt. Lilian Macha (Ujasiriamali) na Bw. Fikiri Salla (Majanga ya moto)

**Wahariri:** Prof. Gaudens Mpangala, Mwl. Victor Itule (Historia) Prof. Faustin Paul Lekule (Ujasiriamali), Dkt. Asubisye Mwamfupe, Dkt. Mohamed Khamis Said, na Dkt. Noah Makula Pauline (Jiografia) na Bw. Mussa Kaoneka (Lugha-BAKITA)

**Msanifu:** Bw. Katalambula Faraji

**Wachoraji:** Bw. Fikiri Msimbe na Alama Art and Media Production Limited.

**Mchora ramani:** Bi. Sauda Kileo

**Mpiga picha:** Bw. Chrisant Ignas

**Waratibu:** Mwl. Beatrice Rulenguka na Mwl. Charles Manyama

Pia, TET inatoa shukurani kwa walimu wote walioshiriki katika ujaribishaji wa kitabu hiki cha mwanafunzi. Vilevile, TET inatoa shukurani za pekee kwa Shirika la “Global Partnership for Education (GPE)” kupitia mradi wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) uitwao “Literacy and Numeracy Education Support (LANES II)” kwa ufadhili wao uliofanikisha kazi ya uandishi na uchapaji wa kitabu hiki.

Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kusimamia kwa karibu zoezi zima la uandishi na uchapaji wa kitabu hiki.

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Utangulizi

Kitabu hiki ni cha tano katika mfululizo wa vitabu vitano vya somo la Maarifa ya Jamii, kuanzia Darasa la Tatu hadi la Saba, kilichoandaliwa mahususi kwako mwanafunzi wa Darasa la Saba. Kitabu hiki, kimeandaliwa kulingana na muhtasari wa Maarifa ya Jamii wa mwaka 2019, uliotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kitabu hiki kimeandaliwa ili kukuwezesha kujifunza Majanga ya asili, Maendeleo ya binadamu na zana za uzalishaji mali, Tabianchi ya Tanzania, Mila na desturi za Watanzania, Usafirishaji na uhusiano wa Tanzania na nchi nyingine, Athari za njia zilizotumika kudai uhuru Afrika, Maendeleo nchini Tanzania baada ya uhuru, Matumizi ya ramani, Mfumo wa Jua, Idadi ya watu na makazi, Shughuli za kiuchumi katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, na Ujasiriamali. Maudhui ya kitabu hiki yamewasilishwa kwa njia ya matini, kazi za kufanya, ramani na picha zenye mvuto ambazo zote zinachochea ujenzi wa umahiri unaokusudiwa kwa kila sura. Vilevile, katika kila sura yapo mazoezi yenye lengo la kupima uelewa wako. Hivyo basi, unapaswa kufanya kazi zote zilizopo kwenye kitabu hiki pamoja na kazi zingine utakazopewa na mwalimu.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 6 30/07/2021 11:58

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kwanza

# Majanga ya asili

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Sita, ulijifunza kuhusu dhana ya mabadiliko ya tabianchi, ongezeko la joto duniani na uhusiano kati ya shughuli za kibinadamu na kuongezeka kwa joto duniani. Vilevile, ulijifunza kuhusu majanga yanayosababishwa na ongezeko la joto duniani, athari zake na mbinu za kukabiliana nayo. Aidha, ulijifunza namna ya kudhibiti uharibifu wa mazingira. Katika sura hii, utabainisha majanga ya asili na namna ya kushiriki katika kudhibiti athari zake. Vilevile, utajifunza vyanzo vya janga la moto na namna ya kushiriki katika kuzuia janga hilo. Aidha, utajifunza kanuni za kuzima moto na namna ya kuokoa waathirika wa janga la moto. Maarifa na ujuzi utakaoupata katika sura hii, utakusaidia kuwa na uwezo wa kubaini majanga ya asili na kuchukua hatua za kukabiliana na athari za majanga hayo.*

## Dhana ya majanga ya asili

Majanga ya asili ni matukio makubwa ya hatari yanayosababishwa na nguvu za asili ambayo hutokea ghafla na husababisha maafa. Matukio haya ya hatari yanakuwa majanga iwapo tu kutokea kwake kutasababisha maafa ambapo rasilimali zilizopo katika jamii haziwezi kuzuia maafa hayo kutokea. Baadhi ya majanga ya asili ni pamoja na tetemeko la ardhi, mlipuko wa volkano, maporomoko ya ardhi, tsunami, moto, mafuriko na ukame. Japokuwa mafuriko, ukame na moto ni majanga ya asili, wakati mwingine huweza kusababishwa na shughuli za kibinadamu.

Majanga huweza kutokea ama kwa ghafla au taratibu. Baadhi ya majanga ya asili yanayotokea kwa ghafla ni mafuriko, tetemeko la ardhi, mlipuko wa volkano, maporomoko ya ardhi, tsunami na moto. Ukame ni mojawapo ya janga la asili linalotokea taratibu. Majanga haya huweza kutokea sehemu yoyote ile kulingana na asili ya janga hilo. Majanga mengine hutokea kwa

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 1 30/07/2021 11:58

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kujirudiarudia katika eneo moja. Majanga hayo yanapotokea husababisha maafa kama vile vifo vya watu na wanyama, kupotea au kuharibika kwa uoto, mali, miundombinu, na magonjwa ya mlipuko. Yafuatayo ni baadhi ya majanga ya asili na athari zake:



**Fikiri**

1. Kuhusu tetemeko la ardhi lililowahi kutokea.
2. Viashirio vya tetemeko la ardhi.
3. Mambo ya kufanya kujikinga na tetemeko la ardhi.

**Tetemeko la ardhi**

Tetemeko la ardhi ni mtikisiko wa ghafla unaotokea katika tabaka la juu la dunia. Mtikisiko huu husababishwa na nguvu za asili zinazotokana na nguvu ya mawimbi yapitayo katikati ya matabaka ya miamba ardhini. Miamba iliyopo chini ya uso wa dunia inapojongeleana aghalabu husababisha mvutano na msuguano. Mchakato huu mwishowe husababisha mpasuko ambao huachia nguvu ya mtetemo. Nguvu hii husababisha mtikisiko wa ghafla katika tabaka la juu la dunia unaoitwa tetemeko la ardhi. Nguvu hizi za mtetemo pia huweza kusababishwa na mlipuko wa volkano na shughuli za kibinadamu kama vile; milipuko ya nyuklia na uchimbaji wa madini. Ukubwa wa tetemeko la ardhi hupimwa kwa kifaa kiitwacho *sesimometa*. Kwa kawaida ni vigumu kutambua dalili za kutokea kwa tetemeko la ardhi, hivyo huweza kusababisha madhara makubwa sana endapo litatokea katika makazi ya watu. Madhara hayo ni pamoja na vifo na uharibifu wa mali.

***Athari za tetemeko la ardhi***

Tetemeko la ardhi huleta athari mbalimbali katika mazingira. Ingawa tetemeko la ardhi hudumu kwa sekunde chache katika eneo linalohusika, athari zake zinaweza kuwa kubwa sana. Athari za tetemeko la ardhi huweza kuwa kubwa, wastani au ndogo kutegemea na ukubwa wa tetemeko, uimara wa majengo na miundombinu mingine, na hali ya asili ya jiolojia ya sehemu inayohusika. Zifuatazo ni baadhi ya athari za tetemeko la ardhi:

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 2 30/07/2021 11:58

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(a) Uharibifu wa mazingira na maeneo ya makazi: Tetemeko la ardhi linapotokea husababisha kupasuka kwa miamba na kuharibika kwa miundombinu kama barabara, reli na viwanja vya michezo. Pia, huweza kusababisha kubomoka kwa majengo, kwa mfano, katika nchi yetu ya Tanzania mnamo mwaka 2016 mkoani Kagera na mwaka 2019 mkoani Katavi, kulitokea matetemeko ya ardhi. Matetemeko hayo yaliharibu miundombinu ya barabara, majengo ya shule, hospitali, na makazi ya watu.

(b) Mlipuko wa magonjwa: Tetemeko la ardhi husababisha kuharibika kwa miundombinu ya maji. Hii husababisha majitaka kusambaa na kuingia katika mifumo ya majisafi na hivyo kuyachafua. Maji haya ambayo siyo salama yakitumiwa na binadamu kwa kupikia, kunywa, kuogea na kusafishia vyombo, huweza kusababisha magonjwa ya mlipuko kama vile homa ya matumbo, kipindupindu na kuhara. Aidha, tetemeko la ardhi husababisha kutimka kwa vumbi na kufuka moshi ambao husambaa katika angahewa. Hali hii huweza kusababisha magonjwa ya macho na athari katika mfumo wa upumuaji.

(c) Mlipuko wa moto: Tetemeko la ardhi huweza kusababisha mlipuko wa moto ambao hutokana na kuharibika kwa miundombinu ya umeme, kulipuka kwa volkano au kugongana kwa mawe na hatimaye kutokea kwa moto. Moto huu mara nyingi huwa ni vigumu kuuzima kwa sababu ya kuharibika kwa miundombinu na hivyo kushindwa kufika katika maeneo yanayowaka moto.

(d) Kutokea kwa tsunami: Tetemeko la ardhi huweza kusababisha kutokea kwa mawimbi makubwa baharini ambayo huitwa tsunami. Mawimbi haya husambaa na kusafiri hadi katika fukwe za bahari ambapo husababisha maafa ikiwamo vifo vya watu na wanyama pamoja na uharibifu wa mali.

(e) Kuongezeka au kupungua kwa kina cha bahari: Tetemeko la ardhi linapotokea, husababisha kutikisika kwa sakafu ya bahari na hivyo kuhama au kuachana kwa miamba chini ya bahari. Hali hii huweza kusababisha kusambaa kwa volkano ambayo huganda na kupunguza kina cha bahari. Aidha, tetemeko la ardhi husababisha kubomoka kwa miamba iliyo pembezoni mwa bahari na hivyo kina cha bahari kuongezeka. Pia, kuachana kwa miamba iliyoko chini kwenye sakafu ya bahari kunaweza kusababisha kuongezeka kwa kina cha bahari.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 3 30/07/2021 11:58

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Tetemeko la ardhi pia linasababisha kuinuka kwa miamba pembezoni mwa bahari.

(f) Husababisha vifo kwa viumbe hai: Matetemeko ya ardhi yamekuwa yakisababisha vifo kwa binadamu na viumbe hai wengine. Tetemeko linapotokea, huweza kubomoa majengo na kuharibu miundombinu. Vifusi vya majengo vinapoangukia watu au wanyama huweza kusababisha vifo. Kielelezo namba 1 kinaonesha baadhi ya athari za tetemeko la ardhi katika mazingira.




**Kielelezo namba 1:** *Baadhi ya athari za tetemeko la ardhi*

***Tahadhari za kuchukua katika kukabiliana na athari za tetemeko la ardhi***

Ni muhimu kuchukua tahadhari mbalimbali ili kukabiliana na athari za tetemeko la ardhi. Tahadhari mojawapo ni kutoa elimu kuhusu namna ya kuepusha au kupunguza athari iwapo tetemeko la ardhi litatokea. Elimu hii ilenge kuwafikia watu wa rika zote yaani watoto, vijana, wenye mahitaji maalumu na wazee. Elimu hii pia izingatie chanzo, maeneo hatarishi na yenye historia ya kukumbwa na tetemeko mara kwa mara, madhara yatokanayo na tetemeko la ardhi na njia za kukabiliana nayo. Kituo cha kuratibu matetemeko ya ardhi kitumie vyombo vya habari na wadau mbalimbali katika kuelimisha jamii na kusambaza elimu kuhusu madhara ya tetemeko la ardhi. Wananchi waelimishwe kuhusu kujenga nyumba imara zenye uwezo wa kuhimili mitikisiko inayotokana na tetemeko la ardhi. Pia, idara za mipango miji zifanye tathmini ya ardhi kabla ya kugawa maeneo ya ardhi kwa wananchi kwa ajili ya ujenzi.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 4 30/07/2021 11:58

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Pia, endapo tetemeko la ardhi limetokea au linaendelea kutokea unashauriwa kukaa mbali na majengo marefu, miti, nyaya na nguzo za umeme, fukwe za bahari na pembezoni mwa mito mikubwa. Kama uko ndani ya nyumba ingia chini ya meza au kitanda na ujifunike kichwa na mwili wako kwa mavazi mazito ili yakukinge na vitu vizito na vyenye ncha kali kama vioo. Pia, unaweza kukaa kwenye kona ya chumba kuepuka kuangukiwa na ukuta. Ukisikia tetemeko limetulia paza sauti kuomba msaada. Aidha, endapo tetemeko likikukuta nje ya nyumba unashauriwa kulala chini mita kadhaa mbali na nyumba au kimbia na uelekee katika maeneo ya wazi yaliyotengwa na serikali kama viwanja na mashamba makubwa.

**Zoezi la 1**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Orodhesha athari nne zinazotokana na tetemeko la ardhi.
2. Eleza kwa kifupi kwa nini tetemeko la ardhi ni janga la asili.

**Mlipuko wa volkano**

Ndani ya ardhi, chini kabisa ya uso wa dunia kuna joto kali sana na mgandamizo mkubwa wa miamba. Joto hili kali huweza kuyeyusha miamba katika eneo hilo na kuifanya iwe katika hali ya kimiminika cha moto mithili ya ujiuji uitwao magma. Mgandamizo unapozidi huisukuma magma ambayo hupenya katika nyufa zilizo katika tabaka za miamba na kutokeza nje ya uso wa dunia. Magma pia huweza kuishia chini ya ardhi kabla ya kutokeza juu ya uso wa dunia na kuganda. Magma hii ikitokeza juu ya uso wa dunia huitwa lava.

Volkano huweza kutoka nje ya uso wa dunia kwa mlipuko au kwa kufuka taratibu. Mlipuko wa volkano unategemea kiasi cha joto katika miamba iliyo chini ya tabaka la ardhi, pamoja na nguvu ya msukumo au mgandamizo iliyoko chini ya ardhi. Magma hii huweza kutoka kwa mlipuko mkubwa na kuruka hewani mita kadhaa, kisha humwagika na kutiririka juu ya uso wa dunia kama Kielelezo namba 2 kinavyoonesha. Lava hii hutiririka na kutapakaa juu ya uso wa dunia na kuganda. Kitendo cha magma kutoka nje kwa kasi kubwa huitwa *mlipuko wa volkano*. Mlipuko wa volkano pia huambatana na kurusha jivu la volkano ambalo husambaa katika angahewa. Mlipuko

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

wa volkano huwa na mchanganyiko wa gesi kama salfadioksidi ambayo ni hatari kwa maisha ya viumbe hai. Mlipuko wa volkano huweza kutoa lava inayotapakaa katika eneo dogo au kubwa na baadaye hupoa na kuganda, kisha hutengeneza mlima au mwinuko wa lava. Nchini Tanzania, ipo milima yenye asili ya volkano. Baadhi ya milima hiyo hulipuka mara kwa mara na huitwa milima yenye volkano hai kama vile mlima wa Oldonyo-Lengai uliopo mkoani Arusha. Milima mingine ni ile iliyowahi kulipuka zamani, lakini bado inaonesha dalili kwamba huenda ikalipuka katika miaka ijayo. Milima hii huitwa milima yenye volkano tuli kama vile mlima Kilimanjaro na mlima Meru. Pia, ipo milima ya volkano iliyokufa au volkano mfu. Milima hii haina dalili za kulipuka tena japo iliwahi kulipuka miaka ya zamani sana kama vile mlima Rungwe.



**Kielelezo namba 2:** *Mlipuko wa volkano*

### *Athari za mlipuko wa volkano*

Volkano inapolipuka juu ya uso wa dunia husababisha athari mbalimbali kwa viumbe hai na mazingira kwa ujumla. Zifuatazo ni baadhi ya athari za mlipuko wa volkano:

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 6 30/07/2021 11:58

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(a) Vifo kwa viumbe hai: Volkano inapolipuka hurusha lava ambayo hufunika eneo la ardhi. Lava hiyo inaweza kuua viumbe hai kama vile wanyama, binadamu, na bakteria muhimu wa mfumo wa ikolojia. Pia, inaweza kukausha mimea.

(b) Matatizo ya kiafya katika mfumo wa upumuaji, macho na ngozi: Volkano inapolipuka hutoa moshi mzito, vumbi na majivu ambavyo huweza kusababisha matatizo ya kiafya kwa viumbe hai hususani wanyama na binadamu. Mfano, majivu yenye sumu yanaposambaa huweza kutua kwenye ngozi na kusababisha muwasho na kubabuka. Moshi mzito wenye gesi ya ukaa unaposambaa na kuvutwa na viumbe hai huweza kuathiri mfumo wa upumuaji na hata kusababisha vifo.

(c) Uharibifu wa mali kama vile miundombinu na makazi ya watu: Mlipuko wa volkano unapotokea kwa kiwango kikubwa hufunika miundombinu zikiwemo barabara kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 3 (a), reli na maeneo ya wazi ikiwamo viwanja vya michezo na uharibifu wa mali kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 3 (b).

(d) Uchafuzi wa vyanzo vya maji: Volkano huweza kutiririka katika vyanzo vya maji na kusambaza kemikali zenye sumu. Kemikali hizi huweza kusababisha magonjwa na vifo kwa viumbe hai kama binadamu, wanyama, mimea na wadudu. Aidha, volkano huweza kuziba vyanzo vya maji na kusababisha ukosefu wa maji.

(e) Kutikisika na kuporomoka kwa ardhi: Mlipuko wa volkano huambatana na kutikisika kwa ardhi ambako kunaweza kusababisha kutokea kwa maporomoko ya ardhi na tetemeko.

(f) Kutokea kwa janga la moto: Lava inaposambaa juu ya nyasi, huweza kusababisha muwako wa moto. Muwako huo unaweza kusababisha kutokea kwa janga la moto linaloweza kuunguza misitu na makazi ya watu, rejea Kielelezo namba 3 (c) na 3 (d).

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



3 (a)



3 (b)



3 (c)



3 (d)

**Kielelezo namba 3:** *Athari za mlipuko wa volkano*

**Vyanzo:** *https://www.vox.com/2018/5/6/17323626/hawaii-volcano-eruption-2018-kilauea-big-island*

*https://www.minnpost.com/earth-journal/2012/12/exploring-our-relative-capabilities-predicting-disasters*

*http://www.jpl.nasa.gov/*

(g) Athari kwa tabianchi: Majivu na gesi ya salfadioksidi hupunguza jotoridi duniani kwa kuakisi mwanga wa Jua. Pia mlipuko wa volkano unaweza kusababisha ongezeko la gesijoto angani, hivyo huchangia kusababisha mabadiliko ya tabianchi.

(h) Mawingu yatokanayo na majivu ya volkano na vumbi ni hatarishi kwa usafiri wa anga na huweza kuharibu injini za ndege.

Licha ya kwamba mlipuko wa volkano una athari nyingi, lakini pia una faida kama vile; kuzalisha udongo wenye rutuba na udongo mpya wa asili, pamoja



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 8 30/07/2021 11:58

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

na kumwaga vipande vidogovidogo vya madini kama dhahabu na almasi kutoka ardhini. Pia, mlipuko wa volkano huweza kusababisha kutokea kwa chemichemi za maji na kupatikana kwa visiwa baharini.

***Tahadhari za kuchukua katika kukabiliana na athari za mlipuko wa volkano***

Mlipuko wa volkano ni moja kati ya majanga ya asili ambayo yanahitaji umakini na maandalizi ya mapema kabla hayajatokea. Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine, itoe elimu kwa wananchi juu ya athari za mlipuko wa volkano. Wananchi waelimishwe kuhusu madhara ya kujenga makazi yao karibu na maeneo au milima yenye asili ya volkano. Inashauriwa kujenga au kuanzisha makazi umbali wa takribani kilomita 50 kutoka kwenye vyanzo vya milipuko ya volkano. Aidha, mamlaka zinazohusika zitoe tahadhari mapema kuhusu viashirio vya mlipuko wa volkano kabla ya janga kutokea.

Hata hivyo, endapo mlipuko wa volkano utatokea katika eneo unaloishi unashauriwa kukimbia na kwenda umbali mrefu ambako ujiuji wa volkano hautafika. Zingatia kuvaa barakoa (kichujahewa) ili usivute hewa yenye sumu itokayo katika moshi mzito wa volkano. Wakati unatembea kuelekea sehemu salama, epuka kukanyaga madimbwi ya maji au kupita katika mito na vijito vitokavyo milimani kwani huenda ukakanyaga ujiuji wa moto au maji ya moto yatiririkayo kutoka katika mlima unaolipuka volkano. Iwapo mlipuko wa volkano utatokea ukiwa ndani ya nyumba, unashauriwa kubaki ndani na kuhakikisha hakuna vitu vinavyoweza kukudondokea na kukudhuru hadi pale timu ya uokoaji itakapofika kukusaidia.

**Zoezi la 2**

**Jibu maswali yafuatayo:**

Chunguza Kielelezo namba 3, kisha jibu maswali yafuatayo:

(a) Unaona nini katika picha zilizoko kwenye Kielelezo namba 3?

(b) Ili kuepukana na athari za mlipuko wa volkano, unafikiri jamii inayohusika ilipaswa kuchukua tahadhari gani?

(c) Je, ni aina gani ya msaada unaohitajika kuwasaidia waathirika wa janga hilo kama inavyoonekana katika picha namba 3 (c)?

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 9 30/07/2021 11:58

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Maporomoko ya ardhi**

Maporomoko ya ardhi ni mmeguko wa ghafla wa mwamba au kipande cha ardhi kutoka katika mwinuko. Maporomoko ya ardhi huchochewa na nguvu ya uvutano. Kadiri mteremko unavyozidi kuwa mkali ndivyo kasi ya kushuka kwa mwamba au kipande cha ardhi inavyozidi kuongezeka. Kielelezo namba 4 kinaonesha maporomoko ya ardhi.



**Kielelezo namba 4:** *Maporomoko ya ardhi*

Maporomoko ya ardhi husababishwa na vyanzo mbalimbali kama vile mlipuko wa volkano, tetemeko la ardhi, mvua kubwa, na mafuriko. Mlipuko wa volkano husababisha kutikisika kwa tabaka la juu la ardhi na hivyo huweza kukatika na kuporomoka. Hii inachangia sana kutokea kwa maporomoko ya udongo kwani ardhi iliyotikiswa huwa dhaifu na yenye mikatiko na nyufa nyingi. Hali hii huifanya ardhi ya maeneo haya kuporomoka kirahisi. Aidha, mitetemo ya ardhi inapotokea huharibu muunganiko wa udongo na miamba. Ardhi huwa dhaifu, hivyo kuwa rahisi kuporomoka. Mafuriko pia



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 10 30/07/2021 11:58

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

huchangia kutokea kwa maporomoko. Kiwango cha maji yaliyoko ardhini kinapoongezeka kutokana na mvua kubwa au kuyeyuka kwa barafu, uzito wa udongo huongezeka na kushikamana kwake hupungua. Kadiri kiasi cha maji kinavyozidi kufyonzwa na kuongezeka katika udongo, hupunguza uwezo wa udongo kushikamana. Hali hii husababisha maporomoko ya ardhi kutokea. Nchini Tanzania maporomoko makubwa ya ardhi yaliwahi kutokea mkoani Kilimanjaro, wilaya ya Same na Morogoro wilaya ya Kilosa mnamo mwaka 2014.

***Athari za maporomoko ya ardhi***

Maporomoko ya ardhi yanapotokea huweza kuleta athari mbalimbali. Athari hizi ni kama zifuatazo:

(a) Uharibifu wa miundombinu, mali na makazi: Maporomoko ya ardhi huweza kuharibu na kuziba barabara (kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 5). Pia, huweza kuharibu reli, madaraja, nguzo za umeme na simu, mabomba ya mafuta na mifereji ya maji. Hali hii huweza kusitisha shughuli za uzalishaji mali kwa kipindi fulani. Aidha, maporomoko ya ardhi yanapotokea huweza kuharibu mali na makazi hivyo kuwaletea wananchi umaskini.

(b) Uharibifu wa mimea na vifo vya wanyama: Maporomoko ya ardhi yanapotokea huporomosha vifusi vya udongo ambavyo vinaweza kuwafunika wanyama na mimea katika maeneo ya bondeni. Hii huweza kusababisha vifo vya wanyama na kuharibu mimea katika eneo linalohusika.

(c) Kuondolewa kwa tabaka la udongo wenye rutuba: Maporomoko ya ardhi husababisha kuondolewa kwa tabaka la ardhi lenye rutuba na kurundikwa bondeni. Maeneo yaliyoondolewa tabaka la juu la ardhi hubaki bila rutuba hivyo kuathiri uoto na shughuli za kilimo. Hali hii huweza kusababisha kutokea kwa baa la njaa katika eneo linalohusika.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 11 30/07/2021 11:58

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kielelezo namba 5:** *Barabara iliyoharibiwa kwa maporomoko ya ardhi*

**Chanzo:** *https://www.123rf.com/photo_62062626_landslide-on-a-national-road-in-sicily.html*

***Tahadhari za kuchukua katika kukabiliana na athari za maporomoko ya ardhi***

Zipo tahadhari ambazo mtu anapaswa kuzizingatia ili kupunguza kiwango cha kutokea kwa maporomoko na kukabiliana na athari zake. Tahadhari zinaweza kuchukuliwa kwa kupanda miti na mimea mbalimbali katika maeneo ya wazi na yenye mteremko mkali. Pia, kuzuia uvunaji hovyo na uchomaji holela wa misitu. Wananchi kutofanya shughuli za ujenzi wa makazi kwenye maeneo yenye mteremko mkali na kwenye mabonde. Kwa sababu kwa kufanya hivyo huchochea kuongezeka kwa athari zitokanazo na maporomoko ya ardhi. Aidha, mamlaka zinazohusika zinapaswa kutoa elimu kuhusu athari zinazoweza kusababishwa na maporomoko ya ardhi na maeneo hatarishi. Pia, kuwahimiza wananchi kufuatilia vipindi vya utabiri wa hali ya hewa kupitia redio na televisheni ili kuchukua tahadhari stahiki. Wananchi wanapaswa kuzingatia sheria zinazohusu matumizi ya ardhi hasa katika maeneo yenye mteremko mkali. Mwananchi yeyote anapaswa kupata ushauri kutoka kwa wataalamu endapo atataka kuishi na kufanya shughuli za kibinadamu kama vile uchimbaji madini na kilimo kwenye maeneo yenye mteremko mkali. Pia, inashauriwa kufukia mashimo na kupanda miti mara baada ya shughuli za uchimbaji madini kukamilika ili kupunguza athari zinazoweza kutokea kutokana na maporomoko ya ardhi.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mara baada ya kutokea kwa maporomoko ya ardhi, unashauriwa kuzibua mifumo ya maji ambayo itakuwa imeziba kutokana na uchafu kama tope na taka nyingine ngumu zinazoletwa na udongo. Ondoa kifusi, miti au takataka nyingine kwa kusafisha eneo ambalo limeathirika ili kulirejesha katika hali yake ya awali. Sawazisha tope na mrundikano wa udongo ulioporomoka ili kupata msawazo wa ardhi husika. Tunashauriwa kurejesha makazi yaliyoharibika katika hali yake ya awali.

**Zoezi la 3**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza kwa kifupi athari zinazoweza kusababishwa na maporomoko ya ardhi katika eneo unaloishi.
2. Ni tahadhari zipi za kuchukua ili kuepuka athari zitokanazo na maporomoko ya ardhi?
3. Mafuriko, tetemeko la ardhi na mlipuko wa volkano vinachangiaje kutokea kwa maporomoko ya ardhi?
4. Eleza kwa kifupi viashirio vitakavyokujulisha kuwa kuna uwezekano wa kutokea kwa maporomoko ya ardhi.
5. Eleza ni kwa jinsi gani uchomaji wa misitu unachangia kutokea kwa maporomoko ya ardhi.

**Kazi ya kufanya namba 1**

Kwa msaada wa walimu, wazazi, au walezi bainisha majanga yaliyowahi kutokea katika mkoa unaoishi, kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo:

(a) eneo lilipotokea,

(b) aina ya janga,

(c) chanzo chake,

(d) athari zake, na

(e) jinsi lilivyokabiliwa.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Tsunami**

Tsunami ni neno la kijapani lenye maana ya “wimbi la bandarini”. Tsunami ni mawimbi makubwa ya bahari yanayosababishwa na tetemeko la ardhi chini ya sakafu ya bahari au mitikisiko mingine ya dunia kama vile milipuko ya volkano na kuanguka kwa vimondo baharini. Tsunami pia husababishwa na kupishana kwa eneo kubwa la sakafu ya bahari pamoja na ujaribishaji na matumizi ya mabomu ya nyuklia. Tetemeko la ardhi au mitikisiko mingine ya dunia husababisha kutokea kwa mawimbi makubwa baharini ambayo husafiri na kusambaa kwa kasi katika eneo kubwa la bahari. Mitikisiko hii inapotokea hutengeneza nguvu katika sakafu ya bahari ambayo husababisha mawimbi makubwa juu ya uso wa bahari. Mawimbi haya huanza kusafiri na kuongezeka nguvu kwa kasi kuelekea katika fukwe za bahari. Mawimbi ya tsunami yana nguvu na uwezo wa kusafiri kwa kasi ya kilomita 10 hadi 800 kwa saa, na huweza kudumu kwa wastani wa saa moja. Mawimbi haya huweza kufikia urefu wa mita 10 hadi 30. Tsunami inaweza kutokea muda wowote usiku au mchana. Bahari ya Pasifiki nchini Indonesia na Japan ni baadhi ya maeneo ambayo hupatwa na majanga ya tsunami mara kwa mara. Kutokea kwa matetemeko makubwa ya ardhi chini ya Bahari ya Pasifiki ndiyo chanzo kikubwa cha tsunami katika eneo hilo. Kielelezo namba 6 kinaonesha muonekano wa wimbi la tsunami.



**Kielelezo namba 6:** *Muonekano wa wimbi la tsunami*

**Chanzo:** *https://www.somagnews.com/tsunami-happen-tsunami-seen-occur*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

***Athari zinazotokana na tsunami***

(a) Vifo kwa wakazi na watumiaji wa maeneo ya fukwe za bahari: Mawimbi ya tsunami huathiri sana maeneo ya fukwe za bahari. Kwa mfano, tukio la tsunami ambalo ni kubwa kuliko yote yaliyowahi kurekodiwa, lilitokea katika bahari ya Hindi, Mashariki mwa Asia, mnamo Disemba 26 mwaka 2004. Tukio hili lilihusisha nchi kama, Indonesia, Singapore, Malaysia na India katika Bara la Asia, na linaloaminika kusababisha vifo vya watu zaidi ya 230 000 katika nchi 14. Athari hizi zilihusisha pia nchi za Afrika ya Mashariki ambapo takribani watu 11 nchini Tanzania na 1 nchini Kenya walipoteza maisha baada ya kusombwa na maji walipokuwa wakiogelea katika Bahari ya Hindi.

(b) Uharibifu wa makazi na miundombinu: Kutokana na mawimbi makubwa ya tsunami ambayo hugonga fukwe za bahari na kusambaa, maeneo ya makazi na miundombinu huathiriwa kama Kielelezo namba 7 kinavyoonesha. Hii ni pamoja na majengo ya makazi, hoteli na migahawa, vibanda vya huduma za utalii, barabara na viwanja vya michezo pamoja na maeneo mengine ya starehe. Pia, tsunami hubomoa reli na viwanja vya ndege pamoja na kuharibu vyanzo vya nishati ya umeme.

(c) Mafuriko na kuchafuka kwa vyanzo vya maji: Hali hii husababishwa na mawimbi makubwa ya maji yanayoletwa na tsunami katika fukwe za bahari. Maji haya husambaa na kujaa katika maeneo jirani na bahari na hivyo kusababisha mafuriko. Pia, maji haya huenea na kutuama katika maeneo mbalimbali ya makazi, hivyo kusababisha kuenea kwa magonjwa kama vile malaria, homa ya matumbo, kipindupindu na kuhara.

(d) Uharibifu wa makazi ya viumbe hai kama samaki na wanyama: Mawimbi ya tsunami yanapopiga katika maeneo ya kutagia mayai ya samaki kama vile matumbawe, huharibu na huathiri mazalia ya samaki. Hali hiyo inaweza kusababisha samaki kufa. Pia, mawimbi ya tsunami huweza kuharibu miundombinu ambayo inaweza kutiririsha sumu baharini na kuua viumbe wa baharini wakiwemo samaki. Kwa upande wa wanyama, tsunami inaweza kuathiri uoto ambao ni makazi ya wanyama na pia huweza kusomba wanyama na kufa.

(e) Kuharibu uoto wa asili: Mawimbi ya tsunami huweza kung’oa miti na mimea mingine. Hii husababisha kupoteza uasilia wa mwonekano wa eneo na hatimaye kuharibika kwa ikolojia katika eneo husika.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kielelezo namba 7:** *Athari za tsunami katika makazi ya watu*

**Chanzo:** *https//www.dw.com/en/climate-induced-sea-level-rise-to-worsen-tsunami-impacts/a-45730449*

### *Tahadhari za kuchukua katika kukabiliana na athari za tsunami*

Tsunami haitokei mara kwa mara, ingawa inapotokea huweza kusababisha maafa makubwa. Zipo tahadhari ambazo mtu anapaswa kuzizingatia ili kupunguza kiwango cha kutokea kwa tsunami na kukabiliana na athari zake. Moja ya tahadhari hizo ni kudhibiti urutubishaji, ujaribishaji, matumizi ya mabomu ya nyuklia na vilipuzi katika bahari. Hii itasaidia kupunguza kiwango cha matetemeko yatokanayo na shughuli za wanadamu. Epuka kujenga au kuishi maeneo ya kando ya fukwe za bahari. Kama ujenzi unafanyika basi uzingatie ushauri wa kitaalamu kuhusu umbali sahihi kutoka fukwe za bahari na kina sahihi kutoka usawa wa bahari. Mamlaka inayohusika wakiwamo wataalamu wa jiolojia watoe tahadhari pindi tu viashirio vya tsunami vinapojitokeza, kama vile, tetemeko la ardhi, na kupwa na kujaa kwa maji kusiko kwa kawaida. Hii iende sambamba na utoaji wa elimu kwa umma juu ya dalili za kutokea kwa janga la tsunami, madhara na jinsi ya kujikinga. Aidha, endapo tsunami imetokea katika eneo ulilopo, unashauriwa kujihifadhi kwa kusimama katika eneo lililoinuka. Kwa kufanya hivyo ni vigumu maji kukufikia na kukusomba, pia hurahisisha uokoaji. Epuka kujaribu kukatisha au kuogelea katika mikondo ya maji inayotiririka kurejea baharini, huenda mikondo hiyo ya maji ikawa bado ina nguvu na hivyo kukusomba.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 16 30/07/2021 11:58

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 4**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Tsunami ni nini?
2. Eleza chanzo cha kutokea kwa tsunami.
3. Eleza kwa nini maeneo ya karibu na bahari ya Pasifiki hukumbwa na janga la tsunami mara kwa mara?

## Majanga ya moto

Moto ni muwako ambao hutoa joto na mwanga. Moto pia huelezwa kuwa ni matokeo ya mgongano wa kikemikali kati ya kitu kinachoweza kuwaka, oksijeni na joto. Majanga ya moto ni miongoni mwa majanga yanayotokea juu ya uso wa dunia, ambayo hutokana na mlipuko wa moto. Majanga haya yamekuwa yakitokea sehemu mbalimbali duniani na kusababisha madhara makubwa katika jamii. Majanga ya moto yanaweza kuwa ya asili au yanayosababishwa na shughuli za kibinadamu. Majanga ya moto wa asili mara nyingi hutokea kwenye misitu minene mfano, msitu wa Amazon uliopo nchini Brazil na misitu ya upande wa Mashariki na Kaskazini Mashariki mwa jimbo la Victoria nchini Australia. Majanga haya hutokea hasa kipindi cha kiangazi ambacho huwa na joto kali. Chanzo cha moto wa asili chaweza kuwa milipuko ya volkano na umeme wa radi ambao ni chanzo kikubwa hasa katika maeneo ya misitu minene. Chanzo kingine cha moto wa asili ni joto kali kutoka angani ambalo husaidia moto kuwaka kwa urahisi. Umeme wa radi na joto kali kutoka angani husababisha kutokea kwa moto na kuunguza vumbi la mbao, majani makavu na nyasi. Moto huu huenea na kuchoma eneo kubwa la msitu.

Mbali na vyanzo vya asili, majanga ya moto pia husababishwa na shughuli za binadamu, kama vile; uchomaji wa makusudi wa misitu, urinaji asali kwa kutumia moto, shughuli za uwindaji, uvutaji hovyo wa sigara na matumizi yasiyo sahihi ya nishati ya gesi, mafuta na umeme. Moto unaosababishwa na shughuli za binadamu mara nyingi hutokea mashambani, misituni, shuleni, kwenye maeneo ya makazi na biashara. Mfano wa majanga ya moto ya aina hii, ni ule uliotokea mwaka 2017 na kuteketeza soko la SIDO mkoani Mbeya, na kusababisha hasara kubwa na uharibifu wa mali na majengo ya biashara kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 8 (a). Janga lingine la moto



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

lililosababishwa na shughuli za binadamu ni lile lililotokea mkoani Morogoro mwaka 2019 ambapo lori la mafuta lilianguka na kumwaga mafuta. Watu walipokuwa wakichota mafuta hayo ghafla kukatokea hitilafu katika mfumo wa umeme wa gari uliosababisha moto kulipuka na kusabisha vifo vya watu zaidi ya 100 na uharibifu wa mali na mazingira kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 8 (b). Mfano mwingine ni moto ulioteketeza shule ya sekondari Mihayo, mkoani Tabora mwaka 2018.



(a) Majengo ya soko la SIDO-Mbeya yakiteketea kwa moto



(b) Zimamoto wakizima moto Msamvu – Morogoro

**Kielelezo namba 8:** *Athari za moto.*

**Chanzo:** *Zimamoto na Uokoaji Tanzania*

**Zoezi la 5**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza jinsi urinaji wa asali usiofaa unavyoweza kusababisha janga la moto.
2. Umeme wa radi na joto kali vinasababishaje kutokea kwa janga la moto?
3. Eleza namna majanga ya moto yanavyotokea.

### Athari za majanga ya moto

Moto ni miongoni mwa majanga yenye uwezo mkubwa wa kusababisha madhara katika jamii. Zifuatazo ni athari za moto katika jamii:



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 18 30/07/2021 11:58

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(a) Husababisha vifo na ulemavu wa muda au wa kudumu kwa binadamu na viumbe wengine. Moto huathiri maisha ya binadamu na wanyama, kwa mfano, moto uliotokea Morogoro mwaka 2019 ulisababisha kupoteza maisha ya watu zaidi ya 100.

(b) Janga la moto huharibu mali na miundombinu kama vile, nguzo za umeme, visima vya mafuta na gesi, na kusababisha hasara kubwa miongoni mwa jamii husika. Moto uliotokea Morogoro mwaka 2019 ulisababisha kuungua kwa mali kama vile pikipiki, baiskeli na magari.

(c) Tabaka la juu la udongo kupoteza uwezo wa kufyonza na kuhifadhi maji kwa muda mrefu. Hii husababisha ardhi kuwa kame na yenye nyufa nyingi, hivyo kushindwa kuhifadhi maji. Ardhi hupoteza hali ya kushikamana na hivyo kuchochea mmomonyoko wa udongo na kutokea kwa maporomoko ya ardhi na mafuriko kwa urahisi.

(d) Kuongezeka kwa hewaukaa katika angahewa. Misitu inapoungua, hutoa moshi mzito wenye gesi ya kabonidioksidi ambayo huchangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa gesijoto angani zinazosababisha mabadiliko ya tabianchi.

(e) Kuharibu makazi ya wanyama pori na Bayoanuai. Majanga ya moto wa msituni huweza kuhatarisha maisha ya viumbe hai. Mfano mioto ya mara kwa mara kwenye hifadhi ya mlima Kilimanjaro na mbuga zingine za wanyama huharibu makazi ya wanyama na kusababisha vifo.

(f) Kusitishwa kwa huduma za kijamii kama shule, viwanja vya ndege, na hospitali. Hivyo, jamii husika huathirika.

(g) Kukosekana kwa ajira endapo mahali pa kazi patateketea kwa moto, mfano soko la Mwanjelwa na SIDO mkoani Mbeya, na soko la Samunge mkoani Arusha.

**Kanuni za kuzima moto na uokoaji**

Kwa mujibu wa sheria ya Tanzania namba 14 ya mwaka 2007 ya Zimamoto na Uokoaji, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lina wajibu wa kuzima na kuokoa maisha na mali, pamoja na kushughulikia dharura zozote ambazo si za kihalifu. Kanuni za uokoaji katika janga la moto zimetengenezwa kwa lengo la kusaidia pande mbili yaani, mwokoaji na mwokolewaji. Pamoja na hayo ili

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kufanikisha jukumu hili jeshi linashirikisha wananchi. Zifuatazo ni kanuni za kufuata ili kuokoa mali na maisha ya watu wakati wa janga la moto:

(a) Piga kengele, king'ora au mayowe kuomba msaada na kuashiria watumiaji wengine wa jengo waliomo ndani kuwa kuna moto.

(b) Toka nje na piga simu namba ya dharura ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ili kuweza kupata msaada zaidi. Namba hiyo ni 114.

(c) Inawezekana kuanza kuzima moto kwa kutumia vizimia moto vilivyopo endapo tu vinalingana na asili ya moto huo.

(d) Kumbuka kwamba, hairuhusiwi kuzima moto ambao chanzo chake ni umeme kabla ya kuzima swichi kuu. Iwapo imeshindikana kuzima swichi kuu tumia mchanga mkavu, mtungi wa hewa ya ukaa au poda kavu kuzima moto.

(e) Watu ambao hawashiriki katika uzimaji wa moto wanashauriwa kukaa sehemu maalumu ya kukusanyikia ili kuwezesha kufahamu kwa urahisi nani yupo na nani hayupo. Ni muhimu kuhakiki watu wote kama wapo ili kuwa na taarifa kamili punde waokoaji wa Zimamoto watakapowasili.

(f) Unapozima moto hakikisha mlango upo nyuma yako na uwe wazi ili ukishindwa kuzima moto uweze kutoka kwa urahisi.

(g) Moshi unapozidi, jaribu kutambaa kwa magoti na mikono ukiwa unaelekeza uso chini ili kuzuia moshi wenye sumu kuingia puani kwa wingi, ikiwezekana tumia kichuja hewa na vumbi (barakoa).

(h) Hairuhusiwi kurudi ndani ya jengo linalowaka moto kama hali bado si salama.

(i) Iwapo jitihada za kutoka nje zimeshindikana kabisa, funga mlango na ziba sehemu ya chini ya mlango kwa kutumia kitambaa kilicholowa.

(j) Simama kando ya dirisha na punga kitambaa cheupe kuashiria uwapo wako na kuomba msaada wa kutaka kuokolewa.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 20 30/07/2021 11:58

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 6**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza ni kwa nini wakati wote wa kuzima moto ndani ya nyumba unashauriwa mlango wa nyuma yako uwe wazi?
2. Orodhesha mambo manne ya kuzingatia wakati wa kuzima moto.
3. Unafikiri ni kwa nini tunashauriwa kuzima swichi kuu ya umeme kabla ya kuzima moto uliosababishwa na umeme?

**Namna ya kushiriki katika kuzuia janga la moto**

Katika kuzuia majanga ya moto, njia mbalimbali zimekuwa zikitumika kulingana na mahali na chanzo cha moto. Unashauriwa kuzingatia kanuni za kimazingira na tahadhari zilizowekwa ili kuepuka kusababisha moto. Mfano, uvutaji wa sigara katika maeneo hatarishi, kama vile kwenye vituo vya mafuta, maghala ya chakula, vyombo vya usafiri na katika misitu mikubwa. Pia vichungi vya sigara vyaweza kuzusha moto endapo havikuzimwa ipasavyo na kutupwa katika vyombo maalumu kwa ajili hiyo.

Ni vema kuhakikisha vifaa vyote vya umeme na gesi ni imara na vinafaa kwa matumizi kabla ya kuvitumia. Epuka kutumia vifaa vya umeme visivyo na ubora au vilivyochakaa. Matengenezo yote yanayohusu umeme na gesi yafanywe na mtaalamu anayehusika. Tunashauriwa kutumia vifaa vya umeme vilivyoidhinishwa na kutambulika kimataifa na kitaifa kwa ubora, mfano wa vifaa hivi ni kama, pasi, mtungi wa gesi, birika la umeme, simu za viganjani, redio, runinga na majokofu. Inashauriwa kufanya ukaguzi wa mfumo wa umeme kwenye majengo mara kwa mara.

Vilevile, unashauriwa kuwa makini na matumizi yote yanayohusisha moto ulio wazi kama vile mshumaa, kibatari na jiko la mkaa. Tunapaswa kuwa na vifaa kinga dhidi ya radi, vizimia moto na viashirio vya moto. Wakulima wanashauriwa kuepuka kuwasha moto shambani wakati wa upepo mkali na nyasi zikiwa kavu sana ili kuzuia moto kusambaa. Kuhakikisha uwapo wa miundombinu ya barabara au njia zinazorahisisha ufikaji wa eneo endapo moto utatokea. Elimu itolewe kwa jamii ili kufahamu wajibu na namna ya kukabiliana na janga la moto. Maeneo maalumu yatengwe kwa wafugaji ili kupata malisho ya mifugo yao kwa urahisi na kuepukana na tabia ya

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 21 30/07/2021 11:58

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kuchoma misitu ili kupata malisho ya mifugo yao. Elimu kuhusu urinaji bora na salama wa asali itolewe. Warinaji waelekezwe njia bora kama kutumia bomba la moshi au kifaa cha moshi kufukuza nyuki badala ya moto ambao ni hatari kwa mazingira.

Uchomaji holela wa taka pia ni chanzo cha moto, inashauriwa taka zichomwe katika maeneo maalumu, mbali na vitu vinavyoweza kushika moto kwa haraka kama gesi, mafuta, pumba za mazao na mabaki ya shughuli za useremala. Shughuli za uchomeleaji vyuma zifanywe kwa tahadhari mbali na vitu vinavyoweza kushika na kusambaza moto kama vile karatasi, mafuta, mbao na nguo. Vilevile, uchomaji wa mkaa upate kibali kutoka mamlaka inayohusika, pamoja na kupewa elimu ya kutosha jinsi ya kutumia teknolojia bora ya uchomaji mkaa. Wananchi waelezwe umuhimu wa kuzima mabaki ya moto baada ya kufukua mkaa au kupika. Moto wa mkaa huzimika taratibu hivyo ni muhimu kuzima mabaki hayo.

Kwa upande wa shule, kanuni hapo juu zinapaswa kuzingatiwa. Udhibiti wa kutumia mishumaa na vibatari unahitajika, pia kutoruhusu kutumia vifaa vya umeme kama hita kwenye mabweni au kujiunganishia umeme kiholela.

**Kazi ya kufanya namba 2**

Soma vyanzo mbalimbali vya taarifa kuhusu njia nyingine zinazoweza kutumiwa kuzuia kutokea kwa janga la moto mbali na zilizotajwa kwenye kitabu hiki. Kisha andika taarifa na uiwasilishe darasani.

**Zoezi la 7**

**Jibu maswali yafuatayo:**

**A. Chagua herufi ya jibu sahihi na uiandike herufi hiyo katika kisanduku.**

1. Seti ya mambo yafuatayo husababisha kutokea kwa mlipuko wa volkano;
   (a) mgandamizo, joto, na lava.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) nyufa, mgandamizo, na magma.

(c) nguvu ya msukumo, lava, na hewa.

(d) nguvu ya msukumo na mgandamizo wa hewa.

2. Moja kati ya njia zifuatazo **si** njia ya kuzuia kutokea kwa janga la moto;

(a) kutumia vifaa vilivyothibitishwa kwa ubora.

(b) matumizi mazuri ya mioto iliyo wazi.

(c) elimu kwa umma.

(d) kutumia moto wakati wa urinaji wa asali.

3. Mmeguko wa ardhi kufuata mteremko mkali huitwa ________.

(a) tetemeko la ardhi

(b) mmomonyoko wa ardhi

(c) maporomoko ya ardhi

(d) kuchimbika kwa ardhi

4. Mambo yafuatayo husababisha kutokea kwa janga la tsunami **isipokuwa** ________.

(a) mlipuko wa volkano

(b) kuanguka kwa vimondo baharini.

(c) tetemeko la ardhi

(d) mafuriko

5. Moja kati ya mambo yafuatayo ni sababu ya asili ya kutokea kwa moto msituni;

(a) kuchoma mkaa

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) umeme wa radi

(c) urinaji wa asali

(d) mila na desturi

**B. Andika KWELI kwa sentensi ya kweli na SI KWELI kwa sentensi isiyo ya kweli katika nafasi uliyopewa.**

6. Mlipuko wa volkano husababisha kufanyika kwa udongo wenye rutuba. __________

7. Maporomoko ya ardhi yanaweza kukabiliwa kwa upandaji wa miti. __________

8. Oksijeni ni hewa ya asili ambayo ikikosekana moto hauwezi kuwaka. __________

9. Uchomaji wa mkaa ni chanzo pekee kinachosababisha janga la moto katika misitu. __________

10. Kuongezeka kwa kiasi cha maji yaliyomo ardhini kutokana na mvua kubwa au kuyeyuka kwa barafu huchangia kutokea kwa mafuriko. __________

**C. Andika jibu sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi.**

11. Mambo matatu ya asili ambayo huweza kusababisha tsunami kutokea ni

    (i) ________________

    (ii) ________________

    (iii) ________________

12. Mmeguko wa ghafla wa miamba au udongo kufuata mteremko mkali ukisaidiwa na nguvu ya uvutano huitwa __________.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

13. Taja milima mitatu yenye asili ya volkano inayopatikana nchini Tanzania.

(i) _______________

(ii) _______________

(iii) _______________

14. Orodhesha athari tano zinazoweza kutokea kutokana na moto wa msituni.

(i) _______________

(ii) _______________

(iii) _______________

(iv) _______________

(v) _______________

**D. Jibu maswali yafuatayo**

15. Taja janga mojawapo la asili ambalo umewahi kusikia au kushuhudia likitokea. Toa majibu yako kwa kuzingatia yafuatayo:

(a) Eneo lilipotokea

(b) Chanzo au sababu ya kutokea

(c) Namna lilivyokabiliwa

(d) Athari zake kwa jamii inayohusika

(e) Funzo ulilolipata kutokana na janga hilo

16. Eleza kwa kifupi tofauti iliyopo kati ya majanga ya asili na yasiyo ya asili.

17. Unafikiri ni tahadhari zipi za kuchukua ili kuepuka athari za tsunami nchini Tanzania?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**E. Oanisha neno au kifungu cha maneno kutoka safu A na neno au kifungu cha maneno yaliyopo safu B kisha andika herufi ya jibu sahihi katika nafasi uliyopewa.**

| Safu A | Jibu | Safu B |
|---|---|---|
| 18. Tsunami | | (a) nguvu za asili na shughuli za binadamu |
| 19. Piga kengele au king'ora | | (b) moto wa asili<br>(c) lava |
| 20. Oldonyo lengai | | (d) mawimbi makubwa ya bahari yanayosababishwa na tetemeko la ardhi la chini ya bahari |
| 21. Umeme wa radi na joto kali | | (e) aina za majanga<br>(f) volkano tuli |
| 22. Tetemeko la ardhi na mlipuko wa volkano | | (g) hewaukaa kuongezeka<br>(h) Miamba iliyoyeyuka kwa joto kali chini ya ardhi<br>(i) TANESCO |
| 23. Athari za janga la moto | | (j) volkano hai<br>(k) moja ya kanuni ya kuzima moto na uokoaji katika janga la moto |
| 24. Magma | | |

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Jivu la volkano | jivu la moto litokanalo na mwako wa volkano |
| Lava | ujiuji wa moto unaotokea juu ya uso wa dunia baada ya mlipuko wa volkano |
| Magma | kimiminika cha moto mithili ya uji mzito, kinachotokana na kuyeyuka kwa miamba kwa sababu ya joto kali |
| Mwamba | jiwe kubwa kavu au jabali lililoko majini au nchi kavu au chini ya ardhi |
| Nishati | nguvu ya kuendesha mitambo au nguvu ya kufanya kazi |
| Nguvu ya uvutano | nguvu mbili zenye uelekeo tofauti |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Pili

# Maendeleo ya binadamu na zana za uzalishaji mali

**Utangulizi**

*Katika sura hii utajifunza dhana ya zana, Zama za Mawe, Zama za Chuma, na Zama za Teknolojia ya kisasa ya kidijitali na mchango wake katika maendeleo ya binadamu. Utajifunza pia, namna binadamu alivyobadilika kimaumbile sambamba na maendeleo yake ya kiteknolojia. Vilevile, utajifunza kulinganisha manufaa na upungufu wa matumizi ya zana za Mawe, zana za Chuma na zana za Teknolojia ya kisasa ya kidijitali. Utajifunza pia, mabadiliko katika maendeleo ya binadamu kiuchumi, kijamii na kiutamaduni, kutokana na ugunduzi na matumizi ya zana za Chuma. Aidha, utabainisha faida na athari za kutumia zana hizo. Maarifa na ujuzi utakaoupata katika sura hii utakusaidia kuchambua nafasi ya matumizi ya teknolojia katika kuendeleza jamii. Vilevile, utaweza kuhimiza matumizi ya teknolojia ya kisasa ya kidijitali katika uzalishaji.*

## Dhana ya zana

Zana ni kifaa chochote ambacho hutumiwa na binadamu ili kumwezesha kufanya kazi zake za kila siku. Binadamu, kwa nyakati mbalimbali, ameweza kubuni na kutengeneza zana kama vile visu, mikuki, majembe, mashoka na vifaa vingine vingi. Zana za kufanyia kazi zinaweza kutumika kulima, kukata, kufyeka, kuchonga, kujilinda, kusuka na kuwinda. Binadamu ameweza pia kubuni vyombo kama vikapu, vyungu na majokofu. Ubunifu na utengenezaji wa zana na vyombo mbalimbali umemwezesha binadamu kufanya kazi kwa ufanisi. Binadamu huishi kwa kuchangamana na kukabiliana na mazingira yake ili kuyaboresha na kuishi maisha bora zaidi. Kwa hiyo, ubunifu, uundaji na utumiaji wa zana ndicho kigezo kinachomtofautisha binadamu na wanyama wengine. Maendeleo ya binadamu yamebadilika kwa nyakati tofauti kutokana na zana alizotumia. Malighafi inayotumika kwa wingi kutengeneza zana ndiyo inayokitambulisha kipindi husika. Kutokana na muktadha huo tunapata vipindi mbalimbali vya maendeleo ya binadamu ambavyo ni; Zama za Mawe, Zama za Chuma na Zama za Teknolojia ya kisasa ya kidijitali.



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 27 30/07/2021 11:58

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zama za Mawe

Binadamu alianza kutengeneza na kutumia zana kwa mara ya kwanza katika Zama za Mawe. Alitumia zana hizo katika uwindaji wa wanyama na ndege, uchimbaji wa mizizi kuangua matunda kwa ajili ya chakula pamoja na kutengeneza mavazi yake. Kwa hiyo, Zama za Mawe zilianza mara binadamu alipoanza kutengeneza na kutumia zana za mawe.

### Zoezi la 1

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza kwa kifupi dhana zifuatazo:
   (a) Zana
   (b) Zama za Mawe
2. Bainisha matumizi matatu ya zana zilizotumika katika Zama za Mawe.

**Maendeleo katika Zama za Mawe**

Binadamu wa kale aliishi duniani yapata miaka 3 000 000 Kabla ya kuzaliwa Kristo (K.K). Katika kipindi hicho, binadamu aliweza kujenga historia ya maisha yake hapa duniani. Kwa uwezo wake wa kutumia akili, alivumbua mambo mengi ili kukabiliana na vikwazo ambavyo vingekwamisha maendeleo yake. Mathalani, alibuni na kutengeneza zana za kuzalisha mahitaji yake ya msingi. Mahitaji hayo ni chakula, makazi na mavazi. Uwezo wa kutengeneza zana sahihi na kuzitumia ndiyo unaomtofautisha binadamu na wanyama wengine waliomtangulia kama sokwe ambao wamekaa duniani kwa miaka 30 000 000 K.K. Historia inaonesha kuwa fuvu la kichwa cha binadamu wa kwanza liligunduliwa Kaskazini mwa Tanzania, wakati huo Tanganyika, katika Bonde la Oldupai mwaka 1959. Mgunduzi wa fuvu hilo alikuwa ni mtaalamu wa akiolojia aliyeitwa Dkt. Louis Leakey na mkewe Dkt. Mary Leakey.

Katika kipindi hiki binadamu wa kale alitumia mawe kutengeneza zana za kufanyia kazi. Utumiaji wa mawe kutengeneza zana ulijulikana kama Zama za Mawe. Zama ni kipindi fulani cha wakati katika maisha. Zama za Mawe zimegawanyika katika vipindi vitatu. Vipindi hivyo ni Zama za Mawe za Kale, Zama za Mawe za Kati na Zama za Mawe za Mwisho.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 28 30/07/2021 11:58

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zama za Mawe za Kale**

Zama hizi zilidumu kuanzia miaka 3 000 000 K.K hadi miaka 300 000 K.K. Katika kipindi hiki, binadamu aliishi kwa upweke. Watu walikuwa wachache sana na walikutana au kushirikiana kwa nadra. Kwa mfano, watu wachache walishirikiana kumfukuza mnyama hadi kumuua na kisha kula nyama yake. Baada ya hapo kila mmoja alirejea kwenye makazi yake. Daima walikuwa wakihamahama kutafuta chakula, maji na sehemu za kujihifadhi.

Zana zao zilikuwa duni na za matumizi ya muda mfupi. Kwa mfano, binadamu aliokota jiwe au kipande cha mti na kuangua tunda. Vilevile, alitumia mfupa wa mnyama kuchimba mizizi na wadudu kwa ajili ya chakula. Baada ya hapo alizitupa zana zake na kubeba mawindo ya mnyama, ndege, mizizi au matunda aliyoyapata. Zana hizi zilitumiwa pia kufukuza au kupigana na wanyama wakali waliowashambulia binadamu kama simba na tembo.

Wakati ule binadamu alifanana zaidi na sokwe ama nyani. Mwili wake ulikuwa na nywele nyingi na kichwa chake kilikuwa kidogo sana ukilinganisha na ukubwa wa mwili wake. Alitembea kwa mikono na miguu. Hivyo, hakuweza kubeba zana kwa muda mrefu. Kadiri muda ulivyopita alianza kutengeneza zana kwa kuchonga mawe ili kupata ncha na umbo alilolitaka. Kielelezo namba 1 kinamwonesha binadamu wa Zama za Mawe za Kale akitengeneza Zana za Mawe.



**Kielelezo namba 1**: *Binadamu wa Zama za Mawe za Kale akitengeneza zana kutokana na mawe*



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Hii ilimwezesha kupata vipande vidogovidogo ama vyenye ncha kali vilivyowiana na malengo yake. Kielelezo namba 2 kinaonesha maumbo ya baadhi ya zana za kipindi cha Zama za Mawe za Kale.



**Kielelezo namba 2:** *Zana za Zama za Mawe za Kale*

**Kazi ya kufanya namba 1**

Chunguza picha katika kielelezo namba 2. Kisha, wasilisha majibu yako darasani.

(a) Eleza kwa kifupi faida au manufaa unayodhani binadamu aliyapata kwa kutumia zana za mawe wakati wa Zama za Mawe za Kale.

(b) Bainisha changamoto unazodhani binadamu alizipata kwa kutumia zana kama hizo.

### Masalia ya zana za Mawe za Kale

Masalia ya zana za Zama za Mawe za Kale yamegundulika katika sehemu nyingi za Tanzania. Baadhi ya maeneo hayo ni Bonde la Oldupai mkoani Arusha, Isimila mkoani Iringa, Bonde la Mto Kagera mkoani Kagera na katika Wilaya ya Kondoa mkoani Dodoma. Kielelezo namba 3 kinaonesha baadhi ya maeneo yenye masalia ya zana za Zama za Mawe na michoro ya kale iliyogunduliwa.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




**Kielelezo namba 3:** *Baadhi ya sehemu zenye masalia ya zana za Zama za Mawe za Kale na michoro ya mapangoni*

Vilevile, katika maeneo kadhaa nchini Tanzania, ipo michoro ya kale ya mapangoni iliyochorwa na binadamu wa enzi hizo. Michoro kama hiyo inaonekana hadi sasa katika mapango ya Kondoa kama ilivyooneshwa kwenye ramani ya masalia ya zana za Zama za Mawe na michoro ya kale hapo juu. Inadhaniwa kwamba michoro hiyo ilikuwa na malengo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuwafunza watoto na vijana mambo muhimu katika jamii. Mfano, michoro hiyo ilionesha zana za kuwindia, mbinu za uwindaji, utamaduni wa jamii za kale na aina za wanyama katika mazingira yao. Kielelezo namba 4 kinaonesha baadhi ya michoro ya kale ya mapangoni iliyopo nchini Tanzania.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kielelezo namba 4**: *Baadhi ya michoro ya kale ya mapangoni iliyopo nchini Tanzania*

## Zoezi la 1

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza tofauti ya msingi iliyopo kati ya binadamu na wanyama wengine.
2. Unafikiri nywele nyingi mwilini zilimsaidiaje binadamu wa kale?
3. Masalia ya zana za Mawe za Kale yanakusaidiaje kufahamu binadamu wa kale alivyoishi?
4. Bainisha aina za michoro ya kale iliyopo mapangoni nchini Tanzania.

### Zama za Mawe za Kati

Kipindi hiki kilidumu kuanzia miaka 300 000 K.K hadi 50 000 K.K. Ni kipindi kilichoambatana na mabadiliko makubwa katika maisha ya binadamu. Kwanza, binadamu alianza kutembea kwa miguu. Mikono yake aliitumia kutengeneza vitu, kuokota, kushika na kutumia zana. Mabadiliko haya



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 32 30/07/2021 11:58

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

yaliambatana na mabadiliko muhimu mengine katika maumbile, mfano uwezo wa kufikiri na kufanya mambo mbalimbali. Mathalani, tofauti na sokwe ambaye alitembelea miguu minne, mabadiliko ya kimaumbile yalimuwezesha binadamu wa Zama za Mawe za Kati kuanza kutembelea miguu miwili akiwa wima. Hivyo, aliweza kuona mawindo na maadui kwa mbali kuliko wakati alipokuwa akitembea kwa miguu na mikono. Vilevile, uwezo wake wa kufikiri uliongezeka kadiri alivyokabiliana na mazingira yake. Kielelezo namba 5 kinaonesha jinsi maumbile ya binadamu yalivyoendelea kubadilika tangu alipoanza kutembea kwa miguu hadi sasa.



**Kielelezo namba 5:** *Hatua mbalimbali katika mabadiliko ya binadamu*

### Kazi ya kufanya namba 2

Chunguza kwa makini picha katika kielelezo namba 5. Kisha, fanya yafuatayo:

1. Bainisha tofauti mbili za kimaumbile kati ya picha ya sokwe aliyepo mtini na binadamu wa kale aliyepo mbele yake.
2. Eleza kwa ufupi tofauti tatu za muonekano wa binadamu wa kale, kwanza kushoto na kwanza kulia.
3. Fafanua umuhimu wa tofauti hizo katika maisha ya binadamu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Pili, ustadi na kasi ya kutengeneza zana viliongezeka. Katika hatua hii, binadamu wa kale alibuni na kutengeneza kwa ustadi zaidi aina nyingi za zana. Zana hizo zilikuwa bora, imara zaidi na za kufanyia kazi mahususi. Mifano ya zana hizo za Zama za Mawe za Kati ni mishale, uta, visu na shoka. Katika kipindi hiki binadamu alianza pia kuvaa ngozi za wanyama zilizolainishwa na zile zilizotokana na magome ya miti baada ya kuyapondaponda na kuyalainisha. Hata hivyo, aliendelea kuishi kwa kuhamahama na hakuwa na makazi ya kudumu. Kielelezo namba 6 kinaonesha baadhi ya mifano ya zana za Zama za Mawe za Kati.



**Kielelezo namba 6:** *Baadhi ya zana za Zama za Mawe za Kati*

**Kazi ya kufanya namba 3**

1. Chunguza kwa makini jembe la mkono linalotumika kulima shambani au kufanya usafi katika bustani, kisha, eleza namna unavyoweza kuliboresha ili kufanya kazi kwa urahisi.
2. Eleza kwa ufupi changamoto ulizokutana nazo katika shughuli hiyo.

***Ugunduzi wa moto***

Wakati binadamu akiboresha zana za mawe, binadamu aligundua moto, mwishoni mwa Zama za Mawe za Kati. Moto ulitokea wakati akigongagonga

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 34 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

na kusugua mawe ili kuyawekea umbo na makali aliyotaka. Mchakato huo ulizalisha cheche na moto ukawaka. Kadiri muda ulivyopita binadamu alipata ujuzi na mbinu anuwai za kutengeneza moto. Njia mojawapo ilikuwa ya kupekecha vijiti viwili vikavu, ambapo kipekecheo huitwa *ulindi* na kipande kinachopekechwa huitwa *uwimbombo.* Kielelezo namba 7 kinahusu utengenezaji wa moto katika Zama za Mawe za Kati.



**Kielelezo namba 7:** *Binadamu wa kale akitengeneza moto kwa kupekecha vijiti viwili vikavu*

***Umuhimu wa ugunduzi na matumizi ya moto***

Ugunduzi na matumizi ya moto ulileta maendeleo makubwa katika maisha ya binadamu. Kwa mfano, binadamu alianza kuchoma nyama na vyakula vingine ili kuvilainisha na kula kwa urahisi, badala ya kula vyakula vibichi. Vilevile, alichoma majani kufukuza wanyama wakali na kusafisha maeneo. Kuanzia kipindi cha Zama za Mawe za Kale binadamu alikuwa akiishi mapangoni. Hivyo basi, moto ulimwezesha kupata mwanga na kuongeza joto ndani ya mapango. Zaidi ya hayo, ugunduzi wa moto ulimwezesha binadamu kusafiri na kuishi katika sehemu zenye baridi kali duniani. Baadaye, moto ulisaidia kutengeneza gundi iliyotumika katika uvishaji wa vichwa vya mishale au mikuki kwenye mipini.



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 35 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya namba 4**

1. Chora jedwali la safu mbili za 'Zama za Mawe za Kale'' na ''Zama za Mawe za Kati''.
2. Katika kila safu onesha viashirio vitatu vya hatua za maendeleo alizopiga binadamu katika utengenezaji wa zana.

## Zoezi la 3

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja faida muhimu ya binadamu kutembea kwa miguu miwili. Kwa nini unafikiri hivyo?
2. Eleza faida za ugunduzi wa moto mwishoni mwa Zama za Mawe za Kati.

### Zama za Mawe za Mwisho

Kipindi hiki kilidumu kuanzia miaka 50 000 K.K hadi miaka 3 500 K.K. Kipindi hiki kiliambatana na ubunifu wa zana bora zaidi kuliko kipindi cha Zama za Mawe za Kati. Zana za zama hizi zilikuwa na kazi mahususi kama kuchuna ngozi za wanyama na kulima. Kielelezo namba 8 kinaonesha baadhi ya mifano ya zana hizo.



**Kielelezo namba 8:** *Zana za Zama za Mawe za Mwisho*

Binadamu alianza kuwekea mipini baadhi ya zana zake za mawe kama mashoka, mikuki na mishale. Mipini iliwezesha utumiaji wa zana kuwa na



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

tija kuliko iliyokuwa haina mipini. Kielezo namba 9 kinamwonesha binadamu amebeba zana zilizowekewa mipini.



**Kielelezo namba 9:** *Baadhi ya zana za Zama za Mawe za Mwisho zilizowekewa mipini*

Makazi ya binadamu wa Zama za Mawe za Mwisho yamegundulika katika mapango mbalimbali kandokando ya mito na maziwa. Maisha yao yamehusishwa pia na mabaki ya zana kama mawe mapana ya kusagia nafaka, mitego ya wanyama na mabaki ya mifupa mikubwa ya wanyama kama tembo na twiga. Inasadikiwa kwamba wanyama hao waliwindwa kwa kutumia mishale ya miti.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 37 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya namba 5**

Chunguza picha za Zana za Mawe katika Kielelezo namba 6 na kuzilinganisha na zana za mawe katika Kielelezo namba 8. Kisha, fanya yafuatayo:

1. Eleza tofauti zilizopo baina ya makundi hayo mawili ya zana za mawe.
2. Wasilisha tofauti hizo darasani kwa majadiliano.

***Kuanza kwa ufugaji***

Zana za aina nyingi na bora zaidi za kipindi cha Zama za Mawe za Mwisho zilimwezesha binadamu kufanya kazi mbalimbali katika kukabiliana na mazingira yake. Miongoni mwa mafanikio ya zana za Zama za Mawe za Mwisho ni kuwa binadamu alianzisha ufugaji wa wanyama na ndege kwenye makazi yake ili kurahisisha na kuongeza upatikanaji wa mavazi na chakula kama nyama, ngozi na maziwa. Aidha, mbwa alikuwa ni miongoni mwa wanyama wa mwanzo kufugwa na binadamu wa kale. Hivyo, ufugaji ulimuondolea binadamu wa kale utegemezi mkubwa wa wanyama na ndege pori katika kujipatia mahitaji muhimu ya maisha.

***Kuanza kwa kilimo***

Moja ya matokeo ya ufugaji mwishoni mwa Zama za Mawe za Mwisho ilikuwa ni kuanzisha makazi ya kudumu. Binadamu alilazimika kwenda kutafuta chakula na kisha kurudi katika makazi yake. Makazi ya kudumu yaliambatana na kuotesha au kupanda mazao ya chakula. Kwa hiyo, ufugaji wa wanyama na kilimo yalikuwa mapinduzi makubwa katika maisha ya binadamu. Baadhi ya viashirio na umuhimu wa mapinduzi ya kilimo na ufugaji katika maendeleo ya binadamu mwishoni mwa Zama za Mawe za Mwisho ni:

(i) Binadamu aliweza kupata chakula cha kutosha na ziada. Hivyo aliacha kutumia muda wake mwingi kutafuta wanyama, ndege, mizizi na matunda;

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 38 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(ii) Upatikanaji wa chakula kwa wingi uliongeza kasi ya kuzaliana na hivyo kuchochea ongezeko la watu;

(iii) Kuishi pamoja kulihimiza kuibuka kwa lugha, ikiwa kiungo muhimu cha mawasiliano baina ya wanajamii;

(iv) Ongezeko la watu katika makazi ya kudumu kulikuza ushirikiano na kuchochea kuibuka kwa uongozi katika jamii husika;

(v) Upatikanaji wa chakula cha kutosha uliwapatia binadamu hawa muda wa ziada ambao waliutumia kufanya kazi za sanaa na ufundi kama vile ufinyanzi, uhunzi, uchongaji wa vyombo anuwai na ususi;

(vi) Ulikuwa mwanzo wa mgawanyo wa kazi baina ya jinsi ya kike na kiume, baina ya rika za watoto, vijana na wazee; na

(vii) Jamii zilianza kuwa na makundi mbalimbali yaliyozalisha mali kama wawindaji, wavuvi, wakulima, wafinyanzi, wachongaji, wahunzi, wasusi na wafugaji. Hali hii ilisababisha wanajamii kubadilishana bidhaa ili kupata mahitaji au bidhaa wasizozalisha. Huu ulikuwa ni mwanzo wa biashara miongoni mwa wanajamii na jamii jirani.

**Ulinganisho wa maendeleo katika vipindi vya Zama za Mawe**

Katika kila awamu ya Zama za Mawe binadamu alipiga hatua muhimu za maendeleo. Hii ilitegemea sana uwezo wake wa kupambana na mazingira ili kuboresha maisha yake na kiwango cha upevu wa ubongo wake au uwezo wake wa kufikiri. Uwezo huu ulikuwa ukiongezeka kadiri alivyokuwa akifanya kazi na kuchangamana na mazingira yake, wakiwamo pia binadamu wengine. Jedwali lifuatalo linalinganisha tofauti za viwango vya maendeleo ya binadamu katika Zama za Mawe za Kale, Zama za Mawe za Kati na Zama za Mawe za Mwisho.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 39 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| Zama za Mawe za Kale | Zama za Mawe za Kati | Zama za Mawe za Mwisho |
|---|---|---|
| 1. Binadamu alianza kutengeneza na kutumia zana. Zana zilikuwa duni, chache na za hapo kwa hapo. Uwezo huu uliashiria mwanzo wa historia ya binadamu.<br>2. Maisha yalikuwa ni ya kuhamahama kutafuta chakula na makazi.<br>3. Aliishi mapangoni, porini na katika mabonde ya mito.<br>4. Alipata chakula kwa kuchimba mizizi, kuokota matunda na kutafuta wadudu na kuwinda ndege, wanyama na kuokota mayai. | 1. Binadamu alianza kutembea kwa miguu miwili.<br>2. Alitengeneza zana bora za mawe na za aina nyingi zaidi.<br>3. Aligundua njia za kutengeneza moto.<br>4. Alitengeneza mavazi kwa kulainisha ngozi za wanyama na kupondaponda magome ya miti. | 1. Binadamu alitengeneza zana bora zaidi za mawe, za aina nyingi na kwa matumizi mahususi.<br>2. Alianza kufuga wanyama na kulima mazao ya chakula.<br>3. Alianzisha makazi ya kudumu.<br>4. Alianza mgawanyo wa kazi kwa kuzingatia jinsi, umri na uwezo wa watu.<br>5. Wasanii na mafundi walianza kutokea miongoni mwa wanajamii. |

## Zoezi la 4

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza kwa kifupi uhusiano kati ya ufugaji na uanzishaji wa makazi ya kudumu katika Zama za Mawe za Mwisho.
2. Bainisha viashirio viwili vinavyoonesha jinsi kilimo kilivyoleta mapinduzi katika maisha ya binadamu.
3. Taja sababu za jamii kubadilishana mali walizozalisha hapo zamani.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Zama za Chuma

Zama za Mawe za Mwisho zilifuatiwa na Zama za Chuma. Zama hizi zilianza miaka 3 500 K.K na zinaendelea hadi sasa. Wakati huo ndipo binadamu aligundua chuma na kutengeneza zana za chuma. Udongo wenye chembechembe za chuma ulipashwa joto kali hadi kutoa majimaji ya chuma. Maji hayo yalikusanywa katika vyombo maalumu yakapozwa, kuganda na kupondwa ili kutengeneza au kufua zana anuwai za chuma. Kielelezo namba 10 kinaonesha wahunzi wakiwa kwenye mchakato wa kufua zana za chuma.



**Kielelezo namba 10:** *Wahunzi wakiwa kwenye mchakato wa kufua zana za chuma*

### Aina za zana za chuma na matumizi yake

Zana hizi zilikuwa imara zaidi, bora na za kudumu kuliko zana za mawe. Zana zilizotengenezwa ni kama vile shoka kwa ajili ya kukatia miti, kukatakata nyama na kufanya shughuli za ulinzi. Zana nyingine zilikuwa ni mikuki kwa ajili ya kuwinda na kujikinga na maadui na mishale iliyotumika kuwinda wanyama wakubwa na wadogo na kuwindia ndege. Aidha, ilifuliwa miundu

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kwa ajili ya kufyeka mimea na kusafisha maeneo ya kulima na kupanda mbegu za mazao anuwai. Vilevile, vilitengenezwa visu kwa ajili ya kuchuna wanyama na kukatia nyama. Pia, yalitengenezwa majembe kwa ajili ya kulima na kuchimba mizizi na wanyama wafukuao. Baadhi ya zana hizo zimeoneshwa katika Kielelezo namba 11(a) na 11(b).



**Kielelezo namba 11(a):** *Baadhi ya zana za chuma za kale zisizo na mipini*



**Kielelezo namba 11(b):** *Baadhi ya zana za chuma za kale zilizo na mipini*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya namba 6**

1. Chora jedwali lenye safu mbili katika daftari lako. Safu **A** ipewe kichwa cha, "Zana za chuma''. Safu **B** ipewe kichwa cha, "Matumizi yake.''
2. Orodhesha zana mojamoja katika safu **A** kisha andika matumizi ya zana hiyo katika safu **B**.

**Manufaa ya matumizi ya zana za chuma**

Zana za chuma zilikuwa na matumizi na manufaa mengi kwa binadamu wa kale kama vile:

*(a) Kupanua kilimo*

Umadhubuti wa zana za chuma uliwezesha binadamu kupanua kilimo kwa kufyeka, kulima na kupanda mazao katika maeneo makubwa zaidi. Aidha, watu walianza kufuga mifugo kama ng'ombe, mbuzi, kondoo na ndege kama kuku na bata.

*(b) Kuongezeka kwa idadi ya watu na uongozi wa jamii*

Upanuzi wa kilimo ulichangia kupatikana kwa chakula kingi na cha aina mbalimbali. Hivyo watu wakawa na afya, wakazaliana kwa wingi na vifo vitokanavyo na lishe duni vikapungua. Hali hii ilisababisha jamii kupanuka na hivyo kuwapo haja ya kuanzisha uongozi katika jamii husika.

*(c) Kuibuka kwa mafundi na wasanifu*

Baada ya kuwa na uhakika wa chakula watu walipata muda wa ziada kufanya kazi nyingine. Hivyo, waliibuka mafundi na wasanifu ambao walikuwa tegemeo la wazalishaji mali wengine kwa kuwatengenezea vitendea kazi muhimu. Mfano, wafinyanzi walifinyanga vyungu na mitungi. Kundi jingine ni la wasusi ambao walisuka majamvi, mikeka, vikapu na nyungo kwa matumizi ya wanakaya. Vielelezo namba 12 na 13 vinaonesha wasusi na wafinyanzi wa kale wakiwa kazini.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 43 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kielelezo namba 12:** *Wasusi wakisuka zana mbalimbali*



**Kielelezo namba 13:** *Wafinyanzi wa kale wakifinyanga vyungu kwa udongo*



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 44 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Vilevile, waliibuka mafundi ambao walitengeneza majembe ya wakulima, mikuki na visu kwa wawindaji na vinu vya kutwangia nafaka kwa kaya mbalimbali. Kielelezo namba 14 kinaonesha wachongaji wa zamani wakiwa kazini.



**Kielelezo namba 14:** *Wasanii wa kale wakichonga kazi ya sanaa*

*(d) Kuibuka kwa mgawanyo wa kazi na majukumu katika kaya na katika jamii*

Ongezeko la shughuli za uzalishaji mali katika kaya kulichochea haja ya kugawana kazi kwa kuzingatia jinsi, umri na rika. Hivyo, wanaume walifanya kazi za nguvu kama kuwinda, kusafisha mashamba, kulima na kulinda familia au jamii. Wanawake walifanya kazi za nyumbani kama kupika, kulea watoto, kutunza wazee na wagonjwa. Watoto wa kike waliwasaidia mama zao, ilihali watoto wa kiume walichunga mifugo na kusaidiana na baba zao.

*(e) Mwanzo wa kubadilishana bidhaa*

Uzalishaji wa ziada wa bidhaa za aina tofauti ndani na nje ya jamii mbalimbali vilichochea haja ya watu kubadilishana bidhaa ili kukidhi mahitaji yao. Huu ulikuwa mwanzo wa kufanya biashara baina ya wanajamii. Kielelezo namba 15 kinaonesha wanajamii wakiwa sokoni.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 45 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kielelezo namba 15:** *Wanajamii wa kale wakiwa sokoni*

*(f) Mabadiliko ya utamaduni*

Maendeleo yaliyotokana na matumizi ya zana za chuma, yalichangia kuleta mabadiliko katika utamaduni wa jamii husika, hususani katika mavazi na lugha.

*(i) Mavazi*

Watu waliboresha mavazi ya ngozi na magome ya miti na hivyo kujisitiri vizuri, kujipamba na kujikinga na baridi. Katika jamii nyingine wasanii walipondaponda magome magumu ya miti maalumu na kuyalainisha, kisha kutengeneza mavazi yaliyovaliwa na wanajamii. Kielelezo namba 16 kinaonesha mtawala wa kale na walinzi wake wakiwa wamevalia ngozi na



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 46 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

magwanda yaliyotokana na magome ya miti. Hatua hii iliboresha mavazi ya binadamu tofauti na zama zilizotangulia.



**Kielelezo namba 16:** *Mavazi ya ngozi na magome ya miti yaliyotumika na jamii za Watanzania*

*(ii) Lugha*

Kadiri jamii zilivyozidi kupanuka na uhusiano kuongezeka, lugha mbalimbali ziliibuka kuwezesha mawasiliano. Vivyo hivyo, uhusiano wa kubadilishana bidhaa kwa bidhaa ulisababisha kuibuka na kukua kwa lugha mbalimbali.

**Zoezi la 5**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja viashirio vitatu vinavyodhihirisha ubora wa zana za chuma kuliko zana za mawe.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Andika **KWELI** kwa sentensi ya kweli na **SI KWELI** kwa sentensi isiyo ya kweli, kisha toa sababu.

   (a) Uimara wa zana za chuma haukusaidia ukuzaji wa kilimo. __________

   Sababu: ______________________________

   (b) Chakula kingi kilichochea ongezeko la watu. __________

   Sababu: ______________________________

   (c) Mgawanyo wa majukumu katika kaya haukuwa wa lazima. __________

   Sababu: ______________________________

   (d) Watu wavivu ndiyo waliohitaji kubadilishana bidhaa. __________

   Sababu: ______________________________

   (e) Lugha zilirahisisha mawasiliano. __________

   Sababu: ______________________________

## Zama za Teknolojia ya Kisasa ya kidijitali

Hadi sasa tumeshaona mabadiliko ya binadamu katika kutengeneza zana za kumwezesha kufanya kazi na kuzalisha mali. Tumeshaona Zama za Mawe ambazo binadamu alitengeneza zana zilizotokana na mawe na kuzitumia katika shughuli mbalimbali. Zana hizo aliziboresha kwa vipindi vitatu yaani, Zama za Mawe za Kale, Zama za Mawe za Kati na Zama za Mawe za Mwisho. Zama za pili ni zama za chuma. Katika zama hizi binadamu alitengeneza zana bora zaidi na kupanua uwezo wa kuboresha maisha yake.

Sehemu hii itahusu zama ya tatu ambayo ni Zama za Teknolojia ya Kisasa ya kidijitali. Zama za Teknolojia ya Kisasa ya kidijitali ni mwendelezo na uboreshaji wa zama za chuma kwa kutengeneza kompyuta na mashine za aina mbalimbali. Mashine hizo ni pamoja na mashine za viwandani, injini za magari, treni, meli, ndege, matrekta na mashine za kurahisisha kazi za maofisini. Zama za Teknolojia ya kisasa ya kidijitali zimempa binadamu

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

uwezo wa kuzalisha mali kwa wingi na kwa muda mfupi na kurahisisha njia za usafiri. Zama za Teknolojia ya kisasa ya kidijitali zimeweza kurahisisha kazi za binadamu. Zama hizi za mashine na kompyuta zimemwezesha binadamu kugundua aina mbalimbali za teknolojia za kisasa. Angalia kielelezo namba 17 kinachoonesha matumizi ya teknolojia ya kisasa ya kilimo kwa njia ya trekta.



**Kielelezo namba 17:** *Kilimo cha kisasa kwa kutumia trekta*

Faida za kulima kwa trekta ni pamoja na kulima eneo kubwa, kupanda mbegu nyingi kwa mistari, kuvuna mazao mengi kwa haraka na hivyo kuokoa muda. Hata hivyo, kuna hasara katika kulima kwa kutumia trekta. Hasara hizo ni pamoja na kukandamiza ardhi, gharama kubwa za uendeshaji na kujaza moshi mwingi hewani na hivyo, huchangia uharibifu na uchafuzi wa mazingira.

### Zana za uzalishaji mali za sasa

Licha ya matumizi ya zana za Zama za Teknolojia ya kisasa, siku hizi zana za uzalishaji mali ni nyingi zaidi na zinatumiwa kwa njia na kazi tofauti. Mifano ya zana hizo ni zana zitumikazo kwa mikono na zana za kukokotwa na wanyama.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 49 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*(a) Zana zitumiwazo kwa mikono*

Kundi hili linajumuisha zana za kawaida kama mapanga, mashoka, majembe, nyundo na misumeno. Zana hizi zina manufaa na upungufu zinapotumika. Zana hizi zinapatikana kwa gharama ndogo na hivyo ni rahisi kununuliwa na watu wengi. Vilevile, ni rahisi kuzitumia. Upungufu wake ni pamoja na utendaji kazi kwenda polepole sana. Kwa mfano, kulima shamba kwa jembe la mkono kunamchosha mkulima na kutumia muda mrefu. Kwa upande mwingine, kukata miti kwa msumeno wa kawaida huchosha na huchukua muda mrefu. Hii ni tofauti na kukata miti kwa kutumia msumenonyororo unaotumia mafuta ya dizeli. Vielelezo namba 18 na 19 vinaonesha aina za misumeno.



**Kielelezo namba 18:** *Msumeno wa kawaida wa mkono*



**Kielelezo namba 19:** *Msumenonyororo*

*(b) Zana za kukokotwa na wanyamakazi*

Zana hizi ni plau, mkokoteni na toroli. Matumizi ya zana hizi ni mengi na yana faida nyingi. Kwa mfano, plau hutumika kwa kulima, mkokoteni hubeba

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mizigo na watu na toroli hutumika kwa kazi za kubeba mizigo. Kielelezo namba 20 kinaonesha mtu anayesafirisha mananasi kwa mkokoteni unaokokotwa na punda.



**Kielelezo namba 20:** *Punda na mkokoteni vikitumiwa kufanya kazi*

Hata hivyo, kuna upungufu katika kutumia zana hizi. Kwa mfano, zinabeba mizigo kidogo zikilinganishwa na malori. Vilevile, wanyamakazi huchoka, hususani mizigo ikiwa mizito kuliko uwezo wao. Kwa kawaida wenye wanyama hawa huwachapa ili watembee haraka au wavute mzigo kwa nguvu zaidi. Kitendo ambacho ni kinyume na haki za wanyama.

### Faida na athari ya kutumia zana za kisasa

Kama tulivyoona hapo juu, matumizi ya zana za kisasa yana athari chanya na athari hasi. Jedwali lifuatalo linaonesha hali hiyo:

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| ZANA ZA MKONO | B. ZANA ZA KUKOKOTWA NA WANYAMAKAZI | C. ZANA ZA MASHINE |
|---|---|---|
| **Faida** | **Faida** | **Faida** |
| 1. Ni rahisi kuzipata na kuzitumia.<br>2. Bei yake ni nafuu.<br>3. Rahisi kuzitunza. | 1. Kurahisisha kazi za kubeba mizigo.<br>2. Kurahisisha kulima, kupanda na kuvuna.<br>3. Kurahisisha usafiri na usafirishaji wa watu na mazao. | 1. Kufanya kazi kwa haraka na kwa viwango sahihi.<br>2. Kuokoa muda wa kazi.<br>3. Kuzalisha mali kwa wingi katika muda mfupi. |
| **Athari** | **Athari** | **Athari** |
| 1. Kazi hufanyika kwa kasi ndogo.<br>2. Watendaji kazi huchoka sana.<br>3. Kinachozalishwa ni kidogo. | 1. Hubeba mizigo ya wastani kuliko magari au malori.<br>2. Wanyamakazi huchoka na kuteseka.<br>3. Inabidi mwenye kazi kuwasimamia wanyamakazi muda wote wa kazi. | 1. Huchangia katika uchafuzi wa hewa na udongo.<br>2. Husababisha mkandamizo wa udongo.<br>3. Hutokea uharibifu wa uoto wa asili na vyanzo vya maji. |

**Kazi ya kufanya namba 7**

Tafakari faida na mapungufu ya kutumia kila aina ya zana za kisasa, hapo juu. Kisha, fanya yafuatayo:

1. Taja faida nyingine mbili kwa kila aina ya zana.
2. Taja athari nyingine mbili kwa kila aina ya zana.
3. Wasilisha majibu yenu darasani kwa majadiliano.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 6

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza kwa kifupi uwezo wa binadamu unaomtofautisha na sokwe.
2. Andika **KWELI** kwa sentensi ya kweli na **SI KWELI** kwa sentensi isiyo ya kweli, kisha toa sababu.

   (a) Katika Zama za Mawe za Kale binadamu alikuwa mpweke. ____________

   Sababu: ____________________________

   (b) Zana za Zama za Mawe za Kale zilikuwa za kudumu. ____________

   Sababu: ____________________________

   (c) Katika Zama za Mawe za Kale binadamu na sokwe hawakutofautiana. ____________

   Sababu: ____________________________

   (d) Michoro ya kale iliyopo mapangoni imesheheni mafundisho ya kihistoria. ____________

   Sababu: ____________________________

3. Taja faida nne za jamii za kale kuwa na mafundi na wasanifu.

   (a) ______________________________

   (b) ______________________________

   (c) ______________________________

   (d) ______________________________

4. Chagua jibu lililo sahihi zaidi kisha andika jibu hilo katika sehemu iliyoachwa wazi.

   (i) Binadamu alianza kutembea kwa miguu yake akiwa wima katika Zama za Mawe za ____________.

   (a) Kati

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) Kale

(c) Chuma

(d) Mwisho

(ii) Binadamu aligundua moto kwa kupekecha vijiti viwili vikavu vilivyoitwa ___________.

(a) mitiki na uwimbombo

(b) ulindi na mnazi

(c) mwanzi na ulindi

(d) uwimbombo na ulindi

(iii) Katika Zama za Mawe za Kale binadamu alipata chakula kwa njia ya ___________.

(a) kulima mazao ya chakula

(b) kufuga wanyama na ndege

(c) kuokota matunda, kuwinda wanyama na kuchimba mizizi

(d) kuvua samaki wa baharini

(iv) Mnyama wa kwanza kufugwa na binadamu alikua ___________.

(a) ng'ombe

(b) paka

(c) mbwa

(d) mbuzi

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Jaza katika jedwali matokeo chanya na matokeo hasi ya kutumia magari na pikipiki katika usafiri na usafirishaji.

| *Matokeo chanya ya kutumia magari na pikipiki* | *Matokeo hasi ya kutumia pikipiki na magari* |
|---|---|
| 1. Kusafiri haraka na kuokoa muda. | 1. Moshi wa injini kuchafua hewa. |
| 2. ____________________ | 2. ____________________ |
| 3. ____________________ | 3. ____________________ |
| 4. ____________________ | 4. ____________________ |
| 5. ____________________ | 5. ____________________ |

## Msamiati

Mahususi maalumu au pekee

Masalia mabaki ya kitu ambacho kilikuwepo kabla au wakati uliopita

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 55 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tatu

# Tabianchi ya Tanzania

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Sita, ulijifunza vipengele vya hali ya hewa ambavyo ni jotoridi, mgandamizo wa hewa, mvua, unyevuanga, mawingu na mwanga wa Jua. Pia, ulijifunza upimaji wa vipengele hivyo na kuchambua majira ya mwaka. Katika sura hii, utajifunza kuhusu dhana ya tabianchi na mambo yanayoathiri tabianchi ya Tanzania. Pia, utajifunza kanda za tabianchi ya Tanzania na sifa zake. Kadhalika, utaweza kuhusianisha kila kanda ya tabianchi ya Tanzania na shughuli za kiuchumi zinazofanyika katika kanda hizo. Aidha, utajifunza kuhusu mabadiliko ya tabianchi na utaweza kueleza namna mabadiliko ya tabianchi yanavyoathiri shughuli za kila siku katika ukanda husika. Maarifa na ujuzi utakaoupata katika sura hii, utakusaidia kuwa na uwezo wa kupanga na kufanya shughuli zako kwa kuzingatia tabianchi ya mahali husika.*

## Dhana ya tabianchi

Tabianchi ni wastani wa hali ya hewa inayochukuliwa na kurekodiwa kwa kipindi kirefu cha muda, kuanzia miaka 30 au zaidi. Hali ya hewa ina vipengele mbalimbali kama vile jotoridi, mvua, mwanga wa jua, upepo, unyevuanga, mawingu, na mgandamizo wa hewa. Vipengele hivi hurekodiwa kila mwaka kwa kipindi cha miaka 30 au zaidi. Wastani wa kila kipengele unakokotolewa kisha unagawanywa kwa miaka ambayo rekodi hizo zimechukuliwa. Kiwango kitakachopatikana ndicho hutumika kueleza tabianchi ya sehemu hiyo. Tabianchi inahusiana kwa karibu na hali ya hewa. Hali ya hewa ni hali ya anga katika sehemu fulani inayorekodiwa kwa muda mfupi mfano kwa saa, siku, wiki au mwezi. Hivyo, mabadiliko yoyote ya hali ya hewa kwa kipindi kirefu cha muda huchochea mabadiliko ya tabianchi ya sehemu husika.

Kutokana na uwapo wa maeneo tofautitofauti katika uso wa dunia, maeneo hayo hupata viwango tofauti vya jotoridi na mvua. Hali hii husababisha uwapo wa tabianchi zinazotofautiana katika maeneo mbalimbali. Pia, kuna

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

maeneo yenye tabianchi yenye kufanana, licha ya kuwa, maeneo hayo ni tofauti. Maeneo yote ya uso wa dunia yaliyo na jotoridi, unyevuanga, mwanga wa jua na mvua zinazofanana, huwa na uoto wa asili unaofanana. Pia, maeneo mbalimbali ya tabianchi inayofanana, watu wake huwa na shughuli za kiuchumi zinazofanana kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, maeneo yaliyo karibu na Ikweta kwa kawaida huwa na jotoridi la juu kwa kipindi cha mwaka mzima kuliko maeneo mengine, wakati maeneo yaliyo karibu na ncha za dunia; Kaskazini na Kusini huwa na hali ya ubaridi kwa takribani kipindi cha mwaka mzima. Hali hii hupelekea kuwapo kwa maeneo yenye tabianchi tofautitofauti ambayo huitwa kanda za tabianchi.

## Mambo yanayoathiri tabianchi ya Tanzania

Mambo muhimu yanayoathiri tabianchi ya Tanzania ni mwinuko, uoto wa asili, umbali kutoka baharini au ziwani, upepo, na latitudo kama ilivyo katika maeneo mengine yote ya uso wa dunia.

### *Mwinuko*

Tabianchi ya Tanzania ni ya kitropiki lakini huathiriwa na milima na miinuko hivyo kuwa tofauti katika maeneo mbalimbali. Maeneo yaliyo katika milima na miinuko huwa na baridi kali kuliko maeneo ya tambarare na mabondeni ambapo huwa na hali ya hewa ya joto na uvuguvugu. Hii ni kwa sababu kadiri mwinuko wa ardhi unavyoongezeka jotoridi hupungua. Mwinuko wa ardhi unapoongezeka kwa kila mita 100, kiwango cha nyuzijoto za sentigredi 0.6 hupungua. Tanzania iko katika mwinuko wa wastani wa mita 0 mpaka 5 895 kutoka usawa wa bahari. Maeneo yaliyoinuka zaidi kutoka usawa wa bahari kama mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Mbeya, Songwe, Njombe, Iringa, Morogoro, Rukwa na maeneo ya Lushoto mkoani Tanga huwa na baridi sana. Baridi inapozidi milima mirefu hufunikwa kwa theluji. Kwa mfano, kwenye kilele cha mlima Kilimanjaro wenye urefu wa mita 5 895 juu ya usawa wa bahari jotoridi ni chini ya nyuzijoto za sentigredi 0. Kiwango hicho cha jotoridi kimechangia kilele kuwa na theluji. Kutokana na mabadiliko ya tabianchi theluji katika mlima Kilimanjaro imeanza kuyeyuka kwa takribani asilimia 80. Aidha, maeneo ya tambarare na yenye mwinuko wa wastani kama mikoa ya Dodoma, Singida, Shinyanga, Simiyu, Mwanza na Tabora huwa na hali ya hewa ya joto la kadiri. Vilevile, maeneo ya pwani kama mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Tanga, Lindi na Mtwara huwa na hali ya tabianchi ya joto jingi na kiwango kikubwa cha unyevuanga.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mwinuko huathiri shughuli mbalimbali za kiuchumi. Mathalani, kilimo kwa baadhi ya mazao hufanyika kwa ugumu sana maeneo yenye miinuko mikali. Hali hii husababishwa na ukosefu wa rutuba na baridi kali ambayo hudhoofisha ukuaji wa baadhi ya mazao. Aina ya mazao yanayostahimili baridi hulimwa kwa wingi katika maeneo haya, mfano, kahawa, chai, pareto na migomba. Aidha, mteremko mkali huleta changamoto katika kutengeneza miundombinu mbalimbali, kama barabara, reli na njia za waenda kwa miguu. Hali hii hupunguza makazi, idadi ya watu na mwingiliano wa kibiashara. Maeneo ya tambarare na yenye mwinuko wa kadiri huwa na idadi kubwa ya watu, makazi na mwingiliano mkubwa wa kibiashara. Hii husababishwa na upatikanaji wa ardhi yenye rutuba, maji, miundombinu rafiki na ufikikaji wa maeneo mbalimbali.

***Uoto wa asili***

Uoto wa asili wa mahali pia huweza kuathiri tabianchi ya eneo linalohusika. Maeneo yenye misitu mikubwa kama Mufindi, Lushoto, Udzungwa, Njombe, Kibiti, Kibondo, na Biharamulo hupata mvua nyingi kwa kuwa mawingu hufanyika kwa urahisi kutokana na mvuke unaopatikana kutoka katika majani ya miti wakati wa usanisi na uvukishwaji. Maeneo hayo huwa na ardhi yenye rutuba ambayo hustawisha miti na aina nyingine ya uoto kwa wingi. Hii husababisha maeneo haya kuwa na mvua nyingi na joto kiasi. Hata hivyo, maeneo yenye uoto kidogo kama Dodoma, Singida, Shinyanga, Tabora na Simiyu hupata mvua kidogo kwa sababu ya kukosekana kwa uoto mwingi ambao ni chanzo cha mvua. Hali hii husababisha kuwa na uoto na mvua kidogo.

***Umbali kutoka baharini au ziwani***

Maeneo ya karibu na bahari au ziwa huwa na mvua nyingi kuliko maeneo yaliyo mbali. Sehemu za maziwa na bahari zina hali ya unyevunyevu na joto inayosababishwa na mwingiliano wa hewa za uvuguvugu na zile zilizopoa, hivyo hupata mvua mara kwa mara. Maeneo yaliyo karibu na bahari ni kama mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Mtwara, na Tanga. Maeneo yaliyo karibu na ziwa ni kama mikoa ya Mwanza, Kagera, Kigoma, Rukwa, Mara, Geita, Ruvuma, Njombe, na Mbeya. Mvua nyingi huweza kunyesha na kuongeza kina cha maji hivyo kusababisha mafuriko au tufani. Maeneo yaliyo mbali na bahari na maziwa hasa ukanda wa kati mikoa ya Dodoma, Singida, na Tabora huwa na mvua chache zinazosababisha hali ya ukame na nusu jangwa hivyo kuathiri shughuli za kilimo katika maeneo hayo.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 58 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

***Upepo***

Upepo unaovuma kutoka baharini au ziwani mara nyingi huleta mvua katika maeneo ya pwani. Upepo huu pia huleta hali ya hewa ya ukavu katika maeneo ya nchi kavu. Pepo za msimu za Kaskazini-Mashariki huleta mvua japo kidogo katika eneo kubwa la Kaskazini mwa Tanzania. Pia, pepo hizi huvuma sambamba na ukanda wa pwani. Kutokana na mabadiliko ya tabianchi, pepo hizi zimekuwa zikibadilikabadilika na kuleta madhara makubwa kwa shughuli za uvuvi na safari za majini. Pia, zimekuwa zikisababisha mafuriko.

***Latitudo***

Maeneo ya Ikweta na yaliyo karibu yake hupata miale ya Jua kwa wingi ukilinganisha na maeneo yaliyo mbali na Ikweta. Katika maeneo hayo, miale ya Jua hufika kwenye uso wa dunia ikiwa karibia pembe mraba. Hivyo, miale ya Jua hufika kwa wingi. Hali hii husababisha uwapo wa hali ya joto kwa muda mrefu katika maeneo hayo na hivyo huchangia katika ufanyikaji wa mvua. Hali ya joto pamoja na mvua katika maeneo hayo huchangia kwa kiasi kikubwa aina ya uoto wa maeneo hayo.

Tanzania inapatikana kati ya latitudo 1° na 12° Kusini mwa Ikweta. Hivyo, ipo karibu sana na Ikweta. Kutokana na kuwapo karibu na Ikweta, hupata miale ya jua kwa wingi katika mwaka na hivyo husababisha kuwa na vipindi virefu vya joto. Pia, pepo zinazovuma kutoka Kusini na Kaskazini huingia kutokana na kuwapo katika ukanda wa mgandamizo mdogo wa hewa, na hivyo pepo hizo kusababisha mvua.

## Kanda za tabianchi ya Tanzania na sifa zake

Kanda ya tabianchi ni eneo la kijiografia katika nchi, bara au dunia lenye tabianchi inayofanana. Nchi ya Tanzania kwa ujumla inapatikana katika ukanda wa tabianchi wa kitropiki kwa kuwa ipo kati ya Latitudo 1° na Latitudo 12° Kusini mwa Ikweta. Sehemu zote huwa za joto miezi ya Desemba, Januari, na Februari, kwa kuwa katika kipindi hiki Jua lipo kizio cha Kusini. Sehemu zote za nchi huwa za baridi katika miezi ya Juni, Julai, na Agosti kwa kuwa katika miezi hii Jua lipo katika kizio cha Kaskazini. Hata hivyo, sehemu za milimani huwa na baridi zaidi katika kipindi hicho kuliko maeneo mengine ya nchi.

Aidha, tabianchi ya Tanzania ambayo ni sehemu ya ukanda wa kitropiki imegawanyika katika kanda kuu nne za tabianchi zenye hali ya hewa

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

tofautitofauti. Kanda hizo ni kama zifuatazo: Ukanda wa pwani, ukanda wa nyanda za juu, ukanda wa kati, na ukanda wa ziwa. Kanda hizi zinatofautishwa kwa hali ya hewa inayopatikana katika maeneo hayo ambayo hutofautiana na sehemu nyingine. Hali hii husababisha eneo hilo kuwa na tabianchi ya pekee isiyofanana na zile za sehemu nyingine za nchi.

**Ukanda wa pwani**

Ukanda wa pwani hupatikana mita 0 mpaka mita 300 kutoka usawa wa bahari na unajumuisha mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, baadhi ya maeneo ya Tanga, baadhi ya maeneo ya Morogoro, Lindi na Mtwara kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 1. Pia, visiwa vya Unguja, Pemba na Mafia vipo katika ukanda huu. Hali ya hewa ya ukanda huu ni ya joto na unyevuanga mkubwa kwa mwaka mzima ingawa huwa na mabadiliko ya hapa na pale. Ukanda huu wa tabianchi kwa kawaida hupata mvua misimu miwili, mvua za masika na vuli. Mvua za masika hunyesha kati ya mwezi Machi na Mei. Hiki ndicho kipindi cha mvua kubwa. Msimu wa pili ni mvua za vuli ambazo hunyesha kati ya mwezi Oktoba na Desemba. Kipindi hiki hupata mvua kiasi. Mvua hunyesha kwa kiwango cha milimita 1 000 hadi 1 930 kwa mwaka.

Mwezi Juni hadi Septemba ni kipindi cha upepo mkali wa Kusini-Magharibi na baridi katika ukanda huu. Jotoridi hupungua hadi kufikia nyuzijoto za sentigredi 21. Hali ya jotoridi katika ukanda huu kwa wastani ni nyuzijoto za sentigredi 27. Joto kali huwa kati ya mwezi Desemba na Februari. Kiwango cha juu cha joto hufikia nyuzijoto za sentigredi 32. Pia, kipindi hiki upepo huvuma kwa kasi kutoka Kaskazini-Mashariki. Kwa ujumla ukanda huu una unyevuanga unaofikia kiasi cha asilimia 80.

**Ukanda wa nyanda za juu**

Ukanda huu una hali ya hewa ya baridi na joto kiasi. Ukanda wa nyanda za juu katika Tanzania unajumuisha safu za milima ya Usambara, Uluguru, Nguru, na Hanang'. Safu nyingine ni za milima ya Rubeho, Udzungwa, Kipengere, Rungwe, Ufipa na Livingstone kama Kielelezo namba 1 kinavyoonesha. Pia, ukanda huu unajumuisha maeneo ya milima ya Kilimanjaro na Meru. Maeneo yaliyo katika ukanda huu hupata mvua za masika zinazoletwa na pepo za Kaskazi. Pepo hizi zinapovuma huwa zina unyevu mwingi kutoka baharini au ziwani. Pepo hizi zinapovuka Ikweta hubadilisha njia na kuwa pepo za Kaskazini-Magharibi. Miezi ya Mei hadi Oktoba pepo za Kusini-



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Magharibi zinapovuma, ukanda huu huwa hauna mvua. Hali hii hutokana na upepo huu kupita maeneo yasiyokuwa na unyevu. Ukanda huu huwa na jotoridi la wastani na sehemu nyingine ni baridi kali sana kama vile Mufindi, Njombe, Lushoto na Rungwe. Maeneo haya hupata mvua nyingi inayonyesha hasa kuzunguka milima kiasi cha milimita 800 hadi 1 250 kwa mwaka. Kutokana na mwinuko katika maeneo ya ukanda huu, jotoridi huwa dogo kati ya nyuzijoto za sentigredi 14 na 20. Unyevuanga katika ukanda huu ni kati ya asilimia 58 na 65.

**Ukanda wa kati**

Ukanda huu una tabia ya nusu jangwa. Tabia hii hupatikana katikati mwa Tanzania katika mikoa ya Singida, Dodoma na Tabora kama inavyoonekana kwenye Kielelezo namba 1. Maeneo haya hupata mvua kiasi, chini ya milimita 500 kwa mwaka. Katika ukanda huu anga huwa lina mawingu kidogo. Katika kipindi kirefu cha mwaka joto ni kali wakati wa mchana, usiku huwa na baridi. Katika ukanda huu hewa ni kavu. Mwinuko katika ukanda huu ni mita 1 000 hadi 1 500 kutoka usawa wa bahari. Kwa sababu ya joto kali na mvua kidogo, maeneo ya ukanda huu huwa kame. Wakati mwingine hewa huwa yenye vumbi. Katika ukanda huu kuna tofauti kubwa ya joto kwa siku yaani joto la mchana na lile la usiku hutofautiana sana.

**Ukanda wa ziwa**

Ukanda wa ziwa huwa na hali ya hewa ya mvua nyingi. Ukanda huu upo upande wa Kaskazini na baadhi ya maeneo ya Magharibi mwa Tanzania. Mikoa iliyoko katika ukanda huu ni Mwanza, Mara, Kagera, Kigoma, Geita, Simiyu, na Shinyanga. Katika ukanda huu kuna mvua kati ya milimita 1 140 hadi 2 000 kwa mwaka. Eneo hili lina kiwango cha kawaida cha unyevuanga cha asilimia 70. Mvua hunyesha miezi minne ndani ya mwaka lakini katika miezi ya Aprili na Mei mvua hunyesha kwa wingi zaidi. Katika miezi hii kiwango cha chini cha unyevuanga huwa ni asilimia 33. Mashariki mwa ukanda huu, wastani wa mvua ni kati ya milimita 750 hadi 1 000 kwa mwaka wakati sehemu ya Magharibi inapata wastani wa mvua wa milimita 2 000 hadi 2 300 kwa mwaka. Jotoridi katika ukanda huu ni kuanzia nyuzijoto za sentigredi 27, pia tofauti ya joto kwa mwaka ni ndogo kiasi cha nyuzijoto za sentigredi 2. Maeneo yote ya ukanda huu hupata mvua nyingi inayoambatana na ngurumo na radi. Kielelezo namba 1 kinaonesha kanda za tabianchi ya Tanzania.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




**Kielelezo namba 1:** *Kanda za tabianchi ya Tanzania*

## Zoezi la 1

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Toa maana ya dhana zifuatazo:

   (a) Tabianchi

   (b) Hali ya hewa.

2. Kwa kutumia kielelezo namba 1, eleza kwa kifupi sababu za mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma, Ruvuma na Arusha kuwa na tofauti ya viwango vya joto.

3. Eleza kwa kifupi sababu za mikoa iliyopo katika ukanda wa ziwa kupata kiwango kikubwa cha mvua kwa mwaka.

4. Kwa nini maeneo ya ukanda wa ziwa huwa na udongo wenye rutuba kuliko mikoa ya ukanda wa kati?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kanda za tabianchi ya Tanzania na shughuli za kiuchumi

Mgawanyiko wa kanda za tabianchi ya Tanzania una uhusiano mkubwa na aina za shughuli zinazofanyika katika maeneo husika ya kanda hizo. Hivyo, shughuli za kiuchumi zinazofanyika katika eneo fulani, zina uhusiano mkubwa na hali ya hewa na tabianchi inayopatikana mahali hapo. Maelezo yafuatayo yanaonesha baadhi ya shughuli zinazofanyika katika kanda mbalimbali za tabianchi ya Tanzania:

Katika ukanda wa pwani wenye hali ya hewa yenye jotoridi kubwa na unyevuanga mkubwa, shughuli kuu za kiuchumi ni kilimo cha mazao kama vile; mpunga, mihogo, mkonge, korosho, miwa, nazi, na karafuu. Pia, shughuli za uvuvi na biashara hufanyika katika ukanda huu.

Katika ukanda wa nyanda za juu, shughuli kuu ni ufugaji na kilimo cha kahawa, mahindi, mihogo, mkonge, pamba, ulezi, mpunga, maharage na ufuta.

Aidha, shughuli kuu zinazotawala katika ukanda wa kati wenye hali ya hewa ya ukavu na joto ni kilimo cha mazao kama vile mtama, mahindi, mihogo, viazi vitamu, pamba, tumbaku, nyonyo, zabibu, ufuta na karanga. Mazao haya hulimwa kwa wingi katika ukanda huu kwa kuwa yanaweza kustahimili ukame. Pia, hufanya shughuli za ufugaji wa ng'ombe, mbuzi, kondoo na uvuvi wa samaki katika maziwa na mabwawa yanayopatikana katika eneo hilo mfano uvuvi katika bwawa la Mtera. Pia Mkoani Singida, kuna maziwa madogo kama Singidani na Kindai ambayo kuna uvuvi wa samaki kwa kiasi kidogo.

Katika ukanda wa ziwa wenye mvua nyingi watu wake hujishughulisha zaidi na shughuli za kiuchumi kama vile kilimo cha pamba, mihogo, ndizi, miwa, mpunga na mahindi. Pia, watu wa ukanda huu hujishughulisha na ufugaji wa ng’ombe. Vilevile, uvuvi ni shughuli kuu kwa wakazi wa maeneo haya kutokana na uwapo wa ziwa Victoria na ziwa Tanganyika.

Zifuatazo ni baadhi ya shughuli kuu zifanyikazo katika maeneo mbalimbali ya kanda za tabianchi ya Tanzania.

### Kilimo cha pamba ukanda wa ziwa

Asilimia kubwa ya pamba nchini hulimwa katika mikoa ya Mwanza, Geita, Shinyanga, Mara, Kagera, Simiyu, na Kigoma. Kwa kawaida pamba hustawi katika udongo wa kichanga, mfinyanzi na tifutifu. Pamba inahitaji mvua ya kutosha wakati wa kupanda na kukua. Kipindi cha jua kinahitajika wakati wa

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kuvuna. Wastani wa mvua inayofaa kustawisha pamba ni milimita 500 hadi 1 000, jotoridi kati ya nyuzijoto za sentigredi 20 hadi 28 baada ya kupandwa. Mkulima anashauriwa kuvuna pamba mapema ili isiharibike. Kielelezo namba 2 kinaonesha zao la pamba.



**Kielelezo namba 2:** *Pamba iliyokomaa tayari kwa kuvunwa*

**Chanzo:** *https://allafrica.com/stories/201708310161.html*

Mara tu baada ya kuvunwa pamba huchambuliwa. Mbegu za pamba husindikwa na kukamuliwa kisha kupata mafuta ambayo hutumika kwa kupikia, kujipaka na kulainisha mashine. Mashudu yanayobaki hutumika kutengeneza chakula cha wanyama kama ng'ombe, nguruwe na mbuzi. Pamba hutumika kutengeneza nguo, mito na magodoro. Pia, hutumika kama kifaa tiba katika hospitali. Zao la pamba huwanufaisha wakazi wa ukanda wa ziwa kwa kuwapatia vipato na malighafi ambazo huzitumia kutengeneza bidhaa mbalimbali. Pia, zao la pamba hunufaisha taifa kwa kujipatia fedha za kigeni na kujiletea maendeleo.

**Kazi ya kufanya namba 1**

1. Chora ramani ya Tanzania kuonesha maeneo yanayolimwa zao la pamba.
2. Taja hali ya hewa inayohitajika kwa ajili ya zao la pamba kutoka kupandwa hadi kuvunwa.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Kilimo cha kahawa ukanda wa nyanda za juu

Kahawa (au buni) ni zao ambalo hustawi vizuri katika sehemu zenye milima. Kuna aina mbili za kahawa ambazo hulimwa sana nchini Tanzania. Aina hizo za kahawa ni Arabika na Robusta. Kahawa aina ya Arabika hulimwa kwa wingi katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Mbeya na Ruvuma. Kahawa aina ya Robusta hulimwa katika mikoa ya Tanga, Morogoro, Manyara, na Rukwa. Ili istawi vizuri, kahawa inahitaji udongo wenye rutuba na usiotuamisha maji. Kahawa inahitaji joto la wastani wa nyuzijoto za sentigredi 17 hadi 23 na mvua kati ya milimita 1 016 hadi 1 500 kwa mwaka iliyotawanyika vizuri katika eneo husika kwa mwaka mzima. Kwa kawaida buni inahitaji kivuli cha miti mingine, hivyo sehemu nyingi kahawa hulimwa katika mashamba yenye miti michache iliyoinuka ili kupata kivuli kitakachoifunika. Kielelezo namba 3 kinaonesha zao la kahawa.



**Kielelezo namba 3:** *Zao la kahawa*

**Chanzo:** *https://mkulimamjasiriamali.wordpress.com/2019/03/08/kilimo-bora-cha-kahawa/*

Miche ya kahawa huoteshwa na kutunzwa kwenye kitalu kabla ya kupandikizwa shambani. Baada ya hapo miche huachwa ikue na kufikia urefu wa sentimita 20, halafu huhamishwa na kupandikizwa shambani. Mashimo yake huwa na upana na kina cha sentimita 60, pia huwekwa mbolea. Nafasi kati ya shimo moja na jingine ni mita mbili na nusu. Miti ya mikahawa

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ikishapandwa hutoa mazao (buni) baada ya miaka mitatu na ina uwezo wa kuzaa kwa muda wa miaka 30. Kahawa hulimwa kama zao la biashara. Zao la kahawa lina matumizi mengi. Matumizi hayo ni pamoja na kutengeneza vinywaji na vitafunwa. Kahawa pia hutumika kutengenezea unga maalumu unaotumika kusafisha ngozi, macho, na vyombo vya nyumbani.

**Zoezi la 2**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja sababu tatu za kahawa kustawi zaidi kwenye sehemu za milima na miinuko.
2. Orodhesha na ufafanue matumizi matano ya kahawa.

**Kazi ya kufanya namba 2**

1. Kwa kutumia vyanzo mbalimbali kama vitabu na kwenye mtandao tafuta taarifa zifuatazo kuhusu zao la kahawa:
   (a) Maeneo yanayolimwa kahawa;
   (b) Hali ya hewa inayofaa kwa kilimo cha kahawa; na
   (c) Namna ya kupanda, kutunza na kuvuna kahawa.

Andaa ripoti fupi kuhusu uchunguzi wako na uwasilishe darasani.

**Kilimo cha nazi ukanda wa pwani**

Minazi hutupatia tunda linaloitwa nazi kama zinavyoonekana katika Kielelezo namba 4. Nazi hustawi zaidi katika mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Tanga, Mtwara na Lindi. Nazi hustawi pia katika Visiwa vya Unguja na Pemba. Minazi hustawi katika maeneo yenye joto la wastani lisilopungua nyuzijoto za sentigredi 20 hadi 30 kwa mwaka. Minazi pia huhitaji mvua nyingi kiasi cha milimita 1 500 hadi 2 000 kwa mwaka. Udongo wa kichanga uliochanganyika na mboji hufaa kwa kilimo cha nazi.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY



**Kielelezo namba 4:** *Zao la nazi*

**Chanzo:** *https://www.habarileo.co.tz/habari/2019-08-075d4a7b4e1e1f6.aspx*

Minazi huoteshwa kwenye kitalu kwa muda wa miezi sita. Baada ya hapo huhamishwa na kupandikizwa kwenye mashimo ya duara yenye kipenyo na kina cha sentimita 90. Ni muhimu kuweka mbolea na kuacha mashimo wazi hadi wakati wa kupandikiza. Kwa kawaida nafasi kati ya shimo hadi shimo ni mita 10 kwa minazi mirefu na mita 3 kwa minazi mifupi. Minazi hutunzwa kwa kupaliliwa na kuzuia isishambuliwe na wadudu. Minazi huzaa nazi baada ya miaka 3 na pia kuendelea kuzaa hadi inapofikia miaka 50. Nazi hutumika kama chakula na kiungo katika mboga na vyakula mbalimbali. Minazi pia hutumika kutoa madafu ambayo maji yake ni kinywaji kinachosaidia kusafisha figo na kupunguza uzito. Pia, nazi hutoa malighafi za ujenzi, utengenezaji wa vifaa na samani mbalimbali.

## Zoezi la 3

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza sifa tatu za hali inayofaa kwa kilimo cha nazi.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Taja vitu vitano vinavyotokana na mnazi.

3. Eleza matumizi ya kila kitu ulichokitaja katika swali namba mbili.

**Kilimo cha mihogo katika ukanda wa ziwa**

Mihogo hustawi mahali popote penye ardhi yenye rutuba ikiwa na hali ya hewa ya joto na mvua ya wastani. Katika ukanda wa ziwa, mihogo hustawi zaidi katika mikoa ya Kigoma, Geita, Mwanza na Mara. Mikoa hii hupatikana katika ukanda wa ziwa ambapo hujumuisha maeneo ya ziwa Victoria na Tanganyika. Zao la mihogo linahitaji jotoridi la wastani lisilopungua nyuzijoto za sentigredi 10 na mvua kiasi wakati wa kupanda. Ustawi wa zao la mihogo unahitaji udongo wa kichanga, japo pia hulimwa katika maeneo yenye udongo wenye unyevu na unaohifadhi maji kidogo.

Mihogo hutumika kama zao la biashara, hivyo huwapatia wakulima fedha na mahitaji mengine muhimu. Mazao ya mihogo kama vile majani yake na mihogo yenyewe hutumika kama chakula. Majani hutumika kama mboga na mihogo hukaushwa na kutwangwa au kusagwa ili kupata unga wa kupikia chakula kama ugali, chapati, maandazi na uji. Watu wengi huchemsha mihogo na kula kama vitafunwa wakati wa kunywa chai. Mabaki ya mimea ya mihogo iliyovunwa hutumiwa kama mbegu na kuni. Wakulima hukata vipande vidogovidogo vya mimea ya mihogo na kuvipandikiza tena ardhini kisha baadaye huota na kuwa mimea ya mihogo. Mbegu za mihogo zinatakiwa ziachane kwa angalau mita 1 kutoka shina hadi shina na mita 1 kutoka mstari hadi mstari. Muachano huu hutoa nafasi kwa mti wa muhogo kustawi. Aidha, mihogo hutumika kama chakula cha mifugo na chanzo cha nishati endapo mabaki yake yataozeshwa na kutengeneza gesivunde. Kielelezo namba 5 kinaonesha shamba la mihogo.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 68 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kielelezo namba 5:** *Shamba la mihogo*

**Chanzo:** *https://www.ice.sua.ac.tz/suatv/index.php/en/habari/478-*

**Shughuli za ufugaji ukanda wa kati, nyanda za juu Kaskazini na ukanda wa ziwa**

Ufugaji ni moja kati ya shughuli kuu za kiuchumi nchini Tanzania. Shughuli ya ufugaji nchini hufanyika sana katika mikoa ya ukanda wa kati, ukanda wa ziwa na ukanda wa nyanda za juu Kaskazini. Katika kanda hizi ufugaji hufanyika katika mikoa ya Mwanza, Geita, Mara, Shinyanga, Simiyu, Dodoma, Singida, Tabora, Manyara na Arusha. Hali ya uoto wa nyasi asili, uwanda na mvua ya kiasi imechangia kwa kiasi kikubwa shughuli za ufugaji. Watu wengi hujishughulisha sana na ufugaji wa wanyama kama vile ng'ombe, kondoo, mbuzi, nguruwe na ndege kama kuku, bata, na kanga. Moja kati ya njia kubwa ya ufugaji inayotumiwa na wafugaji wa ng'ombe, kondoo na mbuzi katika maeneo haya ni ile ya kuchunga kwa kuipeleka mifungo malishoni asubuhi na kisha kuirudisha zizini jioni.

Baadhi ya makabila ya wafugaji ni Wamasai na Wabaribaig kutoka mikoa ya Manyara na Arusha; Wasukuma kutoka mikoa ya Mwanza, Geita,



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 69 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Shinyanga na Simiyu; Wanyamwezi kutoka mkoa wa Tabora na Wagogo kutoka mkoa wa Dodoma. Baadhi ya wafugaji hawana makazi ya kudumu hivyo huishi kwa kuhamahama wakitafuta malisho na maji kwa ajili ya mifugo yao. Faida za ufugaji kwa jamii ni kupata kitoweo kama nyama. Pia kupata maziwa, ngozi na fedha baada ya kuuza mazao yatokanayo na mifugo yao. Kwato za wanyama hutumika kutengeneza bidhaa mbalimbali kama soli za viatu. Mifupa na pembe hutumika kutengenezea vishikizo vya nguo. Ngozi hutumika kutengezea viatu, mikanda na nguo mbalimbali.

**Kazi ya kufanya namba 3**

Soma vyanzo mbalimbali kuhusu shughuli za ufugaji zinazofanyika katika maeneo mbalimbali kisha bainisha sifa za tabianchi zinazochangia shughuli hiyo kufanyika katika eneo linalohusika.

## Mabadiliko ya tabianchi ya Tanzania

Umejifunza kwamba tabianchi ni wastani wa vipengele vinavyounda hali ya hewa unaochukuliwa na kurekodiwa kwa kipindi kirefu cha muda wa miaka 30 au zaidi. Inapotokea kwamba wastani wa vipengele vya hali ya hewa umebadilika kwa kipindi kirefu cha muda katika misimu ya mahali ndipo tunaposema kuwa kuna mabadiliko ya tabianchi. Mathalani, kama jotoridi la mji "A" ni nyuzijoto za sentigredi 25, hii humaanisha kiwango hiki kilipatikana baada ya kuchukua wastani wa jotoridi la mji "A" kwa miaka 30 au zaidi. Wastani wa jotoridi ukikokotolewa tena kwa kuchukua rekodi za miaka 30 au zaidi na kuwa tofauti na nyuzijoto sentigredi 25 za awali, hiyo itamaanisha uwapo wa mabadiliko ya jotoridi katika mji "A". Hii ni ishara kuwa tabianchi ya mji "A" imebadilika. Lakini tabianchi sio jotoridi peke yake, bali pia yaweza kuhusisha mabadiliko katika wastani wa vipengele vingine vya hali ya hewa kama mvua. Jotoridi na mvua ni vipengele muhimu zaidi katika kutathmini mwenendo wa tabianchi.

Moja kati ya viashiria vya mabadiliko ya tabianchi ni kuongezeka kwa joto duniani. Joto linapoongezeka duniani husababisha mabadiliko ya wastani wa vipengele vya hali ya hewa. Kwa nini joto linaongezeka? Joto linaongezeka

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kwa sababu gesijoto zimezidi katika tabaka la juu la dunia. Mfano wa gesijoto hizo ni hewaukaa na methani. Je, uwapo wa hewaukaa na methani katika tabaka la juu la dunia unaongezaje joto? Mionzi ya jua inapotua ardhini huipasha ardhi joto, kisha ardhi nayo hurudisha joto hili katika angahewa na kisha kupanda juu mbali na uso wa dunia. Tabaka linaloundwa kwa gesijoto huzuia joto lisitoke katika uso wa dunia, hivyo kuendelea kuipasha dunia joto na hivyo kubadilisha hali ya hewa na kusababisha mabadiliko ya tabianchi.

Ni kwa nini basi hewaukaa na methani imeongezeka na kusababisha mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi? Sababu ni pamoja na kuongezeka kwa matumizi ya fueli za kisukuku, madini ya uraniamu, na makaa ya mawe. Fueli hizi zikichomwa zinatoa gesijoto ambazo zinaingia katika angahewa. Gesi hizi hupaa angani na kujikusanya kisha kutengeneza tabaka la gesijoto. Tabaka la gesijoto huzuia kutoka kwa miale ya joto iliyoakisiwa kutoka duniani ambayo hurudi tena juu ya uso wa dunia na kuongeza joto. Aidha, ukataji wa miti hovyo na uchomaji wa mkaa ni vyanzo vingine vya kuzalishwa kwa gesiukaa na methani. Miti hufyonza hewaukaa wakati wa kusanisi chakula chake na kutupatia hewa ya oksijeni. Hivyo, ukataji wa miti na uchomaji wa mkaa husababisha kuongezeka kwa hewaukaa angani na kupunguza kiwango cha oksijeni ambacho kingezalishwa. Vilevile, ufugaji wa mifugo mingi husababisha uzalishaji mwingi wa samadi ambayo hutoa hewa nyingi ya methani inayozuia joto kutoka katika uso wa dunia.

## Athari za mabadiliko ya tabianchi ya Tanzania

Mabadiliko ya tabianchi ya Tanzania yamekuwa ya kasi sana katika kipindi cha miaka thelathini ya hivi karibuni. Mfano, tumeona waziwazi ongezeko la joto, katika maeneo mengi ya nchi, mvua za juu ya wastani zinazonyesha tofauti na misimu ya mwaka tuliyoizoea, vipindi virefu vya ukame katika baadhi ya miaka, upepo mkali na kuongezeka kwa kiwango cha maji ya bahari ya Hindi. Mambo haya yote yameleta athari nyingi kwa watu, wanyama pamoja na makazi katika maeneo mengi nchini. Athari za mabadiliko ya tabianchi katika utekelezaji wa shughuli za kila siku nchini Tanzania ni kama zifuatazo;

### *Kubadilika kwa misimu ya mwaka*

Mabadiliko ya tabianchi ya Tanzania yamesababisha mabadiliko ya misimu ya mwaka katika maeneo mengi. Hii imeathiri kalenda na shughuli za kilimo na biashara katika maeneo hayo. Wakulima wamekuwa wakipata hasara

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kubwa kwa kuandaa mashamba na kupanda mbegu wakitegemea mvua kunyesha kwa wakati lakini kutokana na mabadiliko ya tabianchi mvua hazinyeshi kama ilivyotarajiwa, hivyo kusababisha hasara. Wafanyabiashara wamekuwa wakipata hasara kutokana na mabadiliko haya kwani hukusanya bidhaa kwa ajili ya kuuza katika msimu fulani lakini msimu huo huchelewa na kuja baada ya muda mrefu.

***Kuyeyuka kwa theluji katika mlima Kilimanjaro***

Theluji katika mlima Kilimanjaro imeyeyuka kwa zaidi ya asilimia 80 kati ya mwaka 1912 na mwanzoni mwa miaka ya 2000. Theluji hiyo bado inaendelea kupungua. Hii inatokana na kuongezeka kwa joto katika ukanda wa nyanda za juu na maeneo mengine ya nchi. Kuyeyuka kwa theluji kumesababisha kupungua kwa maji yanayotiririka kutoka mlimani katika maeneo mengi yanayozunguka mlima Kilimanjaro. Hali hii huweza kuathiri kilimo cha umwagiliaji.

***Kuongezeka kwa kina cha maji ya bahari***

Katika miaka ya hivi karibuni, Tanzania imeshuhudia kuongezeka kwa kasi kwa kina cha maji ya bahari ya Hindi na hasa kufunikwa kwa baadhi ya fukwe za sehemu za Visiwa vya Pemba na Unguja kwa upande wa Zanzibar na Mafia kwa upande wa Tanzania bara katika mkoa wa Pwani. Maji ya bahari yameongezeka kutokana na kuyeyuka kwa theluji katika ncha za dunia. Maji haya yanasababisha kumomonyoka kwa fukwe, makazi kuharibika na kuzama au kupotea kwa visiwa na matumbawe. Pia, ongezeko la maji baharini husababisha kuingia kwa maji chumvi katika maeneo ya nchi kavu yaliyopo pembezoni mwa bahari. Hali hii husababisha kupotea kwa mimea ya nchi kavu iliyo katika maeneo hayo. Hali hii huweza kuathiri shughuli za utalii.

***Kupotea kwa Bayoanuai***

Viumbe wanaoshindwa kuhimili ongezeko la joto huhama au kufa hivyo kuharibu msawazo asilia na ikolojia katika mazingira. Mfano viboko wengi katika mto Ruaha, mbuga ya wanyama ya Ruaha walikufa baada ya mto huo kukauka kutokana na hali ya ukame iliyosababishwa na mabadiliko ya tabianchi. Vilevile, mabadiliko ya tabianchi huvutia mimea vamizi ambayo huharibu msawazo wa asili na ikolojia ya eneo hilo. Hali hii pia inaweza kuathiri shughuli za utalii.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

***Kuongezeka kwa maradhi***

Moja ya athari ya mabadiliko ya tabianchi ni ongezeko la maradhi kama vile malaria, kipindupindu, maradhi ya shinikizo la damu na magonjwa ya kupumua. Ongezeko la joto Tanzania limesababisha ongezeko la ugonjwa wa malaria ambapo visa vya malaria vimekuwa vikiripotiwa maeneo ya baridi ya nyanda za juu kama vile Lushoto, Kilimanjaro na Njombe. Katika maeneo haya ugonjwa wa malaria haukuwa tatizo kabla ya miaka ya 2000. Kwa upande mwingine ongezeko la joto limekuwa likiwaathiri baadhi ya watu walio na maradhi ya upumuaji kama vile pumu na wenye matatizo ya shinikizo la damu. Pia, kwa miaka ya karibuni kumekuwa na ongezeko la visa vya kujirudia kwa maradhi ya kipindupindu. Mabadiliko ya tabianchi yanayohusisha kunyesha kwa mvua kwa wingi yamekua yakisababisha mafuriko na kuenea kwa maradhi ya kipindupindu nchini Tanzania.

***Kutokea kwa ukame***

Mabadiliko ya tabianchi yamekua yakisababisha kutokea kwa ukame. Ukame husababishwa na ukosefu wa mvua zinazotegemewa katika eneo fulani kwa muda mrefu. Katika miaka ya hivi karibuni, maeneo mbalimbali ya Tanzania kama vile Arusha, Shinyanga, Kilimanjaro, Dodoma, Singida, Simiyu, na Tabora yamekuwa yakikumbwa na ukame. Ukame husababisha madhara mengi ikiwa ni pamoja na uharibifu wa mazao, kufa kwa wanyama na mimea, kukauka kwa vyanzo vya maji na kusababisha baa la njaa na umaskini.

***Uharibifu katika kilimo na mifugo***

Mabadiliko ya tabianchi yamekua yakiathiri sekta ya kilimo na ufugaji kwa kiwango kikubwa. Miongoni mwa athari hizo katika kilimo ni pamoja na kuathiri misimu ya kilimo ya mwaka, kubadilika kwa maeneo ya ikolojia ya kilimo, mvua zisizo tabirika na vipindi virefu vya ukame, ongezeko la wadudu waharibifu wa mazao kama vile nzige na pia ongezeko la magugu yanayoathiri kumea kwa mazao. Pia, uwapo wa mvua za juu ya wastani husababisha mafuriko ambayo huathiri mazao. Athari ya matukio haya yanayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi husababisha uharibifu wa mazao na kusababisha upungufu wa chakula. Aidha, ukame unaotokana

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 73 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

na mabadiliko ya tabianchi umekuwa ukisababisha upungufu wa malisho. Hali hii husababisha mifugo kufa. Kielelezo namba 6 kinaonesha eneo lililokumbwa na ukame.



**Kielelezo namba 6:** *Eneo lililokumbwa na ukame*

**Chanzo**:*https://www.voanews.com/africa/less-severe-drought-forecast-horn-africa*

### *Kuharibika kwa miundombinu*

Uwapo wa mvua zinazonyesha juu ya wastani hasa zinazochangiwa na mabadiliko ya tabianchi zimekuwa zikisababisha uharibifu wa miundombinu mbalimbali. Mvua zinazonyesha juu ya wastani zimekuwa zikibomoa madaraja, barabara na kuharibu miundombinu ya umeme. Mfano, mwezi Machi 2020, daraja la Kiyegeya wilayani Kilosa, Mkoani Morogoro katika barabara iendayo Dodoma lilikatika na kusombwa na maji baada ya mafuriko yaliyotokana na mvua nyingi sana. Mara kadhaa, mvua nyingi kupita kiasi, zimekuwa zikiharibu miundombinu ya reli na kuathiri shughuli za usafirishaji. Kielelezo namba 7 kinaonesha daraja la Kiyegeya lililokatika.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kielelezo namba 7:** *Daraja la Kiyegeya lililosombwa na maji, mkoani Morogoro*

**Chanzo:** *https//www.eatv.tv/slider/naibu-waziri-wa-ujenzi-awasili-daraja-la-kiyegeya-lililosombwa-na-maji-morogoro*

**Jinsi ya kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi**

Tumeona kwamba shughuli za binadamu kwa sehemu kubwa husababisha mabadiliko haya ya tabianchi. Yapo mambo mbalimbali ambayo mwanadamu anaweza kufanya kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi. Baadhi ya mambo hayo ni kama haya yafuatayo:

(i) Kutoa elimu sahihi ya uelewa kwa jamii kuhusu changamoto za mabadiliko ya tabianchi. Elimu sahihi husaidia wananchi kufanya maamuzi sahihi ya namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na athari zake.

(ii) Kupunguza matumizi ya fueli za kisukuku kuendeshea injini za magari, mashine na mitambo ya viwanda. Vyanzo vya nishati mbadala kama vile nishati ya jua, gesivunde, gesi asilia, jotoardhi na nishati ya upepo vitumike.

(iii) Kudhibiti ukataji wa miti hovyo kwa kupunguza matumizi ya kuni na mkaa. Wananchi washauriwe kutumia gesi asilia na majiko sanifu ili kupunguza kiwango cha kuni na mkaa kinachotumika kupikia.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iv) Kupanda miti katika maeneo ya wazi na yaliyokatwa miti. Miti husaidia kuvuta hewaukaa iliyoko katika angahewa. Miti hii itapunguza hewaukaa na kutupatia hewa ya oksijeni ambayo huimarisha tabaka la ozoni na kutuepusha na ongezeko la joto duniani.

(v) Kutunza vyanzo vya maji na kutumia rasilimali maji vizuri na kwa ufanisi ili athari za ukame na kukosekana kwa mvua zisiwe kubwa zaidi.

(vi) Kupanda mazao yanayostahimili ukame na yale yanayokomaa kwa muda mfupi ili kuhakikisha upatikanaji wa chakula katika kipindi cha ukame. Inashauriwa pia kufuata kanuni bora za kilimo ili kuongeza uzalishaji hasa wakati wa mvua chache. Ni muhimu pia kuboresha uhifadhi wa mazao.

**Kazi ya kufanya namba 4**

1. Katika kikundi cha wanafunzi 4 jadilianeni namna ya kukabiliana na madhara yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi katika eneo mnaloishi, kisha wasilisheni darasani.
2. Kwa usimamizi wa mwalimu wa somo, tembelea mamlaka ya hali ya hewa kisha chunguza kiwango cha mabadiliko ya vipengele vya hali ya hewa kwa miaka mitano mfululizo. Bainisha kipengele kilichoathirika zaidi na kisha toa taarifa kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa ya eneo husika.

FOR ONLINE USE ONLY

**Zoezi la 4**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja vitu vitatu vinavyotengenezwa kwa kutumia zao la pamba.
2. Eleza jinsi tabianchi ya eneo au sehemu fulani inavyopatikana au kubainishwa.
3. Eleza kwa kifupi faida nne za kufahamu kanda za tabianchi ya Tanzania.
4. Eleza kwa ufupi vipengele vinavyotambulisha tabianchi katika mkoa wenu.



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 76 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Eleza kwa kifupi tabianchi iliyo katika mkoa unaoishi.
6. Je tabianchi hiyo inaathiri vipi shughuli zinazofanyika katika mkoa wenu?
7. Orodhesha mambo matatu uliyojifunza kuhusu ukanda wa nyanda za juu wa Tanzania.
8. Eleza kwa kifupi tofauti iliyopo kati ya tabianchi na hali ya hewa.
9. Eleza sifa nne za ukanda wa Pwani na shughuli kuu za kiuchumi zinazofanyika katika ukanda huu.

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Bayoanuai | aina mbalimbali za viumbe hai vilivyopo duniani ikijumuisha wanyama, bakteria, na kuvu |
| Fueli za kisukuku | fueli zinazopatikana chini ya ardhi ambazo hutokana na kujikusanya kwa mabaki ya viumbe hai kama wanyama, mimea kwa kipindi cha muda mrefu kama miaka 1 000 000 au zaidi |
| Gesivunde | gesi inayopatikana kutokana na mchanganyiko wa kinyesi cha wanyama au maganda na mabaki ya vyakula. Pia huitwa biogesi au bayogesi |
| Gesijoto | gesi zinazofyonza na kutoa miale ya Jua kwenye uso wa dunia au angahewa |
| Gesiukaa | ni gesi sumu, isiyo na rangi, ladha wala harufu. Gesi hii hutokana na kuchomwa kwa malighafi viwandani na fueli mbalimbali mfano, gesi asilia, fueli za kisukuku na makaa ya mawe. Gesi hii huitwa hewa ya Kabondioksidi |
| Ikolojia | uhusiano baina ya viumbe hai na mazingira yao |
| Kudu | kitita cha kamba ya mkonge |
| Matumbawe | miamba laini ambayo samaki hutagia mayai |

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 77 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nne

# Mila na desturi za Watanzania

## Utangulizi

*Ulipokuwa Darasa la Sita, ulijifunza kuhusu dhana ya utamaduni, ulichambua na kufafanua utamaduni wa Watanzania na umuhimu wa utamaduni katika taifa. Katika sura hii, utatathimini dhima na vipengele vya mila na desturi za Watanzania kabla ya ukoloni na jinsi ya kuendeleza utamaduni unaofaa. Utatathimini pia, madhara ya mila na desturi zisizofaa za Watanzania kabla ya ukoloni, hadi sasa na namna ya kuzitokomeza ili kujenga misingi ya maendeleo katika jamii. Maarifa na ujuzi utakaoupata katika sura hii utakusaidia kudumisha mila na desturi za Watanzania zinazofaa na kuacha zile zisizofaa.*



**Fikiri**

1. Kuhusu mila na desturi.
2. Kuhusu mila na desturi za Watanzania.

## Dhana ya mila na desturi

Mila ni utaratibu wa maisha ambao jamii imejiwekea na kila mwanajamii anapaswa kuufuata. Mila huwapa wanajamii mwelekeo na namna ya kuishi katika jamii. Mila ni mwenendo wa jinsi ya kufanya mambo kulingana na historia na utamaduni wa jamii husika. Kwa mfano taratibu za kufanya msiba na kuzika kwa heshima, vijana wa kiume na wa kike kuoana umri ukifika na taratibu za vijana kupata elimu kwa njia za jando na unyago. Wakati huo, desturi ni mwenendo au mfumo wa sheria ya jamii fulani uliozoeleka. Hivyo, desturi ni kanuni za jamii zinazotekeleza mila mbalimbali. Kwa mfano, kuzikana kwa heshima ni mila, lakini kanuni za uzikaji ni desturi. Vilevile,

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

elimu kwa njia ya jando na unyago ni mila, lakini kanuni zinazotumika katika kutekeleza jando na unyago ni desturi. Mila na desturi hujengwa na kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Mila huanza kama desturi, desturi huundwa na tabia ya mtu au kikundi fulani na kisha huenea katika jamii nzima. Desturi hizi zinapozoeleka katika jamii huathiri mila. Mila na desturi hizo pia zinaweza kupotea aidha kwa kuachwa au kupuuzwa. Hivyo, ni vyema jamii kuwa makini katika kudumisha na kuendeleza mila na desturi zinazofaa katika jamii. Aidha, ni vyema jamii kukemea mila na desturi mbaya zinazoanza na kutaka kuzoeleka katika jamii ili zisije kuathiri mila na desturi za jamii inayohusika. Kadiri muda unavyopita, ndivyo mila na desturi hupitwa na wakati na kushindwa kuendana na matakwa ya jamii. Hivyo, ni wajibu wetu kuachana na mila zisizofaa.

**Kazi ya kufanya namba 1**

Uliza mzazi au mlezi, kuhusu mila na desturi za kale za jamii yako na kisha:

1. Andika mila hizo katika daftari lako.
2. Taja mila zinazofaa kudumishwa kwa sasa.
3. Ainisha mila zisizofaa.
4. Elezea sababu ya mila hizo zisizofaa.

## Dhima ya mila na desturi

Mila na desturi huchukua sehemu kubwa katika utamaduni. Mila na desturi hubeba mapokeo ya mfumo mzima wa jamii inayohusika, kama vile, jamii inavyoishi, kushirikiana na kuhusiana na jamii nyingine. Mila na desturi pia, huonesha mienendo ya jamii, mfano imani, elimu, maadili, ujuzi, uzoefu, malezi, tabia na jinsi ya kujifunza na kuzifuata. Dhima ya mila na desturi ni muhimu kwani huleta utambulisho wa jamii, hutofautisha jamii moja na nyingine na pia huleta ustawi wa jamii na maendeleo ya taifa.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya namba 2**

Uliza mzazi au mlezi wako kuhusu mila na desturi za jamii yako katika malezi, maadili, tabia na kisha andika kuhusu:

1. Malezi katika jamii yako.
2. Maadili ya jamii yako.
3. Tabia na mienendo ya jamii yako.

## Dhima ya mila na desturi kabla ya ukoloni

Kabla ya ujio wa wakoloni, jamii za Watanzania zilikuwa na mila na desturi zake. Aidha, mila na desturi za jamii hizo zilitofautiana kutokana na kuwapo kwa mifumo tofautitofauti ya kiuchumi, kijamii, kiutawala na kimazingira. Dhima za mila na desturi za jamii hizo zililenga katika kukuza uchumi, kujenga maadili na tabia njema pamoja na kutoa mafunzo ya imani na elimu katika jamii inayohusika. Dhima hizi pia zilikuwa na lengo la kuweka taratibu za maisha katika jamii hizo. Dhima ya mila na desturi kabla ya ukoloni zilikuwa na malengo yafuatayo:

(i) Kuenzi na kuhimiza tabia njema;

(ii) Kuhimiza jamii kufanya kazi kwa bidii. Kazi ilikuwa ndiyo msingi wa maendeleo;

(iii) Kuhimiza usawa katika uzalishaji, mgawanyo wa rasilimali na umiliki wake;

(iv) Kuhimiza tabia ya kuheshimu na kujali utu wa mtu mwingine. Hii ilihimizwa ili kujenga tabia ya heshima na nidhamu katika jamii husika;

(v) Kuhimiza malezi bora katika jamii;

(vi) Kuthamini taaluma na teknolojia za jadi katika kuleta maendeleo ya jamii husika;

(vii) Kuijengea jamii uwezo wa kujiendeleza kimaisha kwa kuzingatia taratibu na kanuni za jamii zao; na

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 80 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(viii) Kujenga tabia ya ushirikiano, mshikamano, udugu, uzalendo, upendo na moyo wa kusaidiana katika jamii.

Watu wazima walitumika katika kufundisha, kuelekeza na kurithisha vijana na watoto mila na desturi za jamii husika. Machifu walikuwa ni wahamasishaji na wasimamizi wakuu wa mila na desturi katika jamii zao.

## Vipengele vya dhima ya mila na desturi kabla ya ukoloni

Dhima ya mila na desturi kabla ya ukoloni ziligawanyika katika vipengele mbalimbali ambavyo ni maadili na tabia njema, elimu, malezi na makuzi, pamoja na imani na dini.

### Dhima ya mila na desturi katika kujenga maadili na tabia njema

Mafunzo katika kujenga maadili na tabia njema yalisisitiza mambo yafuatayo:

(i) Utunzaji wa wazee, watoto, walemavu na wasiojiweza. Jamii ilifundishwa kuhudumia watu wa makundi hayo;

(ii) Uwajibikaji na kufanya kazi kwa bidii. Uvivu na kutokupenda kazi vilikemewa katika jamii zote. Watu waliaswa kupenda na kufanya kazi;

(iii) Kuheshimu wazee na watu wakubwa kiumri. Watu wenye umri mkubwa katika jamii waliheshimika na kuaminika kuwa na maarifa kuliko wale wenye umri mdogo. Mfano, wazazi waliitwa kwa majina ya watoto wao, Mfano, Mama Maliganya, Baba Lugane ili kuwapa heshima kama wazazi;

(iv) Kushirikiana katika mambo yote ya furaha na huzuni, kama vile harusi na misiba;

(v) Kukirimu wageni. Jamii zetu tangu awali zilikuwa zikisisitizwa kupenda na kusaidia wageni;

(vi) Kujenga uhusiano mwema katika jamii. Malumbano ya moja kwa moja yalikemewa; na

(vii) Kuheshimu imani za jadi, maeneo ya matambiko na vitu vya matambiko.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 81 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya namba 3**

Uliza mzazi au mlezi kuhusu maadili ya jamii yenu na kisha:

(a) Taja mambo yaliyosisitizwa kama maadili bora katika jamii.

(b) Eleza kwa ufupi jinsi ya kudumisha maadili bora katika jamii ya sasa.

### Dhima ya mila na desturi katika elimu

Dhima ya mila na desturi ilikuwa ni kutoa elimu kwa jamii. Elimu ililenga katika kufundisha na kurithisha uzoefu na maarifa ya jamii kwa vizazi vingine. Jukumu la kutoa elimu lilifanywa na watu rasmi katika jamii ambao walikuwa ni watu wazima, wazee na wenye maarifa. Hapakuwa na shule zilizotoa elimu kama ilivyo sasa. Vijana walifundishwa maarifa mbalimbali kuhusu vita, uwindaji, tiba asili, uhunzi, ufinyanzi, imani za jadi na historia ya jamii katika makundi rika, nyumbani na katika sherehe za jando na unyago. Elimu iliyotolewa ililenga katika:

(i) Tiba, hasa katika kujikinga na kutibu maradhi mbalimbali ya binadamu na wanyama;

(ii) Kuhimiza tabia ya ushirikiano, udugu na upendo;

(iii) Kusisitiza tabia ya kuheshimu utu na kufuata sheria;na

(iv) Kujilinda na majanga mbalimbali katika jamii.

Pamoja na jamii kuwa na dhima zinazofanana katika utoaji wa elimu, jamii zilitoa elimu kulingana na mila na desturi zake na mazingira yaliyowazunguka. Hii ilifanyika ili kuimarisha mfumo wa jamii, uchumi na mazingira ya maeneo walimoishi.

FOR ONLINE USE ONLY

**Zoezi la 1**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza dhima ya mila na desturi katika elimu kwa jamii ya sasa.
2. Fafanua jinsi elimu inavyotumika kuendeleza mila na desturi za jamii ya sasa.



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 82 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Dhima ya mila na desturi katika malezi na makuzi**

Malezi yalitolewa kuiwezesha jamii kushiriki katika kutekeleza itikadi za mila na desturi za jamii husika. Malezi yalitolewa tangu mimba ilipotungwa, mtoto alipozaliwa hadi alipofikisha umri wa kuvunja ungo au kubalehe na kutambulika kama mtu mzima. Malezi hayo yalilenga katika aina ya vyakula mathalani anavyopaswa kula mama mjamzito na vitu vya kufanya ili kupata mtoto mwenye afya bora na salama. Malezi na makuzi ya mtoto pia yalitolewa ili kumjenga mtoto katika maadili na tabia njema katika jamii. Familia ilikuwa ndio kitovu cha malezi katika jamii. Aidha, jamii nzima ilihusika katika makuzi ya watoto ili kupanua wigo wa mtoto kupata malezi bora. Vilevile, jamii nzima ilitambua jukumu la kuandaa na kukuza watoto wote kuendana na maadili mema ya jamii husika.



**Kazi ya kufanya namba 4**

Uliza mzazi au mlezi kuhusu yafuatayo:

(a) Eleza namna malezi yalivyotolewa katika jamii yako.

(b) Eleza kwa ufupi jinsi ya kudumisha malezi bora katika jamii kwa kuzingatia mila na desturi.

**Dhima ya mila na desturi katika imani na dini**

Imani na dini katika jamii za zamani zilijengeka katika misingi ya mila na desturi za jamii husika. Watu waliamini uwapo wa Mungu na miungu na kuwa ndiye mwenye nguvu na mtawala wa vitu vyote. Imani hizo zilisababisha watu kumfananisha Mungu na miungu au vitu vikubwa katika ulimwengu kama vile jua, milima mikubwa, mapango, mito na misitu. Watu waliamini Mungu ndiye anayetawala kila kitu na mwenye mamlaka ya mwisho kwa kila jambo kama vile mabadiliko ya hali ya hewa na maisha ya viumbe vyote. Hivyo, jamii zilifundishwa na kuamini katika imani za jamii yao. Jamii zilikuwa na utaratibu wake wa kufanya ibada. Ibada hizo ziliitwa matambiko. Matambiko hayo yalifanyika katika maeneo mbalimbali kama vile, makaburini, kwenye miti mikubwa, milimani, misituni, mapangoni, njia panda, ziwani, baharini, na kwenye mawe makubwa kutegemeana na aina ya tambiko. Matambiko hayo yaliongozwa na wazee au viongozi wa koo. Kwa mfano msitu wa

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Nyumbanitu mkoani Njombe, ni miongoni mwa maeneo maarufu ya ibada za matambiko kwa nia mbalimbali, nia hizo zilihusisha kupeleka maombi kwa Mungu kupitia mizimu ili kupata baraka, mvua, mavuno na pengine kuondoa mikosi au majanga katika jamii. Jamii pia ziliabudu kupitia mizimu ya kale. Watu walitoa sadaka wakati wa ibada kama vile wanyama, pombe na nafaka na kufanya matambiko kama sehemu ya mila na desturi. Jamii iliamini kutokufanya ibada kungesababisha matatizo na madhara katika jamii. Hata jambo baya kama vile, majanga yalipotokea jamii ziliamini ni sababu ya kutofanya ibada. Mila na desturi za ibada katika jamii zilirithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Katika jamii nyingine, matambiko yalihusisha sherehe za kimila kwa lengo la kutimiza ibada na pia kuwafunza watu maadili mema ya jamii husika kama sehemu ya ibada. Vilevile, watu waliaswa kutimiza na kufuata taratibu za ibada ili kuepuka kupata mikosi na balaa.

Imani za dini pia ziliambatana na matumizi ya dawa za jadi ili kutibu na kukinga magonjwa na maradhi mbalimbali. Huduma hii ilitolewa na wazee wa kimila, waganga na wakunga wa jadi kwa kutumia mitishamba na dawa nyingine za kutibu magonjwa mbalimbali. Aidha, waganga na wazee hawa wa kimila walifanya matibabu kwa kutegemea ibada za mizimu na ramli.

## Mila na desturi zisizofaa

Mila na desturi zisizofaa bado ni tatizo la jamii nyingi za Watanzania na Waafrika kwa ujumla, na ndiyo chanzo kikubwa cha ukatili na unyanyasaji wa kijinsia. Jamii ina wajibu wa kuangalia maendeleo ya sasa na kuamua kubadilika pale inapooneka kuna mabadiliko yenye tija kwa ustawi wa jamii. Aidha, pale jamii inapoona mabadiliko ya kimaendeleo yana dalili za madhara kwa jamii ni vyema kutobadili mila na desturi zetu. Hii haina maana ya kuacha mila na desturi kwa sababu ya maendeleo ya sayansi na teknolojia bali mabadiliko yafanyike iwapo tu yana tija. Baadhi ya mila na desturi zisizofaa za Watanzania kabla ya ukoloni hadi sasa ni kama vile; ukatili wa kijinsia, ukeketaji, watoto wa kike kuolewa katika umri mdogo, imani zisizofaa mfano ushirikina, mauaji ya vikongwe, mauaji ya watu wenye ualbino, kurithi wajane na imani za uchawi.

## Madhara ya mila na desturi zisizofaa katika jamii za Watanzania kabla ya ukoloni

Katika kipindi hiki jamii ziliamini sana mawazo na ushauri wa wazee hasa wale wa kimila na waganga wa jadi. Hali hii iliambatana na kuamini katika

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

imani zisizofaa kama vile upigaji wa ramli. Madhara ya mila na desturi zisizofaa yaliyopatikana wakati huu ni kama vile; vifo vilivyotokana na mauaji ya vikongwe, watu wenye ualbino na ukeketaji. Madhara mengine ni unyanyasaji wa kijinsia na kutengwa kwa watu wenye ulemavu au wenye mahitaji maalumu, mfano wakoma. Hivyo, watu wa aina hii walitengwa, walifichwa au hata kuuwawa katika baadhi ya jamii za Watanzania kwa sababu wanajamii waliamini kuwa kuishi na watu hao ni laana kwa jamii husika.

## Madhara ya mila na desturi zisizofaa katika jamii za Watanzania baada ya ukoloni

Licha ya kuwapo sheria zinazozuia na kutoa adhabu dhidi ya uendelezaji wa mila na desturi zisizofaa, bado mila hizo zinaendelea kuwapo kwa baadhi ya jamii. Mfano wa mila hizo ni ukatili wa kijinsia, ukatili wa kingono na ukeketaji ambapo waathirika hukumbwa na matatizo mengi ya kiafya hasa wakati wa kujifungua kama vile kutokwa na damu nyingi na hata kusababisha vifo. Hali hii inasababisha ukiukwaji  mkubwa wa haki za binadamu.

**Kazi ya kufanya namba 5**

Uliza mzazi au mlezi kuhusu mila na desturi zisizofaa za jamii yako na pia tumia maarifa uliyojifunza katika Darasa la Sita na kisha:

(a) Taja mila na desturi zisizofaa.

(b) Jadili na wenzako jinsi ya kukabili mila na desturi zisizofaa.

(c) Eleza jinsi ya kuondoa mila na desturi zisizofaa katika jamii ya sasa.

(d) Jadili na wenzako umuhimu wa imani za dini kwa jamii ya sasa.

## Njia za kutokomeza mila na desturi zisizofaa baada ya ukoloni

Jamii ya Tanzania kwa kutambua kuwa mhimili wa  nchi ni utamaduni wake, jitihada mbalimbali zimefanyika baada ya uhuru katika kuhimiza, kufuata na kudumisha mila na desturi zinazofaa. Mwaka 1962 serikali iliunda wizara iliyokuwa inasimamia masuala yote yaliyohusu utamaduni nchini. Serikali na asasi za kiraia zinaendelea kupambana na mila na desturi zisizofaa zinazokiuka haki za binadamu hususani kuhusu wanawake na watoto. Kimsingi, juhudi hizi zinazotekelezwa na asasi za kiraia kwa kuunga mkono

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

juhudi za serikali katika kuondoa ukiukwaji wa haki za binadamu kwa misingi ya jinsia ndani ya jamii. Asasi hizi pia zinasaidia kuhamasisha jamii na serikali za mitaa katika kukabiliana na ukiukwaji wa haki za wanawake, watoto, wazee na walemavu kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kujipatia maendeleo endelevu.

Jitihada mbalimbali za miradi inayofadhiliwa na asasi za kiraia, jumuiya za kimataifa, sambamba na serikali kwa ujumla zina lengo la kubadili mtazamo wa wanufaika wa miradi hiyo kuhusu mila na desturi zisizofaa. Mkazo pia umewekwa na asasi pamoja na wananchi kwa ujumla ili kuwawezesha waathirika kutoa taarifa za ukatili wa kijinsia kwenye vyombo mbalimbali vya sheria ili kuwalinda waathirika. Lakini pia, kuimarisha mifumo na miundo ya kitaasisi ili iweze kubaini na kushughulikia matatizo hayo.

Serikali inafanya kazi na asasi za kiraia kuwalinda na kuwatetea waathirika wa matukio ya ukatili katika jamii. Serikali kwa kushirikiana na asasi za kiraia, imeweka mikakati mbalimbali na mbinu zinazotumiwa katika kutokomeza mila na desturi zisizofaa, kama vile:

(i) Uhamasishaji katika jamii kupitia mikutano, maonesho ya njiani na kwenye maeneo ya watu wengi, kutoa elimu na ufahamu zaidi kuhusu athari za ukatili wa kijinsia, na aina nyingine za ukatili;

(ii) Kuwapa mafunzo ya kuwajengea uwezo wataalamu, viongozi wa mila, dini na wale wanaoendeleza mapambano dhidi ya mila zisizofaa katika maeneo yao;

(iii) Kujenga mtandao wa wadau wa kupinga ukatili wa kijinsia na kutumia taasisi na watu ambao ni mifano mizuri katika kuelimisha na kupinga ukatili wa kijinsia. Moja ya jitihada hizo ni uanzishwaji wa Mtandao wa Kijinsia Tanzania;

(iv) Kutoa elimu na hamasa kwa jamii kupitia vyombo vya habari kama vipeperushi, vipindi vya redio na televisheni, majarida na machapisho mbalimbali. Vilevile, kupitia michezo na maigizo katika matukio mbalimbali ya kijamii;

(v) Uundwaji na uendelezaji wa majukwaa ya kupinga ukatili wa kijinsia kwa njia ya vikundi vya watoto kama mabalozi wa kutetea haki zao; na

(vi) Kutoa elimu ya uraia juu ya haki za watu wenye ulemavu, watoto, haki za kina mama katika kupambana na mila na desturi zisizofaa nchini Tanzania.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Hivyo basi, kwa kutumia majukwaa ya kijamii ya kupinga ukatili wa kijinsia, ufuatiliaji na kutoa taarifa za matukio kwa taasisi husika, na kushirikisha sekta mbalimbali tutaweza kutokomeza ukatili wa kijinsia. Hatua hizi zikiungwa mkono na serikali tunaweza kujenga misingi ya maendeleo katika kudumisha mila na desturi zinazofaa katika jamii yetu.

## Zoezi la 2

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza jinsi vyombo vya habari vinavyoweza kuendeleza au kuharibu mila na desturi za jamii zetu.
2. Bainisha dhima za mila na desturi za jamii za Watanzania.
3. Taja mbinu zinazoweza kutumika katika kuendeleza mila na desturi zinazofaa.
4. Eleza jinsi ukoloni ulivyoathiri maendeleo ya mila na desturi za jamii zetu.
5. Taja harakati za kuendeleza mila na desturi za jamii baada ya uhuru.

**Andika KWELI kwa sentensi ya kweli na SI KWELI kwa sentensi isiyo ya kweli katika nafasi uliyopewa.**

6. Wakoloni walikuja kuendeleza mila na desturi za jamii zetu. __________
7. Wazazi na walezi wanaweza kusaidia kudumisha mila na desturi za jamii zetu kwa kizazi cha sasa. __________
8. Michezo na sanaa katika jamii ni nyenzo muhimu katika kukuza na kuendeleza mila na desturi nchini. __________
9. Matumizi ya dawa za kulevya, uasherati, ulevi na uvivu ni maendeleo ya mila na desturi nchini. __________
10. Kitendo cha kuiga tabia zote zinazoibuka katika jamii bila kujali madhara yake ni kuendana na wakati. __________

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tano

# Usafirishaji na uhusiano wa Tanzania na nchi nyingine

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Sita, ulijifunza maana ya uhusiano na maeneo ya uhusiano wa Tanzania na nchi za Afrika baada ya uhuru. Ulijifunza pia sababu za kuwa na uhusiano pamoja na njia zinazotumika kuanzisha na kuimarisha uhusiano. Aidha, ulijifunza faida na changamoto za uhusiano na tahadhari za kuchukua kabla na baada ya kuanzisha uhusiano. Katika sura hii, utafafanua njia za usafirishaji zilizopo kati ya Tanzania na nchi nyingine. Utajifunza pia jinsi njia hizo za usafirishaji zinavyodumisha uhusiano mwema baina ya Tanzania na nchi nyingine na zinavyochangia maendeleo ya uchumi nchini. Maarifa na ujuzi utakaoupata katika sura hii utakusaidia kuzitumia fursa zilizopo katika njia za usafiri na usafirishaji ili kuweza kuongeza pato lako binafsi, familia na taifa kwa ujumla.*



**Fikiri**

Maana ya usafirishaji.

Njia za usafirishaji.

Njia za usafirishaji zinavyochangia maendeleo ya eneo unaloishi.

## Dhana ya usafirishaji

Usafirishaji ni tendo la kupeleka watu au bidhaa kutoka eneo moja kwenda eneo jingine kwa kutumia chombo cha usafiri. Usafirishaji huo unaweza kufanyika kwa njia ya nchi kavu, anga na maji. Usafirishaji kwa njia ya nchi kavu, hutumia barabara, reli na mabomba yanayosafirisha maji, mafuta na gesi. Usafirishaji kwa njia ya maji hutumia meli, boti, mitumbwi, mashua na vivuko. Vilevile, usafirishaji kwa njia ya anga hutumia ndege na helikopta. Tanzania imekuwa ikijenga, kuboresha na kuimarisha njia za usafirishaji katika maeneo mbalimbali nchini.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya namba 1**

Bainisha njia za usafirishaji zilizopo katika mkoa unamoishi.

## Usafirishaji, maendeleo ya kiuchumi na uhusiano kati ya Tanzania na nchi nyingine

Usafirishaji ni sekta muhimu katika kuchochea maendeleo ya kiuchumi, kujenga na kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na nchi nyingine. Kwa kutumia njia kuu tatu za usafirishaji zilizoainishwa hapo juu, Tanzania imeweza kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia kwa namna mbalimbali.

### Usafiri na usafirishaji kwa njia ya nchi kavu

Usafiri na usafirishaji kwa njia hii, hutumia barabara, reli na mabomba. Vyombo vinavyotumia barabara ni magari ya mizigo, magari ya abiria na wanyamakazi kama vile punda na ngamia. Vilevile, chombo kinachotumia reli ni treni inayosafirisha mizigo na abiria. Kwa mfano, Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) husafirisha abiria na mizigo kati ya Tanzania, Zambia na mataifa ya jirani. Usafirishaji wa nchi kavu umekuza uhusiano baina ya Tanzania na nchi jirani kiuchumi na kijamii, hasa katika biashara na viwanda. Uhusiano wa kiuchumi katika sekta ya biashara umejikita katika kusafirisha mazao ya chakula na biashara. Vilevile, usafirishaji wa nchi kavu husababisha uwepo na uendelezaji wa viwanda, kutokana na usafiri na usafirishaji wa uhakika wa malighafi na bidhaa zinazozalishwa viwandani. Usafirishaji pia umesababisha kukua kwa miji katika vituo ambapo njia za usafirishaji zimepita. Biashara mbalimbali za chakula na huduma zitolewazo katika vituo kando ya njia za usafirishaji huwapatia wananchi kipato cha kuendeleza maisha, makazi na kuleta maendeleo katika maeneo yao. Usafirishaji pia umesababisha jamii ya Tanzania kufahamiana na kujenga urafiki na watu wa nchi nyingine wanaokuja nchini.

Usafirishaji wa nchi kavu unahusisha pia njia inayotumia mabomba yanayosafirisha maji, mafuta na gesi. Usafirishaji huu huchochea ukuaji wa uchumi kwa sababu ni rahisi na salama kwa jamii. Kielelezo namba

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 89 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

1 kinaonesha Reli ya TAZARA na bomba la mafuta kutoka Tanzania hadi Zambia: Tanzania Zambia Mafuta (TAZAMA). Mabomba yanayosafirisha mafuta na gesi yanaweza kupita chini ya maji na nchi kavu, kutegemea na asili ya mazingira. Hali hii inatoa fursa kwa wananchi kujiajiri, kuajiriwa na kukuza kipato chao na pato la taifa kwa ujumla. Vivyo hivyo, nishati ya gesi hutumika majumbani na kuendesha mitambo viwandani.




**Kielelezo namba 1:** *Reli ya TAZARA na bomba la mafuta la TAZAMA kutoka Tanzania hadi Zambia*

## Zoezi la 1

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja matumizi ya njia za usafirishaji wa nchi kavu nchini.
2. Bainisha faida za njia za usafirishaji nchini Tanzania.

### Usafirishaji kwa njia ya maji

Usafiri na usafirishaji kwa njia ya maji hufanyika katika bahari, maziwa na mito mikubwa. Kwa upande wa Tanzania, bahari imeunganisha nchi zote za



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 90 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ukanda wa pwani ya Bahari ya Hindi, kama vile, Kenya, Somalia, Visiwa vya Shelisheli, Msumbiji, Afrika Kusini, India na mabara ya Ulaya, Amerika na Australia. Ziwa Victoria linaunganisha nchi tatu ambazo ni Kenya, Uganda na Tanzania. Vilevile, Ziwa Tanganyika ni moja ya maziwa makubwa Afrika likienea mpakani mwa Tanzania, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi na Zambia. Ziwa Nyasa linaunganisha nchi za Tanzania, Malawi na Msumbiji.

Usafirishaji wa njia ya maji umechangia kwa kiasi kikubwa kukua kwa uhusiano kati ya Tanzania na nchi nyingine. Mchango wa sekta ya usafirishaji wa njia ya maji ni muhimu kwa maendeleo ya uchumi wa Tanzania. Biashara baina ya Tanzania na nchi zingine zimeendelea kupanuka kwa sababu ya uwepo wa usafiri wa uhakika wa majini kwa nchi za maziwa makuu na nchi zinazopakana na ukanda wa pwani wa Bahari ya Hindi. Kwa mfano, usafirishaji kwa njia ya maji kupitia Ziwa Victoria ni miongoni mwa njia kuu za usafirirshaji wa abiria na bidhaa mbalimbali kati ya Tanzania, Kenya na Uganda. Vilevile, usafirishaji kwa njia ya maji umekuza sekta ya kilimo na viwanda kwa kiasi kikubwa. Hii ni kwa sababu ya urahisi wa usafirishaji wa vifaa na pembejeo za kilimo kutoka mataifa ya Ulaya na Asia. Hali hii imetoa fursa za biashara, na ajira kwa wananchi hivyo kukuza pato la Mtanzania mmoja mmoja na taifa kwa ujumla. Usafirishaji wa malighafi za viwanda na bidhaa zitokanazo na viwanda unachangia kukua kwa uchumi wa Tanzania na nchi nyingine, sambamba na ukuaji wa masoko ya kitaifa na kimataifa kama vile, soko la samaki la kimataifa Kibirizi (Kigoma) na soko la samaki na dagaa Kirumba (Mwanza).

FOR ONLINE USE ONLY

**Usafirishaji kwa njia ya anga**

Usafiri na usafirishaji kwa njia ya anga hufanyika kwa kutumia ndege na helikopta. Baadhi ya viwanja vya ndege nchini kama vile Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere Dar es Salaam, Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro na Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume, Zanzibar. Viwanja vingine vipo Arusha, Mwanza, Mbeya, Tabora, Bukoba, Kigoma, Dodoma na Mtwara. Serikali imeendelea kuboresha usafiri wa anga kwa kupanua viwanja vya ndege na kuwa na ubora unaotakiwa kimataifa. Kwa mfano, Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere kimeboreshwa na kuongezwa kufikia jengo la tatu la kisasa la abiria kutoka majengo mawili ya awali. Hii imerahisisha usafiri na usafirishaji wa anga nchini. Vilevile, kuwepo kwa mashirika ya ndege



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 91 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

nchini yamesaidia kuunganisha nchi ya Tanzania na mataifa mengi duniani, mfano, ndege zinazotoka Ulaya, Falme za Kiarabu, India, Amerika, Ethiopia, Kenya, Uganda, Rwanda na Afrika Kusini. Vilevile, kupitia usafiri wa ndege watalii, wawekezaji, wafanyabiashara na viongozi mbalimbali huja kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii nchini. Kiwango cha watalii wanaokuja Tanzania kutoka mataifa ya Ulaya, Marekani na China kinazidi kukua na kuongezeka kila mwaka. Hii imesaidia kukua kwa kipato cha mtu mmojammoja na kuongezeka kwa pato la taifa kutokana na biashara zinazofanywa na watu katika maeneo yote yanayozunguka vivutio vya utalii, mfano, huduma za malazi na chakula, afya, michezo na burudani. Vilevile, wafanyabiashara hutumia njia hii kwa ajili ya usafirishaji wa bidhaa na malighafi, mfano, maua, vinyago na vitu vya asili kama mapambo na nguo za asili. Hivyo, kwa kiasi kikubwa usafiri na usafirishaji wa njia ya anga umekuza na kudumisha uhusiano wa kiuchumi baina ya Tanzania na nchi nyingine duniani.

**Zoezi la 2**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Ainisha njia za usafirishaji zilizopo Tanzania.
2. Shughuli zipi za maendeleo zinaweza kufanyika kwa kutumia njia za usafirishaji zilizopo katika eneo lako?

## Manufaa ya njia za usafirishaji

Kwa ujumla, njia za usafirishaji nchini zimekuwa ni chachu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Tanzania imekuwa ikipata mapato kutokana na kodi zinazolipwa kwa ajili ya matumizi ya njia za usafirishaji nchini. Tozo za barabarani, ushuru wa bandari na kodi za viwanja vya ndege zinazolipwa na watumiaji wa njia hizi za usafirishaji huongeza pato la taifa. Njia za usafirishaji zimesaidia taifa kupata zana mbalimbali za uzalishaji mali kutoka nje na bidhaa ambazo Tanzania haina uwezo wa kuzitengeneza. Kwa mfano, mashine na mitambo ya kuendeshea viwanda vikubwa na vidogo nchini.

Njia za usafirishaji zimewavutia wawekezaji wa ndani na wa nje kuwekeza katika sehemu mbalimbali za Tanzania kutokana na kuimarika kwa mazingira ya uwekezaji nchini. Pia, kupitia wataalamu mbalimbali hususani wawekezaji, Tanzania imeweza kupata na kutumia sayansi na teknolojia kutoka nje ya nchi ambayo inachangia maendeleo ya kiuchumi.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Usafirishaji wa mazao na malighafi pia kutoka eneo moja hadi jingine umesaidia katika kukuza pato la wananchi katika maeneo ambayo njia za usafirishaji hupita. Uuzaji wa bidhaa na mazao nchi za jirani pia umekuwa ukichangia maendeleo ya uchumi nchini. Wananchi wa nchi za mipakani hufanya biashara na nchi jirani na hivyo kusababisha kuongezeka kwa pato la wananchi na taifa kwa ujumla.

## Zoezi la 3

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Ni kwa namna gani njia za usafirishaji zinakuza maendeleo ya kiuchumi nchini Tanzania?
2. Kwa kutumia mifano, ainisha aina kuu tatu za njia za usafirishaji nchini.
3. Eleza kwa kifupi, ni kwa jinsi gani njia za usafirishaji zinadumisha uhusiano kati ya nchi ya Tanzania na nchi jirani.

**Andika KWELI kwa sentensi ya kweli na SI KWELI kwa sentensi isiyo ya kweli katika nafasi uliyopewa.**

4. Bomba la mafuta TAZAMA limesaidia kusafirisha madini ya shaba nchini Zambia. ________
5. Njia za usafirishaji nchini huleta maendeleo nchini na nchi jirani. ________
6. Reli ya TAZARA imeimarisha uhusiano wa Tanzania na Zambia katika nyanja za uchumi, siasa na kijamii. ________

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Sita

# Athari za njia zilizotumika kudai uhuru Afrika

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Sita, ulijifunza kuhusu harakati za ukombozi wa Bara la Afrika, sababu za kuanzishwa kwa harakati za kupinga utawala wa kikoloni na mbinu zilizotumika wakati wa kudai uhuru. Vilevile, ulijifunza kuhusu mashujaa wa Afrika katika harakati za ukombozi. Pia, ulijifunza kuhusu njia zilizotumika kudai uhuru katika nchi za Afrika. Vilevile, ulijifunza changamoto za kudai uhuru katika makoloni barani Afrika na mambo ya kujifunza kutoka kwa mashujaa wa Afrika. Katika sura hii, utachambua harakati zilizofanikisha njia za kudai uhuru. Vilevile, utachambua athari za njia na harakati zilizotumika kudai uhuru. Maarifa na ujuzi utakaoupata katika sura hii, utakuwezesha kutumia njia sahihi katika kutatua changamoto na kufanya uamuzi tofautitofauti katika jamii.*

**Kazi ya kufanya namba 1**

1. Kwa msaada wa mwalimu, tengeneza igizo fupi kuonesha maisha ya familia isiyo na uhuru. Igizeni darasani.
2. Uliza mzazi au mlezi wako maana ya nchi huru. Ainisha mambo yanayobainisha nchi kuwa huru.
3. Andika majibu ya mzazi au mlezi wako katika daftari lako na kisha wasilisha darasani..

## Harakati za kudai uhuru Afrika

Madhumuni ya kudai uhuru katika nchi za Afrika yalifanana kwa kiasi kikubwa. Waafrika walidai kupata uhuru wa kujitawala kupitia viongozi wao. Walitaka kuendeleza mifumo yao ya utawala, uzalishaji mali, mila na desturi. Hali hii ilitokana na utawala wa kikoloni ambao ulikuwa na misingi ya ubaguzi na unyonyaji wa nguvukazi na rasilimali zao kama vile ardhi na madini, upendeleo, ubaguzi wa rangi, ukabila na udini ikiwa ni sababu ya kuwatofautisha na kuwagawa Waafrika.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 94 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Harakati tofauti tofauti za kudai uhuru zilitumika kutegemea aina ya mtawala au watawala. Njia kuu tatu zilitumika katika kudai uhuru. Njia hizo zilikuwa ni pamoja na kudai uhuru kwa njia ya majadiliano. Njia hii ndiyo iliyotumika katika makoloni mengi ya Afrika. Wakati mwingine njia hii ya kudai uhuru iliitwa njia ya mabadiliko ya katiba. Njia ya pili ni ile ya kudai uhuru kwa mapambano ya vita na njia ya tatu ilikuwa ni kudai uhuru kwa njia ya mapinduzi.

**Njia ya kudai uhuru kwa majadiliano**

Njia hii ilitumika katika makoloni mengi zaidi Afrika. Kwa kawaida, uhuru ulipatikana kutokana na mashinikizo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa yaliyokuwapo wakati huo. Baadhi ya mbinu zilizotumiwa na viongozi wa mapambano ya kudai uhuru ni kuanzishwa kwa vyama vya siasa vya umma; viongozi wa vyama vya siasa kutoa elimu ya uraia; kufanya mikutano ya hadhara na matembezi ya mshikamano; na kuanzisha vijarida, vipeperushi na magazeti ya vyama vya siasa. Vilevile, migomo ya wafanyakazi na wakulima ilikuwa ni baadhi ya mbinu walizotumia wananchi.

Hivyo, uhuru ulitolewa kwa makubaliano baina ya viongozi wa vyama vikuu vya siasa na wawakilishi wa serikali za kikoloni kutoka Ulaya. Tanzania Bara, zamani Tanganyika ni miongoni mwa nchi za Kiafrika zilizopata uhuru wake kwa njia ya majadiliano tarehe 9/12/1961. Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, akiwa kiongozi mkuu wa chama cha TANU aliongoza majadiliano na mapambano ya kudai uhuru kutoka kwa watawala wa kikoloni wa Waingereza. Nchi nyingine ni Ghana, Uganda, Zambia, na Malawi.

**Athari za kudai uhuru kwa njia ya majadiliano**

Harakati za kudai uhuru kwa njia ya majadiliano zilikuwa na athari nyingi katika nchi za Afrika. Zifuatazo ni baadhi ya athari hizo:

(a) Uhuru ulipatikana bila kumwaga damu. Hili liliwezekana kutokana na mashinikizo ya wakati huo kwa wakoloni;

(b) Uanzishwaji wa vyama vingi katika makoloni. Vyama hivi vilidai uhuru wa nchi zao kwa lengo la kuziongoza baada ya serikali za kikoloni kuondolewa. Kwa mfano: Tanganyika viliundwa vyama kama TANU na ANC;

(c) Uanzishwaji wa matawi ya vyama vya siasa nchi nzima. Matawi haya yalikuwa vituo vya kueneza itikadi na ujumbe kutoka kwa uongozi wa

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

juu. Vilevile, matawi haya yalikuwa sehemu za vyama kupokea maoni na kero za wanachama;

(d) Serikali za kikoloni zilipiga marufuku watumishi wake kujiunga katika vyama vya siasa. Waliokiuka amri hiyo walifukuzwa kazi. Kwa hiyo, ilibidi kiongozi wa chama cha siasa achague kati ya ajira katika serikali ya kikoloni au kutumikia chama cha siasa. Mfano, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alijiuzulu kazi ya kufundisha Shule ya Sekondari ya Mt. Fransis, kwa sasa Shule ya Sekondari ya Pugu, ili kuendeleza harakati za kudai uhuru kama kiongozi wa chama cha TANU; na



***Kielelezo namba 1:*** *Mwalimu Julius K. Nyerere akihutubia mkutano wa hadhara wa wanachama wa TANU na wananchi kwa ujumla*

(e) Viongozi makini wa vyama vya siasa waliandamwa, kunyanyaswa, kutishwa na kufungwa jela ili kuwanyamazisha. Kazi ya viongozi hao ilikuwa ni kufichua ubaya wa ukoloni na faida za kupata uhuru kwa nchi



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

zao. Mfano Mwalimu Nyerere wa Tanganyika alishitakiwa kwa kosa la kuwakosoa wakuu wa wilaya wawili.

**Zoezi la 1**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja athari nne za kudai uhuru kwa njia ya majadiliano.
2. Eleza kwa ufupi malengo mawili ya vyama mbalimbali vya siasa vilivyoanzishwa kipindi cha ukoloni.
3. Ainisha madhumuni mawili ya vyama vya siasa kuanzisha matawi wakati wa harakati za kudai uhuru.
4. Eleza kwa ufupi sababu mbili za wakoloni kuwaandama viongozi wa vyama vya siasa vyenye nguvu.



**Kazi ya kufanya namba 2**

Katika vikundi vya wanafunzi eleza kwa ufupi mafunzo mawili unayoyapata kuhusu changamoto zilizowakabili viongozi wa harakati za kupigania uhuru.

Wasilisha majibu yenu kwa majadiliano darasani.

**Kudai uhuru kwa njia ya vita**

Njia hii ilitumika katika makoloni yaliyokuwa na walowezi wengi wa Kizungu. Walowezi hao walijimilikisha ardhi kubwa na yenye rutuba na migodi ya madini. Walowezi hao pia, waliwekeza katika viwanda na mashamba makubwa ya mazao na mifugo katika makoloni hayo. Wengine walijipatia uraia wa makoloni hayo na hawakuwa tayari kuachia mali walizojimilikisha. Kwa ujumla walowezi hao walikuwa na nguvu za uchumi na siasa. Mfano ni walowezi katika makoloni ya Algeria, Angola, Kenya, Rhodesia ya Kusini (Zimbabwe), Namibia, Afrika Kusini, Msumbiji na Guinea Bissau. Harakati za kudai uhuru katika makoloni hayo, zilizosababisha  wapigania uhuru kutumia silaha za kivita aina mbalimbali kupigana . Pia, Waafrika waliomba kuungwa

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 97 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mkono na nchi zisizofungamana na upande wowote. Mfano mzuri wa nchi hizo ni China na Cuba. Hata hivyo, vyama vya siasa vilitoa mafunzo ya kivita kwa vijana ili wapambane na majeshi na kuharibu mali, makazi ya walowezi, miundombinu na vitega uchumi vya wakoloni hadi uhuru ulipopatikana.

**Athari za kudai uhuru kwa njia ya vita**

Zifuatazo ni athari za mbinu zilizotumiwa kupigania uhuru kwa vita:

(a) Uhuru ulipatikana kwa kumwaga damu na uharibifu wa mali nyingi. Walowezi, wananchi, wapiganaji na viongozi waliuawa katika mapambano hayo;

(b) Viongozi na wapigania uhuru walilazimika kuishi uhamishoni katika mataifa rafiki;

(c) Vita hivi vya ukombozi vilichukua miaka mingi, kwa mfano Msumbiji na Angola miaka 10, Namibia miaka 24 na Afrika Kusini miaka 33 hivyo kuathiri Waafrika;

(d) Mafunzo ya kijeshi na uratibu wa harakati za mapigano vilifanyiwa uhamishoni kwa sababu ya kuwekewa vikwazo na wakoloni na hivyo kukosa uhuru wa kujifunza. Kwa mfano, wapiganaji wa chama cha FRELIMO cha Msumbiji na wapiganaji wa chama cha ANC cha Afrika Kusini walipata mafunzo na hifadhi nchini Tanzania;

(e) Uwepo wa wakimbizi kwenye baadhi ya nchi za Afrika, ikiwa ni matokeo ya vita nchini mwao. Kwa mfano, mikoa ya Ruvuma, Mtwara na Lindi ilihifadhi wakimbizi wengi kutoka Msumbiji;

(f) Viongozi kadhaa wa vyama na harakati za mapigano walifungwa jela ili kufifisha vyama vyao na kuzima harakati za kudai uhuru. Hata hivyo nguvu ya umma ilishinda na uhuru ukapatikana; na

(g) Viongozi wengi wa harakati za ukombozi wakati wa utawala wa wakoloni waliuawa kikatili. Mfano ni Eduardo Mondlane wa koloni la Wareno la Msumbiji. Mauaji haya yalilenga kuwatisha viongozi wengine na wafuasi wao kuacha kudai uhuru kutoka kwa wakoloni.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 98 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 2**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza sababu za baadhi ya makoloni kudai uhuru kwa njia ya vita.
2. Orodhesha nchi zilizopata uhuru kwa njia ya vita.
3. Taja matokeo yaliyopatikana katika nchi zilizohifadhi wapigania uhuru wa vyama mbalimbali barani Afrika.
4. Kwa ufupi bainisha athari za kudai uhuru kwa njia ya vita.

**Kudai uhuru kwa njia ya mapinduzi**

Njia hii ilitumika pale wakoloni walipokabidhi madaraka kwa vibaraka wao wachache badala ya kuyakabidhi kwa wananchi walio wengi. Wakoloni walitaka kuhakikisha kwamba maslahi yao yanalindwa hata baada ya kutoa uhuru. Aidha, walitaka walowezi ama mamwinyi waendelee kuwa tabaka tawala na Waafrika waendelee kuwa tabaka la watwana nchini mwao baada ya kupata uhuru. Mfano wa nchi zilizopata uhuru kwa njia ya mapinduzi Afrika ni Zanzibar na Misri.

Wazalendo walilazimika kuzing'oa serikali za vibaraka zilizoundwa. Mbinu walizotumia zilishabihiana na zile za kupata uhuru kwa njia ya vita. Mbinu zifuatazo zilitumika; viongozi wa harakati za kudai uhuru walianzisha na kutoa mafunzo kwa vikosi maalumu vya askari wa kufanya mapinduzi, viongozi wa mapinduzi waliunda serikali yao iliyoshirikisha makundi anuwai ya wananchi na kuanzisha uhusiano wa kibalozi na nchi rafiki kusudi ziunge mkono wanamapinduzi na kuwapatia misaada ya hali na mali. Kielelezo namba 2 ni picha ya Rais wa kwanza wa Zanzibar Sheikh Abeid Amani Karume kama mmoja wa viongozi wa mapinduzi. Mapinduzi ya Zanzibar yalitokea tarehe 12 Januari 1964.



**Kielelezo namba 2:** *Rais wa kwanza wa Zanzibar Sheikh Abeid Amani Karume aliyeongoza mapinduzi ya Zanzibar*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Athari za mbinu ya mapinduzi**

Zifuatazo ni athari za mbinu za kupata uhuru kwa njia ya mapinduzi:

(a) Vibaraka na walowezi walisalimu amri ya nguvu ya umma na kung'olewa madarakani;

(b) Uhuru wa kweli wa wananchi walio wengi ulipatikana. Mara nyingi ulikuwa uhuru madhubuti kwa sababu kila mwananchi aliguswa na gharama za kuudai uhuru;

(c) Wananchi waliunda serikali yao katika kila moja ya nchi hizo;

(d) Watu walipoteza maisha na mali nyingi kuharibiwa katika mapambano; na

(e) Nchi zilizopata uhuru kwa njia hii ziliendeleza mapinduzi ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

**Zoezi la 3**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza kwa ufupi sababu za baadhi ya makoloni kupata uhuru kwa njia ya mapinduzi.
2. Ipi ilikuwa athari hasi kufuatia kupata uhuru kwa njia ya mapinduzi?
3. Eleza kwa ufupi sababu ya jibu lako katika swali namba 2.

FOR ONLINE USE ONLY

**Zoezi la 4**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Andika **KWELI** kwa sentensi ya kweli na **SI KWELI** kwa sentensi isiyo ya kweli katika nafasi uliyopewa.

   (a) Wafanyakazi Waafrika waliofanya kazi serikali ya kikoloni walipunguziwa mishahara baada ya kujihusisha na harakati za kudai uhuru. __________

   (b) Waafrika walipata huduma za jamii sawa na Wazungu kabla ya uhuru.__________

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(c) Maandamano ya amani hayakusaidia katika juhudi za kudai uhuru.__________

(d) Wafanyabiashara Waafrika waliagiza bidhaa chache sana kutoka nje wakati wa ukoloni.__________

2. Jaza nafasi zilizo achwa wazi

(a) Wapiganaji wa chama cha FRELIMO walipata mafunzo ya kijeshi katika nchi ya __________ na kufanikiwa kuleta uhuru wa kweli Msumbiji.

(b) Katika harakati za kudai uhuru, baadhi ya nchi za Afrika zilizopata uhuru wake kwa njia ya mapinduzi ni __________ na __________

(c) Mwalimu Julius K. Nyerere alifanikiwa kuongoza harakati za kudai uhuru wa Tanganyika akiwa kiongozi wa chama cha __________

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Saba

# Maendeleo nchini Tanzania baada ya uhuru

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Sita, ulijifunza kuhusu uvamizi wa sasa barani Afrika baada ya uhuru, dhana ya ukombozi na mbinu za uvamizi wa sasa. Vilevile, ulijifunza athari za uvamizi wa sasa na harakati za ukombozi katika kupambana na uvamizi huo. Katika sura hii utachanganua maendeleo ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni yaliyopatikana Tanzania tangu kupata uhuru. Vilevile, utajifunza changamoto za maendeleo nchini Tanzania na namna ya kukabiliana nazo. Maarifa na ujuzi utakaoupata katika sura hii utakusaidia kuthamini juhudi za Watanzania katika kuleta maendeleo baada ya uhuru na kushiriki katika kulinda na kuendeleza maendeleo hayo.*



**Fikiri**

Dhana ya maendeleo.

Namna ya kubaini maendeleo ya jamii na taifa.

## Dhana ya maendeleo

Maendeleo ni hali ya kutoka katika hatua duni kwenda hatua bora. Maendeleo hayo yanapaswa kuzingatia haki za binadamu, mila na desturi zinazofaa, utamaduni na kulinda umoja wa kitaifa. Maendeleo hayo pia yanapaswa kuwa endelevu na yanayokidhi mahitaji ya jamii inayohusika. Maendeleo endelevu ni yale yasiyoleta athari kwa kizazi kijacho. Maendeleo hayo yanaweza kutokea katika nyanja mbalimbali za maisha kama vile uchumi, siasa, jamii na utamaduni. Maendeleo katika uchumi yanalenga mabadiliko ya sayansi na teknolojia ili kurahisisha utendaji kazi, mfano uzalishaji mali mashambani, viwandani na migodini. Maendeleo ya kiuchumi husababisha maendeleo ya sekta nyingine, kama vile, miundombinu na huduma za jamii mfano, afya, elimu, maji na umeme. Maendeleo ya huduma za jamii husababisha utulivu wa kisiasa nchini, hivyo huwezesha viongozi na wananchi kuleta maendeleo ya jamii na taifa kwa ujumla.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 102 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya namba 1**

Tembelea shule mbili na kisha:

1. Bainisha maendeleo ya mambo yafuatayo:
   (a) Idadi ya vyumba vya madarasa
   (b) Idadi ya walimu na wanafunzi
   (c) Idadi ya matundu ya choo

Pamoja na nchi kukabiliwa na changamoto nyingi za kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kijamii zilizotokana na mfumo wa kikoloni, Tanzania imeweza kujiletea maendeleo kwa vipindi tofautitofauti kuanzia 1961 hadi sasa. Maendeleo katika nyanja za kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kijamii yamegawanyika katika awamu kuu tatu:

(a) Awamu ya mwanzo ni miaka ya 1961 hadi 1966;

(b) Awamu ya kati ni miaka ya 1967 hadi 1985; na

(c) Awamu ya sasa ni miaka ya 1986 hadi sasa.

## Harakati za maendeleo katika awamu ya mwanzo, 1961 -1966

Kipindi hiki kilikuwa ni kipindi cha mpito cha kuondoa mifumo ya kikoloni baada ya uhuru na kuimarisha sera za nchi. Mara baada ya uhuru nchi haikuwa na uchumi imara. Hii ilitokana na kutokuwapo kwa miundombinu thabiti, viwanda, na wataalamu wa kutosha mfano, wachumi, walimu, wahandisi, madaktari, wauguzi na wataalamu wa kilimo na mifugo. Wataalamu hawa wangeweza kushiriki kuiletea nchi maendeleo kutokana na sekta ambazo wangezisimamia. Hali hii iliifanya Tanzania na nchi nyingi za Kiafrika kuendelea kuwa tegemezi katika nyanja mbalimbali za maendeleo. Ili kuondoa utegemezi huo na kujiletea uhuru katika nyanja mbalimbali za maendeleo baada ya uhuru, Tanzania ilibuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ya maendeleo kiuchumi, kijamii, kisiasa, na kiutamaduni kama ifuatavyo:

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### (a) Maendeleo ya kiuchumi

Hiki kilikuwa ni kipindi cha mwanzo cha ujenzi wa uchumi baada ya Tanzania kupata uhuru. Ingawa uhuru ulishapatikana, njia kuu za uzalishaji mali kama viwanda, mashamba, njia za usafiri na usafirishaji, mashamba makubwa ya mazao na mifugo vilimilikiwa na watu wachache hasa mabepari wa Kizungu. Pamoja na njia za uzalishaji mali kumilikiwa na wachache, serikali huru ya Tanzania ilianza kuimarisha uchumi wake kwa kuboresha njia za usafiri na mawasiliano kama vile barabara, reli na posta. Hii ilifanyika ili kurahisisha usafirishaji wa mazao, pembejeo na watu. Kwa mfano, mwaka 1963 kipande cha reli kutoka stesheni ya Mruazi-Korogwe hadi makutano ya Ruvu kilijengwa. Reli hii ilijengwa ili kuunganisha reli ya Tanga na ya Kati. Barabara zilijengwa pia katika baadhi ya maeneo ya miji na wilaya ili kuimarisha usafirishaji nchini. Vilevile, ulifanyika upanuzi wa masoko ya ndani na nje ili kufanikisha biashara za mazao na malighafi zinazozalishwa nchini na kuondoa mfumo wa uzalishaji uliotegemea kuzalisha malighafi na kuuza nje. Kulianzishwa pia, mipango ya maendeleo ya miaka mitatu 1961-1964 na miaka mitano 1964-1969.

### (b) Maendeleo ya kijamii

Huduma nyingi za kijamii kama vile, huduma za afya, elimu, maji na umeme zilipatikana kwa wachache. Huduma hizi, kwa sehemu kubwa zilikuwa ni zile zilizoachwa na wakoloni. Pia, zilikuwapo huduma za afya na elimu zilizotolewa na madhehebu ya dini. Huduma za jamii kama vile, shule, vyuo, hospitali na zahanati zilikuwa chache ikilinganishwa na idadi ya watu. Maendeleo katika jamii yalilenga zaidi katika kuboresha huduma za afya na elimu; Kwa mfano, serikali iliweza kuanzisha na kujenga shule na vyuo, kama vile Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambacho kilianza kama Chuo Kikuu Kishiriki cha London Oktoba mwaka 1961 pamoja na Chuo cha Ualimu Chang'ombe kilichoanzishwa mwaka 1964 ili kuboresha utoaji wa elimu nchini. Vilevile, kuongeza usajili wa wanafunzi shuleni katika ngazi ya elimu ya msingi na sekondari ili kuweza kupata wataalamu wa kuleta maendeleo nchini na kutoa elimu ya afya kwa jamii ya kujikinga na magonjwa mbalimbali. Katika kipindi hiki ubaguzi wa rangi katika elimu na huduma za afya ulitokomezwa.

### (c) Maendeleo ya kisiasa

Maendeleo ya kisiasa kati ya mwaka 1961 na 1966 yalihusu hatua mbalimbali katika kujenga taifa jipya la Tanzania baada ya uhuru. Tanganyika ilipata uhuru wake kutoka kwa utawala wa Waingereza tarehe 9 Desemba 1961.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 104 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Siku hiyo bendera ya Waingereza ilishushwa na bendera ya Tanganyika ilipandishwa. Mara baada ya kupata uhuru, hatua ya kwanza ilikuwa ni ile ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kujiuzulu wadhifa wake kama Waziri Mkuu wa Tanganyika mwezi Januari 1962. Lengo la kujiuzulu lilikuwa ni kumwezesha Mwalimu Nyerere kupata muda wa miezi kumi ili kuimarisha chama cha TANU na kuandaa misingi ya kulijenga taifa jipya la Tanganyika. Hatua ya pili ni kukabidhiwa madaraka kwa Waafrika ambapo, madaraka mbalimbali serikalini yalikabidhiwa mikononi mwa Waafrika kutoka kwa Wazungu. Hatua ya tatu ilikuwa uchaguzi mkuu wa Rais mwezi Novemba 1962, ambapo Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alichaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Tanganyika kuanzia tarehe 9 Desemba 1962. Hatua ya nne ilikuwa ni kuanzishwa kwa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) mwaka1963 na kuundwa kwa jeshi jipya lililojulikana kama Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) mwanzoni mwa mwaka 1964. Jeshi jipya la wananchi liliundwa baada ya kuvunjwa kwa jeshi la ulinzi la kikoloni. Hatua ya tano ilikuwa ni Mapinduzi ya Zanzibar tarehe 12 Januari, 1964. Hatua ya sita ilikuwa ni muungano wa Tanganyika na Zanzibar tarehe 26, Aprili 1964. Hatua ya saba ilikuwa ni mchakato wa kuachana na mfumo wa vyama vingi na kuanzisha mfumo wa chama kimoja cha siasa kati ya mwaka 1964 hadi Julai 1965. Hatua ya nane ilikuwa ni uchaguzi wa kwanza wa mfumo wa chama kimoja cha siasa uliofanyika Septemba 1965.

### (d) Maendeleo ya kiutamaduni

Katika kipindi hiki serikali ilijitahidi sana kusimamia utamaduni wa Mtanzania katika mfumo mzima wa maisha, mfano mavazi, chakula, burudani na hata kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya taifa kwa lengo la kuunganisha jamii zote nchini kwa lugha moja.

### Zoezi la 1

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza jinsi uboreshaji wa miundombinu kama vile barabara na reli unavyoweza kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini.
2. Bainisha maendeleo ya kijamii kati ya mwaka1961-1966.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Changamoto zilizozikabili harakati za maendeleo awamu ya mwanzo 1961-1966**

Pamoja na mafanikio ya maendeleo yaliyopatikana mara baada ya kupata uhuru zilikuwepo changamoto mbalimbali zilizozikabili harakati za maendeleo ya taifa jipya la Tanzania. Maendeleo yalikabiliwa na uhaba wa viwanda vya kutumia malighafi zilizozalishwa ndani ya nchi. Uhaba wa masoko ya ndani na nje ya kuuza bidhaa zilizozalishwa ndani pia ni changamoto nyingine. Hali hii ilisababisha bidhaa kuuzwa kwa bei ndogo ndani na nje ya nchi. Vilevile, serikali ilikosa mapato kutokana na njia kuu za uchumi nchini kama vile viwanda, mashamba makubwa na mabenki kumilikiwa na watu wachache wakiwamo wageni. Elimu iliyotolewa haikukidhi mahitaji ya Watanzania kwa wakati huo. Mfano, badala ya kuhimiza elimu ya kujitegemea, sera ya elimu iliyorithiwa kutoka kwa serikali ya wakoloni ilijikita katika kuandaa wasomi wachache watakao tegemea kuajiriwa na kufanya kazi za ofisini. Pia sekta ya elimu iliyorithiwa kutoka kwa wakoloni, ilikuwa na uhaba wa walimu na miundombinu duni ambayo ilisababisha idadi kubwa ya watoto waliokuwa na umri wa kwenda shule kushindwa kuandikishwa shule. Vivyo hivyo, kulikuwapo uhaba wa huduma za maji na afya, kama vile dawa, watoa huduma na vitendea kazi katika zahanati na hospitali. Aidha, athari za mgawanyo wa huduma za jamii ulipendelea zaidi maeneo yaliyokaliwa na Wazungu wakati wa ukoloni. Vilevile, maeneo ya uzalishaji mali yaliendelea kuwa bora zaidi huku maeneo mengi yaliyoachwa bila maendeleo wakati wa ukoloni yaliendelea kuwa na huduma duni za kijamii.



**Kazi ya kufanya namba 2**

Jadili na wanafunzi wenzako changamoto zilizozikabili harakati za awali za kuleta maendeleo nchini.

## Harakati za maendeleo katika awamu ya kati, 1967 - 1985

Hiki ni kipindi kilichokuwa na mabadiliko chanya na makubwa katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Hii ilitokana na changamoto zilizozikabili harakati za awali za kuleta maendeleo Tanzania.

### (a) Maendeleo ya kisiasa

Kwa upande wa siasa, Tanzania iliamua kufuata siasa ya Ujamaa na Kujitegemea. Siasa hii ilipitishwa katika Azimio la Arusha tarehe 05/02/1967.



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 106 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Lengo lilikuwa kuhakikisha kuwa njia kuu za uchumi zinamilikiwa na wananchi wote kwa ajili ya maendeleo ya wote. Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea ilitekelezwa kwa ufasaha chini ya siasa ya mfumo wa chama kimoja kilichoitwa TANU. Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea pamoja na mfumo wa chama kimoja vilichangia sana kuleta umoja wa kitaifa, mshikamano na hali ya amani. Aidha, hatua nyingine muhimu ya kisiasa katika kipindi hiki ilikuwa ni kuimarisha uhusiano wa kikanda (Afrika Mashariki). Hivyo, Tanzania kwa kushirikiana na nchi za Kenya na Uganda zilianzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki. Jumuiya hiyo iliundwa mwaka 1967 na kuvunjika mwaka 1977. Sababu mojawapo ya kuvunjika ilikuwa ni nchi za Tanzania na Kenya hazikukubaliana na utawala wa kidikteta wa Idd Amini aliyekuwa Rais wa Uganda kuanzia mwaka 1971 hadi 1979.

Aidha, kabla ya kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ilijipatia mafanikio kadhaa ikiwemo kuimarisha udugu na utengamano wa nchi wanachama, kuanzisha mashirika ya pamoja ili kuboresha miundombinu baina ya nchi wanachama kama vile mashirika ya pamoja ya Afrika Mashariki ya ndege, reli, bandari na posta ili kuchochea ukuaji wa uchumi wa wananchi na pato la taifa la nchi wanachama na kuimarisha ulinzi na usalama.

Kipindi hiki pia kilishuhudia hatua nyingine mbili za kisiasa nchini Tanzania. Hatua ya kwanza ilikuwa ni kuunganisha vyama vya TANU kutoka Tanzania Bara na ASP kutoka Zanzibar mwaka 1977 na kuzaliwa Chama Cha Mapinduzi (CCM). Hatua hii pia iliendana na chama kushika hatamu. Hatua ya pili ilikuwa ni Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kustaafu rasmi kwa hiari yake wadhifa wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Novemba 1985. Hatua hii ya kung'atuka iliweka msingi imara wa demokrasia ya kupokezana madaraka ya uongozi wa nchi kwa amani kwa taifa la Tanzania.

### (b) Maendeleo ya kiuchumi

Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea iliyotokana na Azimio la Arusha ilitoa mwelekeo wa shughuli za maendeleo katika nyanja ya kiuchumi. Serikali ilimiliki njia kuu za kiuchumi kwa niaba ya wakulima na wafanyakazi na kuhimiza utekelezaji wa sera na mikakati ya maendeleo ili kuondoa uchumi tegemezi. Hivyo, harakati za maendeleo zilifanywa na serikali kwa kushirikiana na wananchi wake. Maendeleo yalilenga kuboresha mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi kutoka nje ya nchi. Katika kukabili changamoto mbalimbali za maendeleo, serikali iliendeleza wakulima, kuhimiza kilimo na ufugaji wa kisasa na kuhimiza vyama vya ushirika. Vilevile, serikali ilianzisha na kuendeleza viwanda mbalimbali nchini. Mfano ni baadhi ya viwanda vya

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

nguo kama MWATEX (Mwanza), MUTEX (Musoma), KILITEX (Arusha) na Urafiki (Dar es Salaam). Vingine ni viwanda vya bidhaa za ngozi, viberiti, vipuri vya magari na kiwanda cha mashine cha Mang'ula. Pia, kiwanda cha matairi Arusha (General tyre 1971), viwanda vya vifaa vya ujenzi, Kiwanda cha Sigara (TCC) na kiwanda cha kuunganisha magari ya scania (TAMCO-Kibaha). Kuongezeka kwa uzalishaji mali kulisababisha kuanzishwa kwa mashirika ya umma na mabenki, mfano Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), Benki ya Maendeleo Vijijini (CRDB) na Benki ya Posta (PB). Vilevile, kuendelezwa kwa viwanda vya kuongeza thamani ya mazao. Njia za usafiri na usafirishaji zilijengwa na kuboreshwa. Maduka makubwa ya jumla kwa kila mkoa na maduka ya ushirika ya vijiji yalianzishwa. Kila shughuli ilifanywa na serikali, kama vile, uzalishaji wa chakula na nyama, usafirishaji, usambazaji na uuzaji wa bidhaa muhimu kama vile sukari, mazao ya nafaka na mafuta ya kupikia. Shughuli zote zilifanywa na mashirika ya umma mfano, *National Agriculture and Food Corporation* (NAFCO), *National Milling Corporation* (NMC), kampuni ya usafiri kwa kila mkoa, vyama vya ushirika na maduka ya ushirika.

Shughuli hizi za kiuchumi ziliongozwa na sera za utaifishaji na maendeleo vijijini. Utaifishaji ulihusu kutaifisha njia kuu za uchumi. Maendeleo vijijini yalihusu kuanzisha vijiji vya ujamaa na vijiji vya maendeleo.

**Kazi ya kufanya namba 3**

1. Kwa msaada wa mwalimu wa somo, andaa ngojera au wimbo kuhusu maendeleo ya uchumi katika kipindi cha awamu ya kati mwaka 1967 hadi 1985 na mafanikio yake.
2. Ainisha mafanikio manne ambayo nchi ya Tanzania ilipata kutokana na uhusiano na nchi nyingine za Afrika Mashariki.

### (c) Maendeleo ya kijamii

Katika nyanja ya kijamii, yalikuwapo maendeleo mbalimbali ikiwa ni matokeo ya Azimio la Arusha la mwaka 1967. Azimio hili lilisababisha kutaifishwa kwa mali na taasisi za elimu na afya mfano shule, vyuo na hospitali zilizokuwa zikimilikiwa na taasisi au mashirika ya dini kwa lengo la kuimarisha mfumo



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 108 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

wa elimu na afya nchini. Hali hii ilisababisha watu wengi nchini kupata elimu, kuanzia elimu ya msingi hadi ya chuo kikuu kwa sababu serikali iligharamia utoaji wa elimu. Elimu ya msingi ilikuwa ni lazima kwa kila mtoto aliyefikia umri wa kwenda shule. Sera ya elimu kupitia Azimio la Arusha, ilikuwa ni Sera ya Elimu ya Kujitegemea. Sera hii ililenga kuandaa vijana wapate elimu ya kuwawezesha kujitegemea katika maisha.

Mwaka 1974 serikali iliridhia utoaji wa elimu bure kupitia Azimio la Musoma. Azimio la Musoma lilileta sera ya elimu kwa watu wote (UPE), kwa mtoto aliyefikia umri wa kwenda shule alitakiwa aende shule. Vilevile, serikali ilitoa elimu kwa watu wazima wasiojua kusoma na kuandika kote nchini. Hali hii ilichochea sana kukua kwa uchumi wa mtu mmojammoja na taifa kwa ujumla kwa sababu watu waliweza kusoma na kutambua maelekezo ya kilimo na ufugaji bora na maelekezo ya kanuni za afya. Hatua nyingine ya maendeleo ya kijamii ilikuwa ni uanzishwaji wa vijiji vya ujamaa 1968-1973, kisha vijiji vya maendeleo 1973-1976 kupitia Azimio la Arusha. Hali hii iliirahisishia serikali kutoa huduma za jamii kwa watu wengi zikiwapo huduma za afya, maji na elimu. Katika kipindi hiki, kila kijiji kilitakiwa kuwa na zahanati na shule ya msingi. Kila vijiji vitatu vilitakiwa kuwa na kituo cha afya. Vilevile, palikuwapo na ongezeko la ajira kwa wananchi kutokana na shughuli za viwanda na kilimo na hivyo kuboreka kwa hali za maisha ya watu.

### (d) Maendeleo ya kiutamaduni

Mabadiliko ya maendeleo yalifika mbali sana katika jamii za Watanzania, ikiwa ni pamoja na kudumisha utamaduni na upendo kwa ustawi wa jamii nzima. Kiswahili kiliendelea kuwa lugha ya taifa na kuunganisha jamii za Watanzania zenye makabila zaidi ya 120. Kiswahili pia kilipitishwa kuwa lugha ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi. Umuhimu wa lugha ya Kiswahili ulisababisha kuundwa kwa Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) kwa shabaha ya kukuza, kuimarisha na kuendeleza lugha ya Kiswahili. Kipindi hiki pia kilishuhudia kuundwa kwa Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA) kwa lengo la kukuza na kuendeleza sanaa ya Tanzania. Vilevile, mavazi yenye heshima na maadili katika jamii yaliendelea kuvaliwa, mfano khanga na vitenge. Vyakula vilivyoliwa vilikuwa ni vile vya asili. Shughuli za michezo kama vile riadha, mpira wa miguu na wavu ziliendelezwa sana katika kipindi hiki.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 2**

**Jibu swali lifuatalo:**

Eleza kwa kifupi maendeleo ya siasa yaliyopatikana katika kipindi cha awamu kati ya mwaka 1967-1985.

## Changamoto za harakati za maendeleo katika awamu ya kati, 1967 hadi 1985

Pamoja na maendeleo yaliyopatikana katika awamu hii, Tanzania ilikumbana na changamoto mbalimbali katika harakati za kuleta maendeleo katika kipindi cha mwaka 1967 hadi 1985. Tanzania ilikumbwa na matatizo mengi ya kiuchumi, ikiwa ni pamoja na janga la dunia la kiuchumi la kupanda kwa bei ya mafuta Mashariki ya Kati mwaka 1973 na 1979. Tanzania pia, ilikumbwa na janga la ukame lililotokea miaka ya 1974 na 1975. Ukame huo ulisababisha uhaba mkubwa wa chakula na hivyo serikali kutumia fedha nyingi katika kutatua tatizo la njaa. Vilevile, kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) mwaka 1977 kulisababisha Tanzania kuunda mashirika yake binafsi ili kujikomboa kiuchumi. Vita vya Kagera kati ya Tanzania na Uganda mwaka 1978 hadi 1979 viliathiri uchumi wa nchi kwa kiasi kikubwa. Vita hivi vilisababisha Tanzania kutumia fedha nyingi kukabiliana na adui Nduli Idd Amini aliyekuwa Rais wa Uganda wakati huo. Ubinafsi na matumizi mabaya ya madaraka kwa baadhi ya viongozi katika jamii, ulisababisha ubadhirifu wa mali za umma na hivyo kudorora kwa uchumi. Zaidi ya hayo kati ya miaka 1979 hadi 1985 Shirika la Fedha la Dunia (IMF) na Benki ya Dunia (WB) vilisitisha kutoa misaada ya kifedha kwa Tanzania. Benki ya Dunia pia ilizizuia nchi nyingine zisitoe misaada kwa Tanzania kwa kuwa Tanzania ilikataa kukubaliana na masharti yake.

Kwa ujumla, changamoto hizi zilisababisha kuporomoka kwa uchumi na hivyo faifa kukosa mitaji ya kuendeleza na kuimarisha shughuli za kiuchumi na kijamii. Majanga na matatizo hayo yote yalisababisha taifa kuingia katika sera za soko huria na ubinafsishaji za IMF na WB kuanzia mwaka 1986.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 110 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya namba 4**

Uliza mzazi au mlezi kuhusu mambo yaliyojitokeza kisiasa na kijamii nchini Tanzania kuanzia mwaka 1986 hadi 1992.

## Harakati za maendeleo awamu ya sasa, kuanzia mwaka 1986

Maendeleo nchini Tanzania tangu mwaka 1986 hadi sasa yalilenga katika kujikwamua na matatizo yaliyotokea kuanzia katikati ya miaka ya 1970 hadi katikati ya miaka ya 1980. Maendeleo pia, yalilenga katika kufufua na kuendeleza uchumi, kuleta ustawi wa jamii na uboreshaji wa mapato ya ndani ili kuimarisha uchumi wa nchi. Hii ilifanyika ili kupunguza utegemezi wa mapato ya kuendeshea nchi kutoka nchi za kigeni. Sera mbalimbali za maendeleo zilianzishwa ili kukuza uchumi na kufanikisha maendeleo nchini.

### (a) Maendeleo ya kisiasa

Baadhi ya wananchi wa Tanzania walidai mabadiliko kutoka mfumo wa chama kimoja na kwenda kwenye mfumo wa vyama vingi. Vuguvugu la kuleta mabadiliko ya kisiasa kutoka mfumo wa chama kimoja kwenda mfumo wa vyama vingi lilianza mwaka 1985. Baadaye kuanzia mwaka 1990, Baba wa Taifa aliruhusu mjadala wa kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi ufanyike kwa uwazi. Mwaka 1991, Rais wa awamu ya pili Mheshimiwa Ali Hassani Mwinyi aliunda Tume ya mfumo wa chama kimoja na vyama vingi vya siasa. Mwenyekiti wake alikuwa Jaji Mkuu Francis Nyalali ili kupata maoni ya wananchi ya kutaka mabadiliko kutoka chama kimoja kwenda vyama vingi. Mwaka 1992 tume ilipendekeza Tanzania iingie kwenye mfumo wa vyama vingi, hatua ambayo ilifikiwa rasmi Julai 1992. Aidha, uamuzi wa Tanzania kuingia kwenye mfumo wa vyama vingi ulikuwa pia ni shinikizo kutoka Benki ya Dunia na mataifa ya Magharibi.

Mabadiliko ya siasa nchini yalifanyika kwa kuanzisha mfumo wa vyama vingi mwaka 1992. Mwaka 1992 vyama vya siasa 13 vilisajiliwa na serikali. Vyama kama NCCR-Mageuzi, TLP, CUF, CHADEMA na CCM kilichosajiliwa

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kabla ya mfumo huu pamoja na vingine vingi vilisajiliwa. Uchaguzi mkuu wa kwanza wa vyama vingi ulifanyika mwaka 1995, na kusababisha ushindani wa kisiasa, kuongezeka kwa demokrasia, kuimarika kwa uhuru wa vyombo vya habari ikilinganishwa na hapo awali. Uwajibikaji, uwazi na utendaji katika serikali uliongezeka ili kuwaletea maendeleo wananchi. Licha ya uchaguzi wa 1995, chaguzi za ushindani wa vyama vingi zimeendelea kila baada ya miaka mitano hadi sasa.

### (b) Maendeleo ya kiuchumi

Tanzania ni miongoni mwa nchi wanachama wa taasisi mbalimbali za kimataifa, kama vile Benki ya Dunia (WB), Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Shirika la Biashara la Kimataifa (WTO), Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) na Jumuiya za kimataifa ikiwemo Umoja wa Mataifa (UN). Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa ziliiwekea masharti Tanzania ili iweze kuingia kwenye programu ya urekebishaji wa uchumi baada ya kutokea kwa mdororo wa uchumi, kuanzia katikati ya miaka ya 1970.

Katika kipindi hiki harakati za maendeleo nchini Tanzania ziliambatana na uanzishaji wa soko huria. Uchumi wa soko huria ni mfumo wa uchumi ambao serikali huandaa mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kushiriki katika shughuli za uchumi wa taifa. Serikali ikiweka mazingira wezeshi ikiwa ni pamoja na utungaji na usimamiaji wa utekelezaji wa sera zinazohusu uzalishaji mali. Kwa hiyo serikali hujitoa kwenye shughuli za kumiliki na kuzalisha mali. Aina hii ya uchumi inawawezesha watu na kampuni binafsi au taasisi yoyote kumiliki njia za uzalishaji mali kinyume na ilivyokuwa kabla ya mwaka 1985. Hii ikiwa ni moja ya masharti yaliyowekwa na programu ya urekebishaji wa uchumi nchini. Hivyo serikali katika kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi ilifanya mabadiliko ya sera za kiuchumi. Kipindi hiki ulishuhudiwa uwekezaji katika kujenga na kuendeleza viwanda nchini. Vilevile, kulifanyika ubinafsishaji wa viwanda na mashirika mengine kama vile mashamba, mfano mashamba ya mkonge, chai na kahawa. Katika kipindi hiki, nchi imeendelea kuimarika kiuchumi, na kukabiliana na ushindani kutoka nchi nyingine. Pia, pamekuwepo na kuimarika kwa njia za usafirishaji mfano barabara, madaraja, upanuzi wa bandari ya Dar es Salaam, uundaji wa vivuko mbalimbali na masoko ya bidhaa ghafi. Kielelezo namba 1 kinaonesha Daraja la Watembea kwa Miguu Furahisha mkoani Mwanza.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kielelezo namba 1:** *Daraja la watembea kwa miguu Furahisha-Mwanza*

### (c) Maendeleo ya kijamii

Maendeleo katika nyanja ya kijamii yalijikita katika kuboresha huduma za jamii, kama afya, elimu, makazi, maji na umeme. Kwa upande wa sekta ya afya, serikali na mashirika binafsi yamejenga na kuboresha hospitali, zahanati, vituo vya afya na utoaji wa elimu ya afya ya jamii katika maeneo mbalimbali nchini. Vilevile, maendeleo katika sekta ya elimu yameenda sambamba na ujenzi wa shule za sekondari katika kila kata, kuongezeka kwa idadi ya vyuo vya kati na vyuo vikuu, upanuzi na uboreshaji wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia, kuongezeka kwa udahili na usajili wa wanafunzi kwa ngazi zote za elimu, kuongezeka kwa idadi ya walimu na wahitimu na kusaidia kupunguza idadi ya watu wasiojua kusoma na kuandika nchini. Katika kipindi hiki serikali, taasisi na watu binafsi waliwekeza na kuboresha katika kutoa huduma za makazi, umeme na maji. Programu ya urekebishaji wa uchumi iliitaka serikali kutoza malipo kwa wananchi katika kuchangia gharama za huduma za jamii kama vile, elimu, afya, makazi, umeme na maji. Hata hivyo, kuanzia mwaka 2016 serikali imeamua kutoa elimu bila malipo kuanzia elimu ya awali hadi sekondari kidato cha nne. Kielelezo namba 2 kinaonesha Hospitali ya Taifa Muhimbili, Tawi la Mloganzila jijini Dar es Salaam.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 113 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kazi ya kufanya namba 5**

1. Taja maendeleo ya uchumi na jamii katika awamu ya sasa yaliyopatikana kuanzia mwaka 1985.
2. Taja faida za kutoa elimu bure nchini.




**Kielelezo namba 2:** *Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila, Dar es Salaam*

**Chanzo:** *https://globalpublishers.co.tz/wwf-yaungana-na-wanawake-kupanda-miti-100-mloganzila*

## (d) Maendeleo kiutamaduni

Kipindi hiki cha kukua kwa demokrasia ya mfumo wa vyama vingi nchini kiliambatana na wingi wa vyombo vya habari, uhuru wa kujieleza, kupanuka kwa asasi za kiraia, kuendeleza michezo na sanaa na kukua kwa sayansi na teknolojia. Hali hii, ilisababisha kuwepo kwa muingiliano kati ya nchi ya Tanzania na mataifa ya nje, hasa Ulaya, Asia na Amerika. Muingiliano huu ulileta athari katika utamaduni wa Watanzania katika mfumo wa maisha, mfano mavazi, elimu, aina ya vyakula, burudani, lugha na mengine mengi.



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 114 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Changamoto za harakati za maendeleo nchini kipindi cha 1986 hadi sasa

Pamoja na maendeleo ambayo Tanzania imefikia katika kipindi cha 1986 hadi sasa, bado kuna changamoto mbalimbali zinazokabili maendeleo katika nyanja za kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni. Katika kipindi hicho, nchi ilikumbana na ukosefu wa mifumo imara ya ukusanyaji kodi kutoka kwa wawekezaji binafsi. Hali hii ilisababisha serikali kushindwa kuendeleza mifumo wezeshi ya uwekezaji katika sekta ya uchumi. Kushindwa kuendelezwa kwa vyanzo vya uzalishaji mali vilivyokuwa vimebinafsishwa kinyume na matarajio ya serikali. Pia, rasilimali nyingi kama vile madini yamemilikiwa na kuporwa na kampuni za kibepari kutoka nje. Hata hivyo, kutokana na kipato kidogo cha Watanzania, baadhi ya wananchi wameshindwa kulipia huduma mbalimbali za jamii kama vile, elimu, afya, umeme, usafiri na maji. Kutokana na hali hii, mwaka 2016 serikali iliridhia kutoa elimu bila malipo kuanzia ngazi ya awali hadi kidato cha nne. Kwa upande wa afya, serikali inagharamia sehemu ya gharama ya afya kwa wananchi waliojiunga na bima ya afya.

## Mbinu za kukabiliana na changamoto za harakati za maendeleo awamu ya sasa

Serikali imeweka mikakati mbalimbali ili kukabiliana na changamoto zinazokwamisha maendeleo nchini. Serikali imeanzisha mifumo imara na thabiti ya ukusanyaji wa kodi. Hali hii imezuia upotevu wa mapato nchini. Vilevile, uwepo wa mifumo imara ya udhibiti wa umiliki, uchimbaji na uuzaji wa madini, mfano kuwepo kwa masoko ya madini kila mkoa. Aidha, ujenzi wa ukuta wa Mirelani ni miongoni mwa mikakati ya hivi karibuni kukabiliana na utoroshaji na ukwepaji kodi katika biashara ya madini ya Tanzanite. Vilevile, serikali imeendelea kuhamasisha uzalendo, ili jamii ithamini rasilimali za taifa na kujituma katika uzalishaji mali. Hali hii itayawezesha mashirika ya umma kujiendesha kwa faida, mfano shirika la ndege, reli, mawasiliano (TTCL) na posta. Utunzaji na uendelezaji wa mazingira, mfano katazo la serikali la utengenezaji, usambazaji na matumizi ya mifuko ya plastiki ili kutunza mazingira. Kuhusu masuala ya siasa serikali inafanya juhudi kutoa elimu na kusimamia vizuri mahusiano ya vyama vya siasa.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya namba 6**

Orodhesha maendeleo ya kiuchumi na kijamii yaliyopo sasa katika mkoa unaoishi.

## Zoezi la 3

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Linganisha mikakati ya maendeleo katika **safu A** na maendeleo yaliyofikiwa kwa kuchagua jibu sahihi kutoka **safu B**, kisha andika herufi ya jibu hilo katika nafasi uliyopewa.

| Safu A | Jibu | Safu B |
|---|---|---|
| (i) Utaifishaji wa njia kuu za uzalishaji mali na uchumi. | | (a) Demokrasia na uhuru wa habari nchini |
| (ii) Mikakati ya elimu kipindi cha mwaka 1986 hadi sasa. | | (b) Kufunguliwa kwa vyuo vikuu vya serikali, mashirika ya kidini na watu binafsi. |
| (iii) Mikakati ya kuboresha uchumi kipindi cha mwaka 1986 hadi sasa. | | (c) Ujenzi wa reli ya kisasa na ununuzi wa ndege. |
| (iv) Vyama vingi vya siasa | | (d) Maendeleo ya jamii |
| (v) Harakati za kiuchumi awamu ya sasa | | (e) Kupungua kwa maradhi ya kuambukiza na ya mlipuko. |
| (vi) Kutoa elimu ya afya | | (f) Ongezeko la wanafunzi ngazi ya elimu ya juu. |
| (vii) Utoaji wa elimu bure nchini. | | (g) Ongezeko la wanafunzi katika ngazi ya elimu msingi na sekondari |
| (viii) Kutoa mikopo kwa vikundi mbalimbali | | (h) Sera ya Ujamaa na kujitegemea kati ya mwaka 1967 hadi 1985. |
| | | (i) Ubinafsishaji na soko huria. |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Andika KWELI kwa sentensi ya kweli na SI KWELI kwa sentensi isiyo ya kweli katika nafasi uliyopewa.**

2. Azimio la Arusha lilikuwa na mpango wa kuwaondoa walowezi nchini. __________
3. Ukosefu wa mitaji ni changamoto kubwa katika kuendeleza mikakati ya maendeleo nchini. __________
4. Ukwepaji wa kodi unachangia kukosesha taifa mapato ya kuendeleza mipango ya maendeleo nchini. __________
5. Ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli na usafiri wa anga hauwezi kuleta maendeleo ya jamii nchini. __________
6. Soko huria linaharibu thamani ya vitu vya ndani na kuua viwanda vya ndani. __________

**Jibu maswali yafuatayo:**

7. Ainisha maendeleo ya kiuchumi Tanzania katika kipindi cha awamu ya sasa kuanzia mwaka 1985.
8. Eleza maendeleo ya elimu yaliyofikiwa katika kipindi cha awamu ya sasa kuanzia mwaka 1986.
9. Bainisha changamoto za maendeleo ya uchumi zilizokabili maendeleo ya uchumi nchini Tanzania katika kipindi cha mwaka 1967 hadi 1985.
10. Eleza ni kwa jinsi gani mikakati ya uchumi inaweza kutatua changamoto za maendeleo nchini kwa sasa.

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Changamoto | vitu vinavyozuia au kuzorotesha jitihada fulani |
| Mfumo | utaratibu wa kisiasa, kijamii au kiuchumi unaowaongoza watu fulani au taifa |
| Mikakati | mipango au shughuli za kufanya ili kufikia malengo fulani yaliyokusudiwa |
| Mipango | mikakati ya kufikia au kufikilia malengo ya taifa |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nane
# Matumizi ya ramani

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Sita, ulijifunza kuchora na kusoma ramani ya mkoa unaoishi na ramani ya Tanzania. Pia, ulijifunza kuchora na kusoma ramani katika mazingira yako ya kila siku. Katika sura hii, utajifunza kutofautisha mistari ya latitudo na longitudo. Vilevile, utajifunza jinsi ya kutumia mistari hii kubaini au kuonesha sehemu mbalimbali katika ramani. Aidha, utajifunza jinsi ya kukokotoa muda katika sehemu mbalimbali kwa kutumia mistari ya longitudo. Maarifa na ujuzi utakaopata katika sura hii utakusaidia kuwa na uwezo wa kubainisha na kuonesha mahali katika ramani na kukokotoa muda.*

## Dhana ya latitudo na longitudo

Mistari mbalimbali hutumika kuwasilisha taarifa katika ramani. Mistari ya longitudo na latitudo ni moja wapo ya mistari inayokuwezesha kutumia ramani. Ili kuitumia mistari hii inakupasa kuelewa dhana na kanuni ya matumizi yake. Dunia tunayoishi ni duara tenge lililogawanywa kwa mistari ya kufikirika ya ulalo iitwayo *latitudo* na mistari ya wima iitwayo *longitudo* kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 1. Mstaridunia mkuu uitwao longitudo ya Meridiani au Meridiani kuu huigawa dunia katika vipande vikuu viwili vya wima vilivyo sawa vya Mashariki na Magharibi. Aidha, mstaridunia mkuu uitwao Ikweta, huigawa dunia katika vipande viwili vikuu vya ulalo vilivyo sawa viitwavyo vizio. Vizio hivi ni kizio cha Kaskazini na Kizio cha Kusini. Mistaridunia huwasilishwa katika nyuzi za latitudo na longitudo. Nyuzi hizi huwasilishwa kwa alama yake maalumu ya °, kwa mfano 360°.




**Kielelezo namba 1**: *Mistari ya Latitudo na Longitudo*

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 118 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Latitudo

Latitudo ni mistari ya kufikirika ya ulalo ambayo huchorwa juu ya uso wa dunia Kaskazini na Kusini mwa Ikweta. Mstari wa Ikweta ni mstari wa latitudo wenye nyuzi sifuri, yaani $0^0$ kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 2. Mstari huu huigawa dunia katika vizio viwili vilivyo sawa; kizio cha Kaskazini na Kusini. Mistari ya latitudo huchorwa sambamba na Ikweta hivyo haikutani popote. Thamani ya nyuzi za mistari ya latitudo huhesabiwa kutoka Ikweta na hubainishwa kulingana na kizio kinachohusika. Pamoja na latitudo ya Ikweta, zipo latitudo zingine muhimu. Latitudo hizo ni Tropiki ya Kansa yenye nyuzi 23½ Kaskazini mwa Ikweta; Duara la Aktiki lenye nyuzi 66½ Kaskazini mwa Ikweta; Tropiki ya Kaprikoni yenye nyuzi 23½ Kusini mwa Ikweta; na Duara la Antaktiki lenye nyuzi 66½ Kusini mwa Ikweta. Latitudo hizi muhimu zinaunda duara ambapo thamani ya nyuzi za latitudo hizi huongezeka inapochorwa kutoka Ikweta kuelekea Kaskazini na Kusini. Mstari wa Ikweta ni latitudo pekee inayounda vizio vya duara kubwa. Ikweta husaidia katika kutafuta njia fupi ya usafiri majini na angani.




**Kielelezo namba 2**: *Mistari ya Latitudo*

## Longitudo

Longitudo ni mistari ya kufikirika ya wima iliyochorwa katika uso wa dunia kutoka ncha ya Kaskazini hadi ncha ya Kusini. Meridiani Kuu (au Meridiani ya Greenwich) ni mstari wa longitudo wenye nyuzi sifuri, yaani $0^0$ ambao unachorwa katikati ya dunia kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 3. Mistari ya longitudo huchorwa Magharibi na Mashariki mwa Meridiani kuu, ikiunganisha maeneo mbalimbali ya dunia. Dunia ina jumla ya nyuzi 360. Kutokea kwenye mstari mkuu wa meridiani, longitudo zingine zinachorwa



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 119 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kila baada ya nyuzi 15 kuelekea Mashariki na Magharibi mwa longitudo kuu hadi ifikie nyuzi 180 katika pande zote. Kila mstari wa longitudo hutengeneza duara kubwa. Latitudo na longitudo zinatofautiana kwa namna mbalimbali kama inavyoainishwa katika jedwali.




**Kielelezo namba 3**: *Mistari ya Longitudo*

**Jedwali kuonesha utofauti wa latitudo na longitudo**

| **Latitudo** | **Longitudo** |
|---|---|
| 1. Latitudo yenye nyuzi sifuri au 0° huitwa Ikweta. | Longitudo yenye nyuzi sifuri au 0° huitwa Meridiani Kuu. |
| 2. Ikweta ndiyo latitudo pekee inayotengeneza duara kubwa na kuigawa dunia katika sehemu mbili zilizo sawa yaani kizio cha Kaskazini na kizio cha Kusini. | Kila longitudo hutengeza duara kubwa hivyo kuweza kuigawa dunia katika sehemu kuu mbili. |
| 3. Latitudo ni mistari ya ulalo na huchorwa sambamba na Ikweta hivyo haikutani popote. | Longitudo ni mistari wima na yote hukutana katika ncha ya Kaskazini na pia katika ncha ya Kusini. |
| 4. Latitudo huhesabiwa kuanzia nyuzi sifuri ilipo Ikweta (0°) hadi nyuzi tisini (90°) kuelekea kizio cha Kusini au Kaskazini. | Longitudo huhesabiwa kuanzia nyuzi sifuri ilipo Meridiani Kuu(0°) hadi $180^0$ kuelekea Mashariki au Magharibi. |
| 5. Latitudo husaidia kuonesha mgawanyo wa maeneo yenye sifa mbalimbali za tabianchi. | Longitudo hutumika kuonesha tofauti ya muda kati ya sehemu moja ya dunia na sehemu nyingine. |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 1**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza maana ya mistari ya longitudo na latitudo.
2. Chora umbo la dunia na uoneshe mistari muhimu ya latitudo pamoja na mstari wa Meridiani kuu.

## Matumizi ya latitudo na longitudo

Mistari ya latitudo na longitudo ina matumizi yafuatayo:

(a) Kuonesha maeneo katika ramani: Mistari ya latitudo na longitudo hutumika kuonesha mahali katika uso wa dunia. Mfano, Tanzania inapatikana kutoka latitudo 1° hadi 12° Kusini, na pia kutoka longitudo 29° 30′ hadi 40° 35′ Mashariki kama Kielelezo namba 4 kinavyoonesha;

(b) Kupima umbali wa maeneo katika ramani: Mistari ya latitudo inapokutana na mistari ya longitudo inatengeneza nukta-kutano. Nukta-kutano hiyo hutumika kuonesha mahali hivyo kuweza kupima umbali wa eneo hilo na eneo lingine katika uso wa dunia. Kila sehemu juu ya uso wa dunia ni nukta-kutano yenye thamani fulani ya latitudo na longitudo. Mfano sehemu "A" iliyopo latitudo 0° 00′ na longitudo 35° 00′ Mashariki na sehemu "B" iliyopo latitudo 5° 00′ Kusini na longitudo 40° 00′ Mashariki. Kutokana na matumizi haya ya latitudo na longitudo, umbali uliopo baina ya sehemu hizo mbili unaweza kupimwa na kufahamika kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 4;

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 121 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




**Kielelezo namba 4:** *Nukta-kutano za latitudo na longitudo kwenye eneo A na B*

(c) Kubaini siku na tarehe za sehemu mbalimbali duniani kwa kuzingatia mstarihi;

(d) Kuonesha njia za vyombo vya usafiri wa anga na majini. Hutumika kusaidia nahodha na rubani kubaini njia fupi za kusafiri;

(e) Mistari ya longitudo hutumika kukokotoa muda wa mahali katika dunia; na



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 122 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(f) Mistari ya latitudo husaidia kubainisha sifa za tabianchi ya maeneo mbalimbali ya dunia kulingana na umbali wake kutoka mstari wa Ikweta. Kwa mfano, jotoridi hupungua kadiri unavyotoka katika eneo la Ikweta kuelekea katika kizio cha Kaskazini au Kusini.

## Kutafuta muda wa mahali katika ramani kwa kutumia longitudo

Mistari ya longitudo inakuwezesha kujua muda wa sehemu mbalimbali katika dunia. Ni muhimu kufahamu kanuni za msingi zinazotuwezesha kukokotoa muda wa mahali kwa kutumia longitudo. Pia, ni muhimu kufahamu namna ya kutafuta longitudo ya mahali kwa kutumia muda. Fahamu kuwa mzunguko mmoja wa dunia katika mhimili wake ni sawa na nyuzi 360 za duara. Dunia hutumia saa 24 kutimiza mzunguko huo. Kwa hiyo, dunia hutumia muda wa saa moja (au dakika 60) kutimiza mzunguko wa nyuzi 15. Hii inamaanisha kwamba, dunia inapojizungusha katika mhimili wake hutumia dakika 4 kwa kila nyuzi 1 ($1^\circ$) ya longitudo. Hivyo basi, tunaweza kupata kanuni muhimu ya kukokotoa muda wa mahali husika kama ifuatavyo:

(i) Ikiwa dunia hutumia saa 24 kumaliza mzunguko mmoja wa nyuzi 360, je, itatumia muda gani kuzunguka nyuzi 15?

Njia: $360^\circ \longrightarrow$ saa 24

$15^\circ \longrightarrow$ saa?

Kisha tunazidisha kwa njia ya mkasi ($\times$)

$$\frac{15^\circ \times \text{Saa } 24}{360^\circ}$$

$$\text{Saa } \frac{360}{360}$$

= Saa 1

Hivyo dunia itatumia muda wa saa 1 kuzunguka nyuzi 15

(ii) Ikiwa dunia hutumia muda wa saa moja kuzunguka nyuzi 15, je itatumia muda gani kuzunguka nyuzi moja?

Njia: $15^\circ \longrightarrow$ saa 1

$1^\circ \longrightarrow$ saa?

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 123 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kisha tunazidisha kwa njia ya mkasi (×)

$$\frac{1^\circ \times \text{saa } 1}{15^\circ}$$

$$\frac{\text{saa } 1}{15}$$

Ikumbukwe kuwa saa 1 ni sawa na dakika 60

Kwahiyo:

$$\frac{\text{dakika } 60}{15}$$

= dakika 4

Hivyo, dunia itatumia muda wa dakika 4 kuzunguka nyuzi 1.

Kwa mujibu wa kanuni hizo, muda unaotumiwa na dunia kujizungusha kwenye mhimili wake katika longitudo mbalimbali ni kama ifuatavyo:

(a) Dakika 4 kuzunguka nyuzi 1 (dakika 4 $\longrightarrow$ $1^\circ$)

(b) Saa 1 kuzunguka nyuzi 15 (saa 1 $\longrightarrow$ $15^\circ$)

(c) Saa 24 kuzunguka nyuzi 360 (saa 24 $\longrightarrow$ $360^\circ$)

Kanuni hizi ni muhimu kwani hutumika katika kukokotoa muda wa mahali husika.

Angalia mfano ufuatao wa namna ya kutumia thamani ya nyuzi za longitudo ili kujua muda unaotumika katika mzunguko wa nyuzi, kisha ujibu maswali yanayofuata.

**Mfano:**

Ikiwa dunia hutumia saa 1 kuzunguka nyuzi 15, je itachukua muda gani kuzunguka nyuzi 90?

Zingatia kanuni ifuatayo

$15^\circ \longrightarrow$ saa 1

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Njia: $15^\circ \longrightarrow$ saa 1

$90^\circ \longrightarrow$ saa?

(a) Tafuta uwiano kwa kuzidisha nyuzi 90 kwa saa 1, kisha gawanya kwa nyuzi 15

$$\frac{90^\circ \times \text{saa } 1}{15^\circ}$$

(b) Gawanya nyuzi 90 kwa nyuzi 15.

$$\frac{90^\circ}{15^\circ}$$

$$= 6$$

(c) Jibu ambalo litapatikana zidisha kwa saa 1. Katika mfano huu namba iliyopatikana ni 6 inayozidishwa kwa saa 1.

(d) Hivyo, dunia itatumia muda wa saa 6 kuzunguka nyuzi 90.

**Zoezi la 2**

**Jibu swali lifuatalo:**

Ikiwa dunia hutumia saa 1 kuzunguka nyuzi 15, je itatumia muda gani kuzunguka nyuzi zifuatazo?

(a) $180^\circ$

(b) $225^\circ$

(c) $120^\circ$

**Kutafuta muda kwa kutumia longitudo zilizopo upande mmoja na pande tofauti za Meridiani Kuu**

Unaweza kutafuta muda wa sehemu mbili zinazopatikana katika upande mmoja yaani Mashariki au Magharibi mwa Meridiani Kuu. Pia, unaweza kutafuta muda wa sehemu mbili zinazopatikana pande mbili tofauti yaani moja Mashariki na nyingine Magharibi mwa Meridiani Kuu. Ikumbukwe kwamba unapotafuta muda wa sehemu mbili zilizoko upande mmoja inakupasa kutafuta tofauti zake kwa kutoa nyuzi hizo mbili. Lakini, unapotafuta muda wa sehemu mbili zilizoko pande tofauti inakupasa kutafuta tofauti zake kwa kujumlisha nyuzi hizo mbili. Hii inatokana na mzunguko wa dunia

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kujizungusha kwenye muhimili wake ambapo kadiri unavyoelekea Mashariki mwa dunia saa huongezeka na kadiri unavyoelekea Magharibi mwa dunia saa hupungua. Ni vema kufahamu kwamba, dunia inapojizungusha katika muhimili wake, hufanya hivyo kutoka Magharibi kuelekea Mashariki. Hii hufanya watu walioko mashariki ya mahali fulani katika uso wa dunia kuwahi kuona mawio na machweo ya Jua mapema zaidi kuliko walioko magharibi ya sehemu hiyo.

***Kutafuta muda wa longitudo zilizo upande mmoja wa Meridiani Kuu***

Mfano 1:

Ikiwa ni saa tatu asubuhi katika mji "A" unaopatikana longitudo 30° Mashariki, je itakuwa ni saa ngapi katika mji "B" unaopatikana longitudo 60° Mashariki?

**Njia:**

Hatua za kufuata:

(a) Tafuta tofauti kati ya longitudo ya mji "A" na longitudo ya mji "B". Kwa kuwa miji yote iko Mashariki mwa Meridiani kuu tofauti ya nyuzi za longitudo hupatikana kwa kuchukua nyuzi kubwa na kutoa ile ndogo.

$60° - 30° = 30°$

(b) Tafuta tofauti ya muda wa mji "A" na ule wa mji "B"

Kwa kuwa muda wa mji "B" hatujapewa na tofauti ya longitudo kati ya mji "A" na "B" ni 30°, tunatafuta muda huo kwa kutumia kanuni ya mzunguko wa dunia. Dunia hutumia saa 1 kuzunguka nyuzi 15.

Saa 1 ⟶ 15°

Saa ? ⟶ 30°

Kisha zidisha kwa njia ya mkasi (×)

$$\frac{30° \times \text{saa } 1}{15°} = \text{saa } 2$$

Tofauti ya muda wa mji "A" na ule wa mji "B" ni saa 2

(c) Tafuta muda wa mji "B" kwa kuongeza au kupunguza ile tofauti ya muda kati ya mji "A" na mji "B"



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kwa kuwa mji "B" upo Mashariki zaidi ya mji "A" hivyo kuwa mbele kwa muda, unajumlisha tofauti hizi za saa 2 na muda wa mji "A" ambao ni saa 3 asubuhi.

$3 + 2 = 5$

Saa 3 asubuhi + saa 2 = saa 5 asubuhi

Hivyo muda wa mji "B" unaopatikana longitudo 60° Mashariki utakuwa saa 5 asubuhi.

Mfano 2:

Ikiwa mji "D" ulioko 15° Magharibi ni saa 3:00 asubuhi. Tafuta muda wa mji "E" ulioko 45° Magharibi.

**Njia:**

Hatua za kufuata:

(a) Tafuta tofauti kati ya longitudo ya mji "D" na longitudo ya mji "E".

Kwa kuwa miji hii yote iko Magharibi mwa Meridiani Kuu, tofauti ya longitudo hupatikana kwa kutoa.

$45^\circ - 15^\circ = 30^\circ$

(b) Tafuta tofauti ya muda wa mji "D" na ule wa mji "E"

Kwa sababu muda wa mji "E" hatujapewa na tofauti ya longitudo kati ya mji "D" na "E" ni 30°, tunatafuta muda huo kwa kutumia kanuni ya mzunguko wa dunia: dunia hutumia saa1 kuzunguka nyuzi 15.

Saa 1 $\longrightarrow$ 15°

Saa? $\longrightarrow$ 30°

Kisha zidisha kwa njia ya mkasi (×)

$$\frac{30^\circ \times \text{saa } 1}{15^\circ} = \text{saa } 2$$

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Tofauti ya muda wa mji "D" na ule wa mji "E" ni saa 2

(c) Tafuta muda wa mji "E" kwa kuongeza au kupunguza ile tofauti ya muda kati ya mji "D" na mji "E".

Japo miji yote ipo Magharibi mwa Meridiani Kuu, lakini mji "E" upo Magharibi zaidi ya mji "D". Ikimaanisha mji "D" uko mbele kwa muda kuliko mji "E". Hivyo basi, kupata muda wa mji "E" tunatoa hizi saa 2 kutoka kwenye muda tuliopewa wa saa 3 asubuhi.

3 - 2 = 1

Saa 3 asubuhi - saa 2 = saa 1 asubuhi

Hivyo muda wa mji "E" unaopatikana longitudo 45° Magharibi utakuwa saa 1 asubuhi.

***Kutafuta muda wa longitudo zilizo pande tofauti za Meridiani Kuu***

Mfano 3:

Ikiwa mji "C" ulioko 45° Mashariki ni saa 7:00 mchana. Tafuta muda wa mji "D" ulioko 15° Magharibi.

**Njia**

Hatua za kufuata:

(a) Tafuta tofauti kati ya longitudo ya mji "C" na longitudo ya mji "D". Kwa kuwa miji hii ipo katika pande mbili tofauti za Meridiani Kuu yaani Mashariki na Magharibi, tofauti ya nyuzi za longitudo tunaipata kwa kujumlisha.

$45° + 15° = 60°$

(b) Tafuta tofauti ya muda wa mji "C" na ule wa mji "D"

Kwa sababu muda wa mji "C" hatujapewa na tofauti ya longitudo kati ya mji "C" na "D" ni 60°, tunatafuta muda huo kwa kutumia kanuni ya mzunguko wa dunia: dunia hutumia saa1 kuzunguka nyuzi 15.

Saa 1 ⟶ 15°

Saa? ⟶ 60°

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 128 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kisha zidisha kwa njia ya mkasi (×)

$$\frac{60^\circ \times \text{saa } 1}{15^\circ} = \text{saa } 4$$

Tofauti ya muda wa mji "C" na ule wa mji "D" ni saa 4

(c) Tafuta muda wa mji "C" kwa kuongeza au kupunguza ile tofauti ya muda kati ya mji "C" na "D".

Kwa kuwa mji "C" upo Mashariki na mji "D" upo Magharibi, kupata muda wa mji "D" tunatoa hizi saa 4 kutoka kwenye muda tuliopewa wa saa 7 mchana.

7– 4 = 3

Saa 7 mchana – saa 4 = saa 3 asubuhi

Hivyo muda wa mji "D" unaopatikana longitudo 15° Magharibi utakuwa saa 3 asubuhi.

**Zingatia:** Kama muda tuliopewa ni wa mji ulioko Magharibi mwa Meridiani Kuu, tunapaswa kuongeza ile tofauti ya muda kati ya mji "C" na mji "D" kupata muda wa mji ulioko Mashariki mwa Meridiani Kuu.

**Zoezi la 3**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Tafuta muda wa mji wa Malindi, Kenya uliopo longitudo 40° Mashariki ikiwa ni saa 9:00 alasiri katika mji wa Tunisi uliopo longitudo 10° Mashariki.
2. Tafuta muda wa mji "N" uliopo longitudo 60° Magharibi ikiwa mji "M" uliopo longitudo 30° Mashariki ni saa 7:00 mchana.
3. Tafuta Muda wa mji "X" uliopo longitudo 65° Magharibi ikiwa mji "Z" uliopo 10° Magharibi ni Saa 4:00 Usiku.

**Kutafuta longitudo ya mahali**

Pamoja na kutafuta muda wa mahali ambapo longitudo yake tumepewa, tunaweza kutafuta longitudo ya eneo iwapo tumepewa muda wa maeneo mawili na longitudo ya eneo mojawapo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mfano 4:

Tafuta longitudo ya mji "Y" ambao muda wake ni saa 9:00 alasiri ikiwa mji "Z" uliopo longitudo 40° Mashariki ni saa 7:00 mchana.

**Njia**

Hatua za kufuata:

(a) Tafuta tofauti ya muda uliopo kati ya mji "Y" na mji "Z"

9.00 – 7.00 = 2

(b) Tafuta tofauti ya longitudo

Kwa kuwa tumepata tofauti ya muda kati ya mji "Y" na mji "Z" ni saa 2, tunatafuta longitudo kwa kutumia kanuni ya mzunguko wa dunia ambayo ni: dunia hutumia dakika 4 kuzunguka 1°.

Badili saa ziwe dakika

saa 1 ⟶ dakika 60

saa 2 ⟶ dakika?

Kisha zidisha kwa njia ya mkasi (×)

$$\frac{\text{saa } 2 \times \text{dakika } 60}{\text{saa } 1} = \text{dakika } 120$$

Badili dakika ziwe katika nyuzi

1° ⟶ dakika 4

? ⟶ dakika 120

Kisha tunazidisha kwa njia ya mkasi (×)

$$\frac{1^\circ \times \text{dakika } 120}{\text{dakika } 4}$$

$$\frac{120^\circ}{4} = 30^\circ$$

(c) Tafuta longitudo ya mji "Y" kwa kujumlisha au kutoa nyuzi (°) ulizopata na zile za mji "Z" ulizopewa.

Kwa kuwa muda wa mji "Z" uliopo longitudo 40° Mashariki upo nyuma ya ule wa mji "Y", hivyo tunajumlisha 30° na 40° ulizopewa.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

$40^\circ + 30^\circ = 70^\circ$

Kwa hiyo longitudo ya mji "Y" itakuwa 70° Mashariki

## Zoezi la 4

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Andika majina ya latitudo zenye nyuzi zifuatazo:
   (a) 23½° Kaskazini
   (b) 66½° Kaskazini
   (c) 23½° Kusini
   (d) 0°
   (e) 66½° Kusini
2. Ikiwa mji "Y" wenye longitudo 40° Mashariki ni saa 4:00 asubuhi, je itakuwa saa ngapi katika mji "P" wenye longitudo 55° Mashariki?
3. Tafuta muda wa mji wa Tanga-Tanzania ulioko longitudo 39° Mashariki, ikiwa mji wa Kinshasa-Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ulioko longitudo 14° Mashariki, muda wake ni saa 6:00 mchana.
4. Tafuta longitudo ya mji "X" ambao muda wake ni saa 10:00 jioni, ikiwa mji "Y" uliopo longitudo 56° Magharibi ni saa 8:00 mchana.

**Chagua herufi ya jibu sahihi na uiandike herufi hiyo katika kisanduku.**

5. Mji upi utashuhudia mawio ya Jua mapema kabla ya miji mingine?
   (a) Mji uliopo 40° Mashariki
   (b) Mji uliopo 45° Magharibi [ ]
   (c) Mji uliopo 45° Mashariki
   (d) Mji uliopo 40° Magharibi
6. Eneo gani litashuhudia machweo ya Jua mapema kabla ya maeneo mengine?
   (a) Kasese 30° Mashariki [ ]
   (b) Tanga 39° Mashariki

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(c) Kisumu 35° Mashariki

(d) Bujumbura 29° Mashariki

7. Moja ya mambo yafuatayo **siyo** matumizi ya latitudo;

(a) kuonesha mahali katika ramani

(b) kuonesha njia za safari za anga na baharini

(c) kukokotoa muda wa mahali

(d) kuonesha umbali wa maeneo katika ramani

**Andika KWELI kwa sentensi ya kweli na SI KWELI kwa sentensi isiyo ya kweli katika nafasi uliyopewa.**

8. Nchi zilizo upande wa Mashariki mwa Meridiani Kuu muda wake uko mbele kuliko nchi zilizoko upande wa Magharibi mwa Meridiani Kuu. ___________

9. Longitudo kuu huitwa Ikweta. ___________

10. Dunia hutumia zaidi ya saa 24 kukamilisha mzunguko mmoja wa 360°. ___________

11. Mistaridunia ya latitudo na longitudo hutumika kuonesha mahali katika picha. ___________

12. Mstari wa Ikweta unaigawa dunia katika vipande viwili vikuu ambavyo ni kizio cha Mashariki na kizio cha Magharibi. ___________

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Duara Kubwa | ni duara ambalo huigawa dunia katika sehemu mbili zilizo sawa. Kila mstari wa longitudo hutengeneza duara kubwa |
| Mstarihi | mstari wa kimataifa wa tarehe unaofuata longitudo ya 180° |
| Nukta-Kutano | nukta au sehemu ambayo mistari miwili imekutana |
| Nyuzi | kipimio chenye kuonesha ukubwa wa pembe katika eneo |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tisa

# Mfumo wa Jua

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Sita ulijifunza mfumo wa Jua, dhana ya dunia kulizunguka Jua na matokeo yake. Pia, ulijifunza kuhusu kupatwa kwa Jua na mwezi na matokeo yake. Vilevile, ulijifunza jinsi ya kupanga shughuli zako kufuatana na mabadiliko ya hali ya hewa na majira ya mwaka yatokanayo na mzunguko wa dunia kulizunguka Jua. Katika sura hii, utajifunza Mfumo wa Jua na angahewa, dhana na umuhimu wa tabaka la ozoni; shughuli za binadamu zinavyoathiri tabaka la ozoni na jinsi ya kudhibiti athari hizo. Maarifa na ujuzi utakaoupata katika sura hii, utakusaidia kuwa na uwezo wa kufahamu mfumo wa Jua, angahewa na matabaka yake, umuhimu wa tabaka la ozoni na namna ya kuchambua shughuli za kufanya ambazo ni rafiki kwa mazingira na ambazo husaidia kutunza tabaka la ozoni. Pia, maarifa haya yatakupatia mbinu za kudhibiti shughuli za binadamu zinazoathiri tabaka la ozoni.*

## Mfumo wa Jua na angahewa

Ulimwengu unaundwa na mifumo ya nyota zaidi ya bilioni moja. Mfumo wa Jua hupatikana katika mojawapo ya mifumo hiyo. Mfumo wa Jua hujumuisha Jua, sayari, satilaiti, asteroidi, vimondo, vumbivumbi la angani na mabonge ya barafu. Jua lipo katikati ya mfumo huu. Katika mfumo wa Jua, Dunia ni sayari ya tatu kwenye mpangilio wa sayari zinazolizunguka Jua. Dunia iko umbali wa takribani kilomita milioni 150 (km 150 000 000) kutoka kwenye Jua. Kama ilivyo kwa sayari nyingine, Dunia imezungukwa na tabaka la hewa lenye mchanganyiko wa gesi mbalimbali. Tabaka hili huitwa angahewa.

## Angahewa

Angahewa ni tabaka la gesi mbalimbali linaloizingira dunia. Angahewa imegawanyika katika matabaka makubwa manne kutoka katika uso wa dunia kuelekea angani. Matabaka haya ni *angatropo, angastrato*, *angameso* na *angajoto* kama yanavyoonekana katika Kielelezo namba 1. Matabaka haya yamejipanga kulingana na kiwango cha jotoridi kilichopo katika kila tabaka.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 133 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




**Kielelezo namba 1:** *Matabaka ya angahewa*

## Angatropo

Hili ni tabaka la chini la angahewa kutoka kwenye uso wa dunia. Kimo cha tabaka hili kinakadiriwa kuanzia kilomita 0 hadi 10 kutoka katika uso wa dunia kuelekea juu angani. Binadamu na viumbe hai wengine tunaishi katika tabaka hili. Pia, shughuli zote za binadamu hufanyika katika tabaka hili. Ndege za abiria na za mizigo huruka katika anga hili. Katika angatropo jotoridi hupungua kadiri kimo kinavyoongezeka.

## Angastrato

Tabaka hili la anga linapatikana kati ya angatropo na angameso. Kimo cha tabaka hili kinakadiriwa kuwa kati ya kilomita 10 hadi 50 kutoka katika uso wa dunia kuelekea juu angani. Mara chache ndege za abiria na za mizigo huruka

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 134 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE
katika eneo la chini la tabaka hili iwapo katika angatropo kuna mawingu mazito. Angastrato ni muhimu sana kwa maisha ya viumbe hai kwani ndani yake kuna tabaka la ozoni ambalo huikinga dunia dhidi ya mionzi mikali ya Jua. Katika angastrato, jotoridi huongezeka kadiri kimo kinavyoongezeka. Hii hutokea kwa sababu tabaka la ozoni husharabu mionzi mikali ya utravaoleti inayotoka kwenye Jua.

### Angameso

Angameso ni tabaka la angahewa ambalo hupatikana juu ya angastrato. Kimo cha tabaka hili kinakadiriwa kuwa kati ya kilomita 50 hadi 85 kutoka katika uso wa dunia kuelekea juu angani. Hili ni tabaka lenye baridi kali. Katika tabaka hili jotoridi hupungua kadiri kimo kinavyoongezeka hadi kufikia nyuzijoto za sentigredi zipatazo -90 (yaani $-90^0$C) kwenye mpaka wa meso.

### Angajoto

Angajoto ni tabaka la anga la juu zaidi. Anga hili hupatikana juu ya mpaka wa meso. Kimo cha tabaka hili kinakadiriwa kuwa kati ya kilomita 85 hadi 1 000 kutoka katika uso wa dunia kuelekea juu angani. Katika tabaka hili jotoridi ni kubwa sana, linakadiriwa kufikia nyuzijoto za sentigredi 2 000. Katika tabaka hili, jotoridi huongezeka kadiri kimo kinavyoongezeka. Ongezeko hili la jotoridi husababishwa na tabaka hili la anga kusharabu mionzi mikali ya utravaoleti na eksirei inayotoka kwenye Jua. Kutokana na mpangilio huu wa angahewa jotoridi hutofautiana tofautiana kati ya usiku na mchana na katika majira mbalimbali ya mwaka. Anga hili, huakisi mawimbi ya redio, hivyo ni anga muhimu sana kwa mawasiliano.

### Zoezi la 1

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Angahewa ni nini?
2. Taja matabaka manne yanayounda angahewa
3. Shughuli za kila siku za binadamu hufanyika katika tabaka lipi la angahewa?
4. Taja vituo vikubwa vitatu vya redio vinavyopatikana nchini Tanzania ambavyo hutegemea mawimbi kutoka katika angajoto ili kurusha matangazo yake.
5. Taja faida tatu za angatropo katika maisha ya mwanadamu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Tabaka la ozoni

Tabaka la ozoni kama linavyoonekana katika Kielelezo namba 2, ni sehemu ya chini ya angastrato inayosharabu karibu mionzi yote mikali kama vile utravaoleti inayotoka kwenye Jua. Tabaka la ozoni linapatikana katika umbali wa kilometa 20 hadi 30 juu ya uso wa dunia. Tabaka hili linaundwa kwa gesi ya ozoni. Ozoni ni molekuli zenye atomi za oksijeni. Molekuli hizi za ozoni zina jumla ya atomi tatu za hewa ya oksijeni na huzalishwa na kuharibiwa katika angastrato. Tabaka hili lina kiwango kikubwa cha molekuli za ozoni kuliko sehemu nyingine za angahewa. Tabaka hili huzuia karibu mionzi yote mikali ya Jua kupenya katika uso wa dunia. Hivyo hutumika kama chujio la mionzi mikali, kama vile eksirei na utravaoleti inayotoka kwenye Jua isifike kwenye uso wa dunia na kusababisha madhara kwa maisha ya viumbe hai. Mionzi hii mikali ya Jua ni hatari na inaweza kuharibu au kudhuru na kuua viumbe hai.

Kwa kusharabu na kuzuia mionzi mikali na hatari inayotoka kwenye Jua, tabaka la ozoni hutukinga na magonjwa kama vile saratani ya ngozi na athari nyingine za kiafya. Hata hivyo, kemikali zinazotumika katika majokofu, manukato na marashi, unyunyizaji wa viua wadudu na katika vizimia moto, zimekuwa zikizalisha gesi ambazo zimepunguza kiwango cha ozoni katika angastrato. Pia, uyeyukaji wa theluji kwenye maeneo ya vizio hutoa kemikali zinazoathiri ozoni.  Athari hii inaonekana zaidi katika vizio vya Kaskazini na Kusini, hali hii husababisha kuwa na vishimo katika tabaka la ozoni viitwavyo vishimo - ozoni, mfano vishimo ozoni vya antaktiki. Kutokea kwa vishimo hivi kunaruhusu miale mikali na hatari ya utravaoleti kupenya na kufika duniani ambapo huathiri viumbe hai.




**Kielelezo namba 2:** *Tabaka la ozoni*



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 136 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Umuhimu wa tabaka la ozoni**

Tabaka la ozoni ni muhimu sana kwa viumbe hai kwani husadia katika mambo yafuatayo:

(a) Kuchuja mionzi mikali ya Jua: Mionzi mikali ya Jua isipochujwa katika tabaka la ozoni ni hatari kwa viumbe hai kama binadamu, wanyama na mimea. Viumbe hawa huathiriwa na mionzi ya ultravaoleti inayosababisha magonjwa kama vile saratani ya ngozi, macho, na kuharibiwa kwa seli za ngozi na kuzeeka kwa ngozi. Hivyo, mionzi mikali inapochujwa hupunguza uwezekano wa binadamu pamoja na viumbe hai wengine kuathiriwa na mionzi. Hii huepusha magonjwa na athari nyingine za kiafya kwa viumbe hai na mazingira kwa ujumla.

(b) Kudhibiti kiasi cha joto kinachotakiwa duniani: Mionzi ya Jua inaposafiri kuja kwenye uso wa dunia huchujwa katika tabaka la ozoni na hivyo baadhi ya mionzi kushindwa kupenya moja kwa moja na kuifikia dunia. Hali hii husaidia kupunguza joto duniani, na hivyo kupunguza athari za ongezeko la joto.

**Zoezi la 2**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza kwa kifupi maana ya tabaka la ozoni.
2. Tabaka la ozoni linapatikana katika tabaka lipi la angahewa?
3. Ni gesi ipi inapatikana kwa kiasi kikubwa katika tabaka la ozoni?
4. Unadhani, nini kingetokea kwa viumbe hai endapo tabaka la ozoni lisingekuwapo? Elezea.

**Shughuli za binadamu zinavyoathiri tabaka la ozoni**

Maisha ya mwanadamu yanategemea mazingira yanayomzunguka. Kwa hiyo, ili aweze kuishi na kukidhi haja ya maendeleo yake inampasa afanye shughuli mbalimbali kama vile usafirishaji, kilimo, ufugaji na uzalishaji mali kwa kutumia nishati. Shughuli hizi zimekuwa zikizalisha gesi zinazoharibu tabaka la ozoni. Gesi hizi zinatokana na kompaundi zilizotengenezwa na binadamu kama vile gesi za klorini, florini na kaboni (CFCs), gesi za halojeni, bromini na haidro-kloro-floro-kaboni (HKFK). Gesi zinazoharibu tabaka la ozoni zimekuwa zikitumika katika shughuli mbalimbali za binadamu kama vile;

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

matumizi ya vipoza hewa (viyoyozi) kwenye magari, majumbani, maofisini, na kwenye majokofu. Pia, viulia wadudu (viwatilifu), kutumia viyeyushi katika kufanya usafi na uzalishaji viwandani, na kufua nguo kwa mvuke. Hata hivyo, gesi za kloro-floro-kaboni hazitumiki tena katika vipoza hewa kwenye magari, majumbani na maofisini, na kwenye majokofu kutokana na mchango wake katika kuharibu tabaka la ozoni. Badala yake kompaundi ya Haidro-kloro-floro-kaboni hutumika, ijapokuwa pia, huchangia kuongezeka kwa joto duniani kwavile nayo ni gesijoto. Maelezo yafuatayo yanafafanua jinsi shughuli mbalimbali za binadamu zinavyochangia katika uharibifu wa tabaka la ozoni kwa kutumia au kuzalisha gesi haribifu kwa tabaka la ozoni.

(a) Utengenezaji na utumiaji wa vipoza hewa (viyoyozi) na majokofu: Vipoza hewa na majokofu mfano katika Kielelezo namba 3 (a) na (b), ni muhimu hasa kwa nchi za ukanda wa joto. Vipoza hewa hivi na majokofu hutumika kuhifadhi vyakula, dawa, na kupoza hewa katika chumba. Gesi haribifu kwa tabaka la ozoni zimekuwa zikitumika katika vipoza hewa vya kwenye magari, majumbani, maofisini, viwandani, na kwenye majokofu.

(b) Utumiaji wa viua wadudu: Gesi haribifu kwa tabaka la ozoni inatumika viwandani kuzalishia viua wadudu (viwatilifu), majumbani (kufukiza) na kunyunyiza mashambani. Kadhalika vifaa mbalimbali vya umeme husafishwa kwa kutumia gesi hizi.

(c) Kutengeneza magodoro: Baadhi ya gesi hizi hutumika katika kutengeneza magodoro viwandani. Gesi hizi ni kama vile klorofloroкaboni (KFK) na Haidro kloro-floro-kaboni (HKFK).

(d) Matumizi kwenye vifaa vya kuzimia moto: Gesi haribifu za tabaka la ozoni zitokanazo na halojeni zimekuwa zikitumika katika mifumo ya kuzimia moto.

(e) Viyeyushi: Baadhi ya gesi hizi kama vile kaboni tetrakloraidi imekuwa ikitumika kama kiyeyushi kwa ajili ya matumizi mbalimbali viwandani na majumbani. Mfano, kufanya usafi, kufua nguo kwa mvuke, na matumizi kwenye viwanda vya kemikali na dawa.

(f) Matumizi kwenye vipulizi (aerosoli): gesi ya klorofloroкaboni pia hutumika kama visukumizi kwenye vipulizi vya aerosoli kama vile uturi, rangi au dawa ya mbu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



3 (a) *Jokofu*



3 (b) *Kiyoyozi*

**Kielelezo namba 3:** *Mfano wa vifaa vinavyotoa gesi inayoharibu tabaka la ozoni*

**Vyanzo:** *https//thubajvc.files.wordpress.com/2014/02/fridge.jpg*
*https//www.indiamart.com/proddetail/old-window-ac-10839676230.html*

**Kazi ya kufanya namba 1**

Kwa usimamizi wa mwalimu wa somo, tembelea kiwanda kilichopo karibu, chunguza shughuli zinazofanywa kiwandani hapo, kisha andika ripoti ya ulichokibaini ukihusianisha na uharibifu wa tabaka la ozoni.

**Jinsi ya kudhibiti uharibifu wa tabaka la ozoni**

Uharibifu wa tabaka la ozoni unaweza kudhibitiwa kwa namna zifuatazo:

(a) Kununua vipoza hewa (viyoyozi) na majokofu ambayo hayatumii gesi haribifu za tabaka la ozoni. Hivyo, serikali idhibiti uingizaji na utengenezaji wa viyoyozi na majokofu yanayozalisha gesi hizi.

(b) Kununua vipulizi (aerosoli) visivyotumia visukumizi vya gesi haribifu za tabaka la ozoni.



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 139 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(c) Kuhakikisha gesi ya viyoyozi kwenye magari na majokofu haipotei angani wakati wa kubadilisha au matengenezo. Gesi hii irejelezwe kila inapowezekana.

(d) Kutumia malighafi mbadala katika kutengeneza bidhaa za viwandani zinazotumia gesi haribifu za tabaka la ozoni. Bidhaa hizo ni kama vile magodoro, viyeyushi, wino na viwatilifu.

(e) Matumizi ya teknoloja ya kisasa katika kutengeneza viyoyozi vya majumbani, kwenye magari na viwandani.

(f) Kudhibiti uingizaji wa viyoyozi na majokofu yanayozalisha gesijoto zinazochangia kuharibu tabaka la ozoni. Viyoyozi na majokofu bora ni yale yanayotumia nishati kwa ufanisi na kuzalisha kiasi kidogo sana cha hewa zinazoharibu tabaka la ozoni. Mara nyingi bidhaa hizi huwa na maelekezo kuhusu ufanisi katika matumizi ya nishati; na

(g) Kuboresha teknolojia katika mashine za viwandani kwa kuweka vichuja hewa ili kuizuia hewa yenye kemikali kufika angani.

Pamoja na namna mbalimbali za kudhibiti uharibifu wa tabaka la ozoni, mnamo mwaka 1987, nchi nyingi duniani ziliingia mkataba wa kupunguza matumizi ya gesi haribifu za tabaka la ozoni. Mkataba huu wa Montreal, Kanada, umeridhiwa pia na Tanzania. Matokeo ya mkataba huu ni kupungua kwa kiasi kikubwa cha uharibifu wa tabaka la ozoni. Hata hivyo bado umakini unahitajika katika kuhakikisha tabaka hili haliendelei kuharibiwa ili kulinda maisha ya viumbe hai duniani.

Pamoja na kwamba shughuli za viwanda, uchukuzi, uzalishaji wa nishati na kilimo ni muhimu katika maendeleo ya binadamu, ni muhimu, kuzifanya kwa umakini. Tusipokuwa makini tabaka la ozoni linaweza kuharibiwa na hatimaye kuhatarisha maisha ya viumbe hai vya sasa na vijavyo.

**Kazi ya kufanya namba 2**

Jadiliana na wenzako namna ya kudhibiti shughuli za binadamu ili zisiharibu tabaka la ozoni. Andaeni majibu na kuyawasilisha darasani.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 140 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3

**Jibu maswali yafuatayo:**

**A. Chagua herufi ya jibu sahihi na uiandike herufi hiyo katika kisanduku.**

1. Moja kati ya mambo yafuatayo huathiri uimara wa tabaka la ozoni;
   (a) upepo
   (b) hewa ya oksijeni
   (c) radi na mvua
   (d) gesi ya kloroflorokaboni

2. Tabaka la ozoni ni sehemu ya tabaka la chini la __________.
   (a) angatropo
   (b) angastrato
   (c) angameso
   (d) angajoto

3. Mionzi hatari ya Jua huchujwa katika tabaka gani?
   (a) Tabaka la ozoni
   (b) Tabaka la angameso
   (c) Tabaka la angajoto
   (d) Tabaka la angatropo

4. Moshi mzito unaotoka viwandani huwa na vitu gani vinavyoharibu tabaka la ozoni?
   (a) Hewa ya oksijeni
   (b) Harufu mbaya
   (c) Gesi haribifu
   (d) Upepo

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Mionzi ya Jua ya utravaoleti inaweza kusababisha nini?

   (a) Magonjwa ya ngozi kwa binadamu

   (b) Wadudu kuzaliana

   (c) Vichaka kuungua

   (d) Joto kupungua duniani

**B. Jaza nafasi zilizoachwa wazi**

6. Mionzi ya Jua huchujwa katika ____________ kabla ya kufika kwenye uso wa dunia.
7. Baadhi ya gesi zinazoharibu tabaka la ozoni ni ____________ na ____________.
8. Mionzi ya Jua isipochujwa huweza kusababisha ____________ na ____________ kwa mwanadamu.
9. Tabaka la ozoni ni la muhimu kwa sababu ____________ na ____________

**C. Jibu maswali yafuatayo**

10. Shughuli za kila siku za binadamu zinafanyika katika tabaka lipi la angahewa?
11. Ndege kubwa za mizigo huruka katika tabaka lipi la angahewa?
12. Eleza jinsi ambavyo viumbe hai vinaweza kuathiriwa endapo tabaka la ozoni litaharibiwa.
13. Elezea namna utakavyodhibiti uharibifu wa tabaka la ozoni katika eneo unaloishi.
14. Eleza kwa kifupi sifa za matabaka manne ya angahewa.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**D. Chunguza picha ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata**



15. Mkulima aliyepo katika picha D anafanya nini?
16. Taja hasara zitokanazo na kitendo anachofanya mkulima katika picha ukihusianisha na uharibifu wa tabaka la ozoni.

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Eksirei | mionzi inayoweza kupenya vitu na kuonesha vilivyomo ndani au kutoa picha za vitu vilivyomo |
| Sharabu | fyonza mwanga wa Jua |
| Ulimwengu | sehemu inayobeba nyota, sayari, vimondo na magimba mengine yanayoelea angani kama kitu kimoja |
| Ultravaoleti | mionzi mikali ya Jua yenye mawimbi mafupi ya urefu wa nm10 hadi nm 400 |
| Uturi | manukato, mafuta mazuri |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi

# Idadi ya watu na makazi

## Utangulizi

*Ulipokuwa Darasa la Sita ulijifunza rasilimali zilizopo Tanzania na maeneo zinakopatikana, mchango wa rasilimali zetu katika maendeleo ya taifa, vikwazo katika matumizi ya rasilimali zilizopo Tanzania na njia za kukabiliana na vikwazo hivyo. Pia, ulijifunza njia zinazochangia uharibifu wa rasilimali za Tanzania na mbinu za kulinda na kutunza rasilimali hizo. Katika sura hii, utajifunza kuhusu matumizi ya rasilimali na idadi ya watu, makazi ya watu, namna idadi na makazi ya watu vinavyoathiri shughuli za uzalishaji mali, sababu za mtawanyiko wa watu, na mambo yanayoathiri idadi ya watu. Vilevile, utabainisha madhara ya ongezekokasi la watu na namna ya kuyadhibiti. Maarifa na ujuzi utakaoupata katika sura hii, utakusaidia kuwa na uwezo wa kutambua uhusiano uliopo kati ya idadi ya watu na maendeleo katika jamii.*

## Dhana ya rasilimali



**Kumbuka**

1. Rasilimali zilizopo Tanzania
2. Rasilimali za asili
3. Rasilimali za kutengenezwa
4. Mifano ya rasilimali jadidifu

## Matumizi ya rasilimali na idadi ya watu

Watu ni mojawapo ya rasilimali muhimu kwa ajili ya maendeleo ya taifa. Rasilimali nyingine hutegemea rasilimali watu katika utunzaji, utumiaji na uendelezaji wake. Idadi ya watu na makazi vina mchango mkubwa katika

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 144 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

matumizi endelevu ya rasilimali. Idadi ya watu inapokuwa kubwa kuliko rasilimali zilizopo husababisha matumizi yaliyopitiliza, uchakavu, uharibifu na upotevu wa rasilimali hizo. Aidha, idadi ya watu inapokuwa ndogo rasilimali hutumika chini ya kiwango.

**Idadi ya watu**

Idadi ya watu ni jumla ya watu wanaoishi katika eneo fulani mfano kijiji, kata, wilaya, mkoa au nchi katika kipindi fulani. Idadi ya watu inajumuisha rika na jinsi zote za watu. Watu hawa wanaweza kuwa ni wa imani moja au tofauti, kabila moja au tofauti, watu waliotoka katika taifa moja au mataifa tofauti na wenye viwango tofauti vya elimu. Pia, wanaweza wakawa wanaishi pamoja au katika mtawanyiko. Watu wote hawa wakiwa katika eneo fulani kwa wakati fulani, tunaweza kupata idadi yao.

**Vyanzo vya kupata idadi ya watu**

Idadi ya watu inapatikana kutokana na vyanzo mbalimbali. Vyanzo hivyo ni sensa ya watu na makazi, tafiti, usajili wa vizazi na vifo, takwimu za uhamiaji na taarifa za usafiri wa ndani, pamoja na zile za kutoka katika ofisi za serikali za mitaa kuhusu idadi ya watu wanaohama na kuhamia katika eneo fulani. Baadhi ya njia za kupata idadi ya watu zimeelezewa kama ifuatavyo:

**Sensa ya watu na makazi**

Ni kitendo cha kuhesabu watu wa eneo kama vile vijiji, kata, tarafa, wilaya, mkoa au nchi. Ni mchakato wa kukusanya, kuchakata na kutangaza takwimu za idadi ya watu wa eneo fulani kwa wakati fulani kwa sababu fulani. Katika sensa kila mtu anapaswa kuhesabiwa kuanzia mtoto hadi mzee, awe wa jinsi ya kike au ya kiume, mfanyakazi au asiye mfanyakazi. Sensa pia huonesha muda na mahali ilipofanyika. Kuna aina mbili za sensa. Sensa ya kuhesabu watu kulingana na mahali wanapoishi; na ile ya kuhesabu watu kulingana na mahali watakapokutwa na wakala wa sensa siku ya kuhesabiwa.

Nchini Tanzania sensa hufanyika kila baada ya kipindi cha miaka 10. Kwa mara ya mwisho Tanzania ilifanya sensa ya watu na makazi mwaka 2012. Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, idadi ya Watanzania ilikuwa milioni 45. Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu inaonekana idadi ya watu Tanzania inaongezeka kwa kasi ambapo hadi kufikia mwaka 2020, idadi ya Watanzania ilikadiriwa kuwa zaidi ya milioni 59.8.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 145 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Ili sensa iwe na matokeo mazuri yapo mambo ambayo yanapaswa kuzingatiwa. Mambo hayo ni kama vile:

(a) Mtu kuhesabiwa mahali atakapokutwa na wakala wa sensa siku ya kuhesabiwa au nyumbani anakoishi;

(b) Aina ya dodoso na maswali yatakayotumika yakidhi taarifa muhimu zinazotakiwa na serikali;

(c) Upatikanaji wa watu watakaohusika katika zoezi la sensa na jinsi ya kuwapa mafunzo;

(d) Kutoa taarifa kwa umma juu ya zoezi la sensa na umuhimu wake kwa wananchi na taifa kwa ujumla;

(e) Kutoa vifaa na usafiri kwa mawakala wa sensa; na

(f) Kutumia teknolojia bora zaidi ya kukusanyia, kuchakata, na kutangaza takwimu.

Kwa ujumla zoezi hili linahitaji maandalizi ya kutosha na ushiriki wa hali ya juu wa wananchi ili zoezi liweze kufanikiwa.

**Tafiti za watu na makazi**

Katika njia hii taarifa za kina za mtu, familia au sehemu ya watu wote wa eneo linalohusika huchukuliwa ili kuwakilisha idadi ya watu waliopo katika eneo hilo. Katika tafiti za watu na makazi, njia ya savei hutumika. Savei inahusu uchukuaji wa sampuli na ukusanyaji wa taarifa za watu wote waliomo katika kaya zilizoko kwenye sampuli hiyo. Pia, katika savei, taarifa za msingi kama vile uzalishaji, matumizi, na huduma za umma hukusanywa na kuchakatwa ili kupata taarifa ya kina. Matokeo yanayotokana na sampuli iliyochukuliwa huwakilisha jumla ya watu waliopo katika eneo ambalo sampuli imechukuliwa.

**Usajili wa vizazi na vifo**

Usajili wa vizazi na vifo ni njia mojawapo ya kuweza kupata idadi ya watu waliopo katika eneo fulani kwa wakati fulani. Njia hii inahusisha ukusanyaji wa taarifa za jumla ya watoto waliozaliwa katika eneo fulani kwa wakati fulani na jumla ya vifo vya watu vilivyotokea. Taarifa hizi hupatikana katika ofisi za vizazi na vifo. Jumla ya vizazi na vifo vilivyotokea katika eneo fulani

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

inaweza kutumika kupata idadi ya watu waliopo katika eneo hilo katika kipindi fulani. Njia hii husaidia kupata takwimu kwa urahisi, ingawa nchi nyingi hutumia sensa kupata idadi ya watu na makazi. Hata hivyo, katika nchi nyingi hasa zinazoendelea, yapo matatizo ya kupata taarifa kamili za vizazi na vifo. Miongoni mwa sababu zinazosababisha ukosekanaji wa taarifa hizo ni pamoja na watu kutotoa taarifa kuhusu vizazi na vifo vinavyotokea majumbani.

**Taarifa za uhamiaji**

Idadi ya watu katika eneo fulani hupatikana pia kwa kutumia taarifa zinazopatikana katika ofisi za uhamiaji. Taarifa hizi zinajumuisha idadi ya watu wanaohamia katika nchi na kuomba uraia wa kudumu baada ya kukidhi vigezo vya nchi inayohusika. Pia, inajumuisha idadi ya watu wanaohama kutoka nchi inayohusika kwenda nchi nyingine. Uhamiaji pia unaweza kufanyika ndani ya nchi kwa watu kutoka eneo moja kwenda eneo lingine.

**Zoezi la 1**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza maana ya rasilimali.
2. Taja faida mbili za rasilimali watu katika eneo unaloishi.
3. Eleza maana ya idadi ya watu.
4. Orodhesha mambo manne ambayo serikali inapaswa kuyazingatia ili sensa iwe na matokeo mazuri.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 147 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kazi ya kufanya namba 1**

1. Chunguza cheti chako cha kuzaliwa kisha orodhesha taarifa zote zilizopo.
2. Taarifa gani ungependa ziongezwe au kupunguzwa katika cheti hicho? Toa sababu za pendekezo lako.
3. Tafuta idadi ya watu iliyopo katika maeneo yafuatayo:
   (a) Nyumbani kwako
   (b) Darasani kwako
4. Katika vikundi vya wanafunzi wanne, kwa kutumia vyanzo mbalimbali kama vitabu, atlasi, tovuti na wavuti, tafuta taarifa zifuatazo kisha wasilisha darasani:
   (a) Nchi ya Afrika Mashariki yenye idadi ya watu karibu sawa na nchi ya Tanzania.
   (b) Nchi ya Afrika Mashariki yenye watu wengi zaidi na sababu nne za kuwa na wingi huo wa watu.
   (c) Nchi yenye watu wachache zaidi Afrika Mashariki. Unadhani nini sababu ya nchi hiyo kuwa na watu wachache?

## Makazi ya watu



**Fikiri**

1. Maana ya makazi.
2. Aina ya makazi.
3. Jinsi makazi yanavyoweza kuathiri shughuli za uzalishaji.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 148 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Binadamu huishi katika nyumba na huwa na majirani zake ambao pia huishi katika nyumba zao. Eneo hilo ambalo binadamu wanaishi huitwa makazi ya watu. Hivyo, makazi ya watu ni mahali ambapo binadamu huishi na kuanzisha jamii inayoingiliana. Makazi ya watu siyo uwapo wa nyumba tu au umbo la mji au kijiji, bali hujumuisha shughuli na huduma zinazofanyika, kama uzalishaji mali, huduma za elimu na afya, utamaduni, maeneo ya kupumzika na muonekano wa eneo hilo. Makazi yanaweza yakawa na watu wengi, au wachache. Kwa mfano kwa kawaida miji ina watu wengi wakati vijiji vina watu wachache. Makazi hurahisisha shughuli mbalimbali za kiuchumi kama uzalishaji mali, biashara, ukusanyaji wa kodi kutokana na mkusanyiko na mwingiliano wa watu. Hivyo, makazi ya watu huboresha uchumi wa mtu na taifa kwa ujumla. Pia, makazi hurahisisha utoaji wa huduma kwa jamii.

### Aina ya makazi

Makazi ya watu yanaweza kugawanywa katika aina kuu mbili. Makazi ya mjini kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 1 na makazi ya kijijini kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 2.



**Kielelezo namba 1:** *Makazi ya mjini*



FOR ONLINE USE ONLY

MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 149 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kielelezo namba 2:** *Makazi ya kijijini.*

Kwa kuchunguza Vielelezo namba 1 na 2 unaweza kupata sifa za makazi ya watu. Baadhi ya sifa hizo ni:

(a) Majengo katika makazi ya mjini yamekaribiana ikilinganishwa na makazi kwenye maeneo mengi ya vijijini. Hali hii husababishwa na uwapo wa idadi kubwa ya watu katika eneo dogo kwenye makazi ya mjini na idadi ndogo ya watu katika eneo kubwa kwenye makazi ya vijijini.

(b) Makazi ya mjini yanaambatana na miundombinu ya huduma za uchumi na jamii zilizo bora zaidi kuliko za vijijini.

(c) Makazi ya mjini huambatana na ujenzi wa nyumba bora zaidi ikilinganishwa na makazi ya vijijini.

**Muundo wa makazi ya watu**

Makazi ya watu yanaweza kujengwa kwa miundo mbalimbali. Miundo hii imegawanyika katika makundi matatu. Muundo wa kwanza ni ule wa makazi ya mstari. Katika muundo huu, nyumba hujengwa kwa kufuata barabara, reli, ziwa au mto. Watu hujenga makazi yao katika mtindo huu wakifuata upatikanaji wa huduma za kijamii kama usafiri wa barabara, reli, na usafiri wa majini. Pia, hujenga makazi yao katika mtindo huu ili kufuata fursa za kibiashara. Mtindo mwingine wa makazi ni ule wa makazi yanayojengwa kwa mkusanyiko katika sehemu moja. Makazi haya hujengwa katika mtindo huu ili kutumia huduma za kijamii zilizopo kama shule na hospitali. Pia hufuata



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 150 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

shughuli za kiuchumi kama masoko, viwanda, uchimbaji madini na shughuli za utalii. Mara nyingi huduma na shughuli hizi huwa chache au za pekee na kusababisha watu kukaa katika eneo moja la makazi. Pia, makazi huweza kujengwa kwa mtawanyiko au muachano. Mtindo huu wa makazi hutokana na uwapo wa eneo la ardhi la kutosha ambapo watu huamua kujenga makazi yao mbalimbali. Aidha, miundo yote ya makazi huathiriwa na sababu za kijiografia kama vile sura ya nchi, kiwango cha rutuba katika udongo, majanga ya asili na sheria za uhifadhi na utunzaji wa ardhi. Vielelezo namba 3 , 4 na 5 vinaonesha miundo mbalimbali ya makazi.



**Kielelezo namba 3**: *Makazi ya mstari*



**Kielelezo namba 4**: *Makazi ya mkusanyiko*



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 151 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kielelezo namba 5:** *Makazi ya mtawanyiko*

## Athari za idadi ya watu na makazi katika shughuli za uzalishaji mali

Idadi ya watu na hali ya makazi katika eneo fulani vina nafasi kubwa katika shughuli za uzalishaji mali. Katika sehemu hii utajifunza namna idadi ndogo au kubwa ya watu na hali ya makazi katika eneo inavyoathiri shughuli za uzalishaji mali.

### Idadi ndogo ya watu

Shughuli za uzalishaji mali hutegemea idadi ya watu wanaoishi katika eneo linalohusika. Eneo linapokuwa na idadi ndogo ya watu (ikilinganishwa na raslimali zilizopo), watu katika eneo hilo hushindwa kutumia ipasavyo rasilimali zilizopo hivyo kufanya uchumi na shughuli nyingine za maendeleo kudorora. Idadi ndogo ya watu katika eneo inaweza kuathiri shughuli za uzalishaji mali kwa namna mbalimbali. Baadhi ya athari hizo ni:

(a) Upungufu wa nguvukazi kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali kama vile kilimo na viwanda.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) Uchache wa bidhaa na masoko katika eneo linalohusika: Kutokana na uchache wa watu katika eneo, uwezo wa kununua bidhaa huwa mdogo. Hali hii inaweza kufanya bidhaa chache zinazozalishwa zikose soko. Hivyo, uzalishaji hupungua ili kuendana na ukubwa wa soko. Matokeo ya hali hii ni kudumaa kwa uchumi.

(c) Kiwango cha chini cha matumizi ya rasilimali kama vile madini, ardhi, wanyamapori, maji na misitu. Uchache wa watu husababisha matumizi madogo ya ardhi na rasilimali nyingine. Hali hii hufanya watu kushindwa kufikia maendeleo yanayokusudiwa.

(d) Hali duni ya maisha: Kutokana na uzalishaji mali kuwa chini, kiwango cha maisha ya watu pia huweza kuwa duni.

(e) Kilimo cha kuhamahama na makazi holela: idadi ndogo ya watu katika eneo kubwa hufanya watu kulima kwa kuhamahama na kujenga bila mpangilio. Watu huchoma misitu na kukata miti ilikusafisha maeneo kwaajili ya kilimo na makazi. Hali hii huweza kusababisha mmomonyoko wa udongo na uhaba wa mvua, hivyo kupungua kwa uzalishaji.

Hata hivyo, watu wachache katika makazi wakitumia ipasavyo rasilimali zao, wanaweza kujiletea maendeleo endelevu kwao wenyewe na kwa vizazi vijavyo.

**Idadi kubwa ya watu**

Eneo linapokuwa na idadi ya watu inayozidi uwezo wa raslimali zilizopo katika eneo hilo huathiri uzalishaji mali. Watu hutumia rasilimali zilizopo kwa kiwango kikubwa kuliko uwezo wa rasilimali hizo. Idadi kubwa ya watu katika eneo, hasa wengi wao wakiwa na upungufu wa maarifa inaweza kuathiri shughuli za uzalishaji mali kwa namna mbalimbali. Baadhi ya athari hizo ni:

(a) Kuharibu mazingira: Idadi kubwa ya watu husababisha kuharibika kwa mazingira kutokana na uhitaji kuzidi uwezo wa raslimali zilizopo na kwa hiyo kuwapo na uhaba wa rasilimali kama ardhi, maji na wanyamapori. Hali hii huweza kusababisha mmomonyoko wa udongo, hivyo kupungua kwa uzalishaji.

(b) Idadi kubwa ya watu husababisha uchafuzi wa mazingira ambamo uzalishaji mali hufanyika.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(c) Kupungua au kuharibika kwa rasilimali: Idadi kubwa ya watu husababisha rasilimali zilizopo kama madini na ardhi kutumiwa zaidi kupita kiwango kinachotakiwa na hivyo kusababisha kuisha, kupungua au kuharibika.

(d) Kuongezeka kwa gharama za huduma kwa jamii: Idadi kubwa ya watu inahitaji fedha na mali nyingi ili kutimiza mahitaji yake. Watu wanapokuwa wengi uhitaji huongezeka katika elimu, afya, uchukuzi na maeneo mengine ya huduma. Hii huipa serikali gharama kubwa katika kutimiza mahitaji yote ya wananchi wake.

(e) Ukosefu wa ajira. Idadi ya watu inapoongezeka kwa wingi kuliko shughuli za kiuchumi, huathiri soko la ajira. Hali hii husababisha uhitaji mkubwa wa ajira.

(f) Upungufu wa ardhi na chakula. Idadi ya watu inapoongezeka eneo la kuzalishia mali kama mashamba hutumiwa kama sehemu za makazi. Hii hufanya ardhi ya kilimo kupungua na kusababisha kupungua kwa uzalishaji wa chakula. Hali hii husababisha uhaba wa chakula katika nchi au eneo hilo. Mfano mkoa wa Kilimanjaro unakabiliwa na upungufu wa ardhi kutokana na idadi kubwa ya watu na makazi hasa maeneo ya milimani.

Hata hivyo, idadi kubwa ya watu ikiambatana na uwapo wa teknolojia inayofaa na masoko ya bidhaa za kilimo huchochea ugunduzi wa njia bora za matumizi ya raslimali katika eneo dogo na hivyo kuongeza tija katika kilimo. Kwa hiyo, idadi kubwa ya watu inaweza kuongeza uzalishaji mali.

**Athari ya makazi katika shughuli za uzalishaji mali**

Makazi ni mahali ambapo watu wanaishi na kufanya shughuli mbalimbali. Makazi yanaweza kuwa ya nyumba moja ya familia, kijiji, mji au jiji kubwa kama Dar es Salaam. Kuna aina mbili za makazi ya watu, makazi ya mjini na makazi ya vijijini. Aina za makazi na namna ujenzi wake ulivyopangiliwa huathiri shughuli za uzalishaji.

***Makazi ya mjini***

Makazi ya mjini yana mkusanyiko wa watu wengi katika eneo dogo na hivyo huwa na nyumba zilizosongamana. Miji hutofautiana kwa jinsi ujenzi wake ulivyopangiliwa na inavyokua. Miji inaweza kujengwa kwa mpangilio

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

au kiholela. Pia miji yaweza kukua kwa kwenda juu (wima) kwa kujenga maghorofa, na kwa kutanuka kufuata usawa wa ardhi. Hali hizi za ujenzi na ukuaji wa miji huathiri uzalishaji kama ifuatavyo:

(a) Mpangilio wa miji: Miji iliyojengwa kwa mpangilio hurahisisha shughuli za uzalishaji mali kwa kuwa hujengwa kulingana na mahitaji ya ardhi kwa shughuli mbalimbali za uzalishaji na utoaji wa huduma. Miji iliyojengwa kiholela huathiri uzalishaji kwa sababu mpangilio wake hauzingatii mahitaji tofauti ya uzalishaji. Mara nyingi husababisha mgongano katika matumizi ya nafasi kwa shughuli mbalimbali. Pia ujenzi holela huathiri ujenzi wa miundo mbinu kwa ajili ya kurahisisha uzalishaji mali na utoaji wa huduma. Hali hii hukwamisha uzalishaji mali na utoaji wa huduma na hivyo huongeza umaskini mjini.

(b) Jinsi miji inavyokua: Kukua kwa miji kwa kwenda juu na kwa kusambaa kuna athari tofauti katika uzalishaji mali. Miji inapokuwa kwa kwenda juu (kujenga maghorofa) husababisha msongamano wa watu katika eneo dogo. Hii yaweza kurahisisha ujenzi wa miundo mbinu na utoaji wa huduma. Pia makazi yenye msongamano wa watu ni chanzo cha masoko ya bidhaa na huduma yanayosaidia ukuaji wa uzalishaji. Pia hufanya shughuli zinazotegemeana kufanya uzalishaji kwa urahisi zaidi. Lakini kutanuka kwa miji inayokua kwa kusambaa huongeza gharama za ujenzi wa miundombinu na utoaji wa huduma. Sehemu nyingi zilizo pembezoni mwa miji hukosa miundo mbinu na huduma za kurahisisha uzalishaji. Hali hii huathiri uzalishaji na hivyo kufanya uchumi wa miji kuwa duni.

### *Makazi ya vijijini*

Vijiji ni makazi ambayo watu ni wachache ukilinganisha na mijini. Kwa kuangalia mpangilio wa nyumba, makazi ya kijijini hutofautiana. Kuna makazi mtawanyiko na makazi msongamano. Aina zote mbili hupatikana nchini Tanzania, japo makazi ya msongamano ni mengi zaidi kwa sababu ya sera ya ujamaa na kujitegemea iliyosisitiza uundaji wa vijiji vya aina hiyo. Hali hizi za makazi zinaathari tofauti katika uzalishaji vijijini. Katika vijiji vyenye msongamano wa nyumba, umbali kati ya nyumba ni mdogo kwa vile nyumba ziko karibu karibu. Lakini umbali kati ya makazi na sehemu za kazi (mashamba, vyanzo vya maji, nishati) ni mkubwa. Katika vijiji vyenye makazi mtawanyiko, kuna umbali mkubwa kati ya nyumba. Kwa kuwa nyumba zimejengwa katika mashamba, umbali kati ya nyumba na sehemu za kazi



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 155 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ni mdogo. Hali hizi za makazi ya vijijini zinaathiri uzalishaji kama ifuatavyo:

(a) Umbali mkubwa kati ya nyumba na mashamba huathiri kilimo kwa kuwa inakuwa ni gharama kubwa na vigumu kuhudumia mashamba ikiwa mkulima anatakiwa kutembea mwendo mrefu kwenda na kurudi kutoka shambani. Hii inaathiri uchukuaji wa zana za kilimo kupeleka shambani na mazao kutoka shambani kwenda nyumbani na sokoni. Pia huathiri uwezo wa mkulima kusimamia matumizi bora ya raslimali.

(b) Nyumba kuwa karibu karibu: Umbali mdogo kati ya nyumba na nyumba una faida ya kurahisisha ujenzi wa miundombinu na utoaji wa huduma za uzalishaji. Ili kuboresha kilimo wananchi huhitaji kuwezeshwa kwa kuwa na miundombinu kama ya barabara na masoko. Pia wanahitaji kupata huduma kama za afya, elimu na namna bora za kutumia raslimali. Haya hufanyika kwa urahisi iwapo wakazi wako karibu karibu. Pia huduma za utawala na ushirikishwaji wa wananchi zinakuwa rahisi zaidi.

(c) Umbali mkubwa kati ya nyumba na nyumba: Iwapo nyumba zitakuwa zimetawanyika, itaathiri ujenzi wa miundo mbinu na utoaji wa huduma za jamii kwa kuwa itakuwa gharama zaidi. Hii itadhoofisha matumizi bora ya rasilimali na itaathiri uzalishaji.

(d) Umbali mdogo kati ya makazi na mashambani: Nyumba inapokuwa imejengwa katika shamba la mkazi hurahisisha uzalishaji kwa kuwa mkazi hutumia muda na nguvu kidogo kufika sehemu ya kazi na maeneo yenye rasilimali kwa ajili ya kupata mahitaji ya nishati, maji na ujenzi.

**Zoezi la 2**

**Jibu maswali yafuatayo:**

**A. Jaza nafasi zilizoachwa wazi**

1. Mahali ambapo binadamu huishi na kuanzisha jamii inayoingiliana huitwa _____________.
2. Makazi ya watu yanaweza kugawanywa katika aina mbili ambayo ni _____________ na _____________.
3. Nyumba zilizosongamana katika eneo dogo ni kiashirio cha makazi ya _____________.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Makazi ya mstari hujengwa kwa kufuata ____________ na ____________.

**B. Jibu maswali yafuatayo**

5. Kuna uhusiano gani kati ya idadi ya watu na makazi ya watu?
6. Orodhesha athari tano za idadi kubwa ya watu katika shughuli za uzalishaji mali.
7. Orodhesha athari tano za idadi ndogo ya watu katika shughuli za uzalishaji mali.

## Mtawanyiko wa watu

Watu hawaishi katika sehemu moja, wametawanyika katika maeneo mbalimbali. Hali hii hufanya eneo au nchi kuwa na idadi tofauti ya watu katika maeneo mbalimbali. Katika sehemu hii utajifunza dhana ya mtawanyiko wa watu na sababu za mtawanyiko huo.

### Dhana ya mtawanyiko wa watu

Mtawanyiko wa watu ni namna wakazi walivyoenea katika eneo fulani kutokana na sababu mbalimbali za kijiografia, kisiasa, kihistoria, kiuchumi na kijamii. Mtawanyiko wa watu huonesha namna watu walivyosambaa katika eneo hilo.

Mtawanyiko wa watu unatofautiana kutoka eneo moja hadi jingine. Baadhi ya maeneo yana watu wengi, wakati maeneo mengine yana watu wachache na maeneo mengine hayana watu kabisa. Kwa misingi hiyo tunaweza kusema mtawanyiko wa watu hauko sawa katika maeneo yote.

Mtawanyiko wa watu katika mikoa ya Tanzania unatofautiana, kuna baadhi ya mikoa ina idadi kubwa ya watu kuliko mikoa mingine kama Kielelezo namba 6 kinavyoonesha. Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, na Kagera ina idadi kubwa ya watu. Mikoa iliyo na idadi ndogo ya watu ni pamoja na Lindi, Njombe, na Katavi. Miongoni mwa sababu za mtawanyiko huo wa watu ni pamoja na upatikanaji wa maliasili, fursa za kiuchumi, huduma za kijamii na aina ya udongo.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 157 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




**Kielelezo namba 6:** *Mtawanyiko wa watu Tanzania mwaka 2016*
**Chanzo:** *Ofisi ya Taifa ya Takwimu, April 2016*

## Sababu za mtawanyiko wa watu

Zipo sababu mbalimbali zinazofanya maeneo mbalimbali kuwa na idadi tofauti ya watu. Zifuatazo ni baadhi ya sababu hizo:

### Sababu za kijiografia

Aina ya udongo, hali ya hewa, uoto na sura ya nchi vinachangia kwa sehemu kubwa mtawanyiko wa watu. Kwa mfano, maeneo yenye udongo

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 158 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

wenye rutuba nyingi huwa na watu wengi zaidi kuliko maeneo yenye udongo wenye rutuba kidogo, mfano baadhi ya maeneo ya mkoa wa Kilimanjaro yenye udongo wa volkano wenye rutuba nyingi yana idadi kubwa ya watu. Shughuli nyingi za kilimo na ufugaji hufanyika katika maeneo yenye rutuba kwani udongo wake hustawisha mazao na upatikanaji wa majani kwa ajili ya malisho.

Maeneo yenye milima mikali mara nyingi huwa na watu wachache ukilinganisha na maeneo ambayo ni tambarare katika baadhi ya maeneo. Ujenzi na shughuli za kiuchumi hufanyika kwa shida, pia gharama za ujenzi huwa kubwa milimani ukilinganisha na maeneo ya mabondeni au tambarare. Maeneo yenye baridi ya kadiri na unyevunyevu kama baadhi ya maeneo ya mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Iringa, Kagera, Njombe na Mbeya yana watu wengi kwa sababu ni maeneo mazuri kwa kilimo. Maeneo yenye hali ya jangwa na ukame kama vile Dodoma, Singida na Tabora yana watu wachache kwa sababu ya ukame ambao huathiri kilimo na maisha ya watu kwa ujumla. Maeneo yenye misitu minene yana wanyama wakali na mbung'o. Hali hii huweza kuathiri shughuli za ufugaji, hivyo watu huhofia kuanzisha makazi jirani na maeneo hayo.

**Sababu za kiuchumi**

Watu hupenda kuishi maeneo yanayoruhusu shughuli za uzalishaji mali kama vile biashara, kilimo, uvuvi na viwanda. Miji mingi kama vile Dar es Salaam na Mwanza, pamoja na mambo mengine, uwapo wa fursa nyingi za kibiashara husababisha watu wengi kuhamia katika maeneo hayo. Maeneo yenye mashamba makubwa, uchimbaji wa madini na kwenye miji mikubwa pia huvutia watu wengi kufanya makazi. Maeneo haya hutoa ajira kwa wingi hivyo husababisha watu kuhamia. Wafanyabiashara wengi hupenda kukaa maeneo ambayo masoko ya bidhaa zao hupatikana kwa wingi.

**Sababu za kijamii**

Kuwapo kwa huduma bora za afya, elimu, njia za uchukuzi na mawasiliano, usalama pamoja na masoko makubwa hufanya eneo kuwa na idadi kubwa ya watu. Watu huhamia katika maeneo haya wakitoka maeneo mengine yenye huduma duni kufuata huduma hizo. Mfano, uwapo wa taasisi nyingi za elimu katika jiji la Dodoma kama vile Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Chuo cha Mipango, Chuo cha Biashara na Chuo cha Madini vimechangia kwa kiasi kikubwa watu kuhamia katika mji wa Dodoma.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya namba 2**

Shirikiana na wanafunzi wenzako katika vikundi vya wanafunzi 4 kufanya kazi zifuatazo:

1. Bainisha aina na muundo wa makazi ya watu ilivyo katika eneo unaloishi.
2. Eleza hali hiyo ya makazi inavyoathiri shughuli za uzalishaji mali katika eneo unaloishi.

Wasilisha kazi darasani.

**Zoezi la 3**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza jinsi sababu za kijiografia, kiuchumi na kijamii zinavyoweza kuathiri mtawanyiko wa watu.
2. Tumia Kielelezo namba 6, kuchunguza ramani ya Tanzania ukibainisha mikoa yenye:
   (a) Watu wengi zaidi. (b) Watu wachache zaidi.
3. Eleza sababu tatu za kuwapo kwa mtawanyiko wa watu kama ilivyo kwenye swali namba 2 (a) na (b).

## Mambo yanayoathiri idadi ya watu

Mambo yanayoathiri idadi ya watu ni mambo au vitu vinavyofanya idadi ya watu kuongezeka au kupungua katika eneo fulani. Yapo mambo mbalimbali yanayoweza kuathiri idadi ya watu mambo hayo ni; idadi ya watoto wanaozaliwa, idadi ya vifo, na uhamiaji. Muda wa kuishi ukiongezeka au kupungua pia huweza kuathiri idadi ya watu. Ufuatao ni ufafanuzi wa mambo yanayoathiri idadi ya watu:

**(a)** **Idadi ya watoto wanaozaliwa**: hii ni jumla ya watoto wanaozaliwa katika eneo fulani la kijiografia kwa wakati fulani. Watoto wanapozaliwa kwa wingi kuliko idadi ya watu wanao kufa inasababisha kuongezeka kwa idadi ya watu. Kwa mfano, nchi nyingi za Kusini mwa jangwa la Sahara watu wanazaliana sana, hivyo nchi hizo zina ongezeko kubwa la watu. Wakati kupungua kwa idadi ya watoto wanaozaliwa husababisha kupungua kwa idadi ya watu. Mfano, nchi nyingi zilizoendelea kuna idadi ndogo ya watoto wanaozaliwa, hivyo nchi hizo zina tatizo la kuwa

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

na idadi ndogo ya watu.

**(b)** **Vifo:** Vifo vinapokuwa vingi zaidi ya idadi ya watoto wanaozaliwa, ni sababu ya kupungua kwa idadi ya watu katika eneo hilo. Mfano, nchi nyingi zilizokumbwa na vita, au magonjwa ya mlipuko kama COVID-19 watu wake wengi walipoteza maisha na kusababisha upungufu mkubwa wa watu. Aidha, kupungua kwa idadi ya vifo husababisha kuongezeka kwa idadi ya watu katika eneo hilo.

**(c)** **Uhamiaji:** Idadi ya watu wanaohamia ikiwa kubwa zaidi ya wanaohama hufanya eneo hilo kuwa na ongezeko la watu. Mfano, Tanzania imekuwa ikipokea wahamiaji kutoka nchi mbalimbali kama vile Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Maeneo wanakotoka watu hawa, huwa na upungufu wa watu, wakati kwa upande wa Tanzania kunakuwa na ongezeko la watu.

## Kudhibiti mambo yanayoathiri idadi ya watu

Mambo yanayoathiri idadi ya watu hufanya idadi ya watu katika eneo fulani la kijiografia kwa wakati fulani kuwa kubwa au ndogo. Mambo hayo yanayosababisha kuongezeka au kupungua kwa idadi ya watu yanaweza kudhibitiwa. Zipo njia nyingi zinazoweza kusaidia kudhibiti mambo hayo kama ifuatavyo:

(a) Elimu ya afya ya uzazi itolewe kwa wanajamii ili iweze kuwa na idadi ya watoto wanaowahitaji. Pia, jitihada zifanyike kuzuia mimba za utotoni kwa kuipa jamii elimu kuhusu madhara yake. Aidha, elimu itolewe kwa jamii kuhusu faida za kuwa na nguvukazi ya kutosha na yenye tija kwa jamii;

(b) Vifo vinaweza kudhibitiwa kwa kuboresha huduma za afya, lishe pamoja na kuboresha miundombinu. Pia, kuelimisha jamii kuhusu afya bora na kupunguza au kuzuia ajali;

(c) Serikali idhibiti uhamiaji haramu. Uingiaji wa watu kiholela unachangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la watu katika eneo fulani;

(d) Upatikanaji wa elimu kwa vijana. Upatikanaji wa huduma ya elimu katika nchi huweza kudhibiti ongezeko la watu. Kwa mfano, wasichana wengi wanaotumia miaka mingi kwenye masomo mara nyingi huchelewa kuingia kwenye ndoa au kufanya uamuzi wa kupata watoto mapema. Hivyo kipindi cha uwezo wa kupata watoto huwa kimepungua; na

(e) Wanawake wapewe zaidi fursa za kushiriki katika shughuli za kiuchumi na maendeleo. Wanawake ambao hushiriki katika shughuli za kiuchumi na maendeleo mara nyingi huwa na idadi ndogo ya watoto kuliko wale ambao hawajishughulishi na shughuli za kiuchumi.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya namba 3**

Tembelea maeneo yenye watu wengi na maeneo yenye watu wachache, kisha:

(a) Bainisha mambo yanayoathiri idadi ya watu waliopo katika maeneo hayo.

(b) Eleza utakavyoshiriki kudhibiti mambo uliyoyabaini katika maeneo hayo.

Wasilisha kazi yako darasani

## Ongezekokasi la watu

Ongezekokasi la watu ni hali ya idadi ya watu kuongezeka kwa kasi. Ongezeko la watu likiwa linakua kwa kasi kuliko kiwango cha uzalishaji mali, huleta matatizo katika jamii. Katika nchi nyingi zinazoendelea ongezeko la watu ni kubwa zaidi kuliko ukuaji wa uchumi. Hii inasababishwa na idadi kubwa ya watoto wanaozaliwa katika kipindi cha muda mfupi, kuongezeka kwa muda wa wastani wa kuishi pamoja na ongezeko kubwa la wahamiaji kwa muda mfupi kama vile wakimbizi.

### Madhara ya ongezekokasi la watu

Yapo madhara ambayo hujitokeza katika mazingira kutokana na ongezekokasi la idadi ya watu. Madhara hayo ni pamoja na: uharibifu wa mazingira unaotokana na mahitaji makubwa ya eneo la kujenga na kulima; ongezeko la watoto waishio katika mazingira magumu na uchafuzi wa mazingira; kukosekana kwa huduma za kijamii kama vile dawa, huduma za uzazi salama; njaa inayotokana na serikali husika kulemewa na mzigo wa watu wengi; milipuko ya magonjwa inayotokana na uharibifu na uchafuzi wa mazingira. Uharibifu na uchafuzi huu wa mazingira unatokana na kipato duni cha watu na msongamano hivyo kushindwa kutupa taka ipasavyo; uhaba wa huduma za jamii kama vile shule, hospitali, na usafiri; upungufu wa rasilimali na ukosefu wa ajira. Hali hii hutokana na ongezeko la idadi ya watu lisilolingana na ukuaji wa uchumi wa nchi.

### Kudhibiti madhara ya ongezekokasi la watu

Madhara ya ongezekokasi la watu yanaweza kudhibitiwa kwa njia zifuatazo: Jamii ielimishwe juu ya utunzaji wa mazingira; kuzuia mimba za utotoni kwa kuwapa watoto wa kike elimu; elimu ya uzazi wa mpango itolewe kwa wanajamii hii itasaidia kupunguza ongezeko la watoto wanaozaliwa; serikali

FOR ONLINE USE ONLY

au mtu binafsi kubuni ajira mpya ili watu waajiriwe au wajiajiri; na kutoa elimu ya ujasiriamali itakayo wawezesha watu wengi kujiajiri.

## Zoezi la 4

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja sababu mbili zinazochangia watu kuongezeka kwa kasi.
2. Tofautisha ongezekokasi la watu na ongezeko la idadi ya watu.
3. Toa hoja nne, kueleza kwa ufupi jinsi unavyoweza kudhibiti ongezeko kasi la watu katika mkoa wako.

## Zoezi la 5

**Jibu maswali yafuatayo:**

**A. Chagua herufi ya jibu sahihi kisha andika herufi hiyo katika kisanduku.**

1. Ipi ni njia sahihi ya kupata idadi ya watu katika eneo fulani?
   (a) Kufanya mkutano
   (b) Kuwaandikisha watu katika vyama vya siasa [ ]
   (c) Kufanya sensa ya watu na makazi
   (d) Kusajili idadi ya watoto wanaozaliwa nchini
2. Makazi ya watu ni _______.
   (a) uwapo wa nyumba
   (b) sehemu ambapo binadamu huishi [ ]
   (c) eneo tupu
   (d) umbo au mwonekano wa mji
3. Idadi ndogo ya watu ni _______.
   (a) hali ya watu kuwa wengi hivyo kutumia rasilimali ipasavyo
   (b) hali ya watu kuwa wa kutosha katika eneo [ ]
   (c) hali ya watu kuwa wachache hivyo kushindwa kutumia rasilimali ipasavyo
   (d) hali ya watu kupungua



FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE
FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B. Jaza nafasi zilizoachwa wazi**

4. __________ ni muundo wa makazi yanayojengwa kwa kufuata barabara.
5. Sababu zinazowafanya Watanzania waongezeke ni __________ na __________.
6. Vifo vya watu vinaweza kudhibitiwa kwa __________ na __________.
7. Jiji la Dar es Salaam linakuwa kwa kasi kwa sababu ya __________.
8. Kukua kwa jiji la Dodoma kunachangiwa na __________.
9. Sensa nchini Tanzania hufanyika kila baada ya miaka __________.
10. Nchini Tanzania sensa ya watu na makazi iliyoonesha idadi ya watu kuwa imefikia milioni 45 ilifanyika mwaka __________.

**C. Andika KWELI kwa sentensi ya kweli na SI KWELI kwa sentensi isiyo ya kweli katika nafasi uliyopewa.**

11. Idadi kubwa ya Watanzania huishi mjini. __________
12. Vifo katika eneo ni kisababishi cha ongezeko la watu. __________
13. Kuzuia mimba za utotoni ni njia mojawapo ya kudhibiti ongezeko kasi la watu. __________
14. Idadi ya watu ni jumla ya watu wanaoishi katika maeneo mbalimbali. __________

**D. Jibu maswali yafuatayo**

15. Fafanua njia tatu zinazotumika kupata idadi ya watu Tanzania.
16. Elezea madhara manne yanayoweza kutokea endapo watu wataongezeka kwa kasi katika eneo unaloishi.
17. Eleza kwa ufupi jinsi idadi ndogo ya watu na makazi katika eneo inavyoathiri uzalishaji mali.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 164 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Moja

# Shughuli za kiuchumi katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Sita, ulijifunza shughuli mbalimbali za uzalishaji mali katika jamii na kueleza namna uzalishaji mali unavyochochea uhusiano mwema baina ya Tanzania na nchi nyingine. Katika sura hii, utajifunza na utahusianisha shughuli za kiuchumi zinazofanyika katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na faida zake. Maarifa na ujuzi utakaoupata katika sura hii, utakusaidia kuwa na uwezo wa kubaini na kushiriki katika shughuli za kiuchumi ngazi ya familia, taifa na kimataifa. Vilevile, utakusaidia kutumia fursa za kiuchumi zilizopo katika nchi zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki.*

## Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

Jumuiya ya Afrika Mashariki ni jumuiya ya ukanda wa kiuchumi inayoundwa na nchi sita ambazo ni: Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Sudani Kusini. Nchi hizi zinatofautiana kwa ukubwa wa eneo na idadi ya watu. Kwa mfano, nchi ya Tanzania inaongoza kwa kuwa na eneo kubwa na idadi kubwa ya watu. Nchi ya pili kwa ukubwa wa eneo ni Sudani Kusini (ingawa ni ya nne kwa idadi ya watu) ikifuatiwa na Kenya ambayo ni ya tatu kwa ukubwa wa eneo (ingawa ni ya pili kwa idadi ya watu). Nchi ya nne kwa ukubwa wa eneo ni Uganda. (ingawa ni ya tatu kwa wingi wa watu), ikifuatiwa na Burundi na nchi ya mwisho kwa ukubwa wa eneo ni Rwanda. Jedwali lifuatalo linaonesha idadi ya watu na ukubwa wa eneo la nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki:

**Jedwali:** Idadi ya watu na ukubwa wa eneo la kila nchi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki

| Na | Nchi | Eneo(Km$^2$) | Makadirio ya idadi ya Watu mwaka 2019 |
|---|---|---|---|
| 1 | Tanzania | 945 090 | Milioni 54.2 |
| 2 | Kenya | 582 646 | Milioni 47.8 |
| 3 | Uganda | 236 000 | Milioni 39.0 |
| 4 | Rwanda | 26 338 | Milioni 12.1 |
| 5 | Burundi | 27 834 | Milioni 11.7 |
| 6 | Sudani Kusini | 619 745 | Milioni 12.3 |

**Chanzo:** *East African Community (https://www.eac.int/eac-partner-states)*



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 165 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Aidha, Kielelezo kifuatacho kinaonesha mipaka ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.




**Kielelezo:** *Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Shughuli kuu za kiuchumi katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

Wananchi wa kila nchi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki hujishughulisha na shughuli mbalimbali za kiuchumi zinazowaingizia kipato. Shughuli kuu za kiuchumi katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ni pamoja na: kilimo, uchukuzi, utalii, ufugaji, uvuvi, uchimbaji madini, viwanda na biashara. Baadhi ya shughuli hizi husababisha muingiliano wa watu miongoni mwa nchi hizi. Shughuli hizi zinafanywa na serikali na taasisi zake, watu binafsi na kampuni mbalimbali. Mapato yanayopatikana kutokana na shughuli hizo yanachangia katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ufuatao ni ufafanuzi wa baadhi ya shughuli kuu za kiuchumi katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

### Kilimo

Kilimo ni shughuli ya kiuchumi inayohusisha uzalishaji wa mazao mbalimbali ya chakula na biashara. Baadhi ya mazao makuu ya biashara yanayolimwa katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kahawa, pamba, chai, chikichi, korosho, katani, miwa, tumbaku, vanila, maua na karafuu. Mazao ya chakula ni mahindi, ndizi, mihogo, karanga, mpunga, uwele, njugu, ngano, maharage, mtama, viazi mviringo, viazi vitamu na nazi. Mazao haya yanalimwa katika sehemu mbalimbali za Afrika Mashariki kutegemeana na hali ya tabianchi na aina ya udongo katika eneo linalohusika. Mazao haya hulimwa karibu kila nchi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, japo baadhi ya nchi hulima mazao hayo kwa kiwango kikubwa. Mfano, zao la pamba na kahawa hulimwa zaidi katika nchi za Tanzania, Burundi, Kenya na Uganda. Mazao ya chakula kama vile mahindi, maharage, ngano, mpunga na mtama yanalimwa kwa wingi katika nchi za Rwanda, Burundi, Tanzania, Sudani Kusini na Kenya. Mazao ya chakula yakilimwa kwa wingi hutumika pia kama mazao ya biashara.

Shughuli za kilimo katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa sehemu kubwa hufanywa na wakulima wadogo. Wakulima hawa hutumia pembejeo duni kama vile jembe la mkono. Pia, wanalima mashamba madogo kwa ajili ya chakula na kwa kiasi kidogo kuyauza ili kuweza kukidhi mahitaji mbalimbali. Wakulima wadogo hupata mazao kidogo kwa sababu ya kutumia zana duni za kilimo, eneo dogo na hutegemea mvua.

Wakulima wakubwa hulima mazao kwa ajili ya biashara. Hutumia pembejeo za kisasa kama vile mashine katika kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia na hata kuvuna mazao. Wakulima wakubwa hulima mashamba makubwa na hutumia teknolojia ya kilimo cha umwagiliaji. Wakulima hawa husafirisha

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

na kuuza mazao yao ndani na nje ya nchi ili kujiongezea kipato binafsi na taifa kwa ujumla. Hivyo kuna uhusiano mkubwa wa shughuli za kilimo zinavyofanyika katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kilimo cha mazao ya biashara na chakula kina faida nyingi. Baadhi ya faida hizo ni familia za wakulima wadogo kuwa na uhakika wa kupata chakula cha kutosha na kuuza ziada ya mazao ya chakula ili kujiongezea kipato. Wakulima wakubwa huuza mazao ya kilimo na kupata pesa kwa ajili ya kujikimu na kufanya shughuli za kimaendeleo. Kilimo huingizia nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki fedha za kigeni ambazo huinua uchumi wa nchi hizo. Aidha, kilimo kimeongeza ajira kwa wananchi. Ajira hizi zinabainishwa katika kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia, kuvuna, kupakia na kusafirisha mazao. Vilevile, kilimo kimechangia kuanzishwa kwa viwanda vya kuchakata, kusindika na kutengeneza bidhaa mbalimbali zitokanazo na mazao ya kilimo. Mfano, zao la karafuu hutumika kutengenezea dawa, mafuta, na kiungo katika chakula. Viwanda hivi vimeajiri watu wengi katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Viwanda na biashara**

Shughuli za viwanda zinahusisha uchakataji wa malighafi ili kuzalisha bidhaa za aina mbalimbali ambazo zinaweza kutumiwa na jamii. Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zimeweza kuanzisha viwanda mbalimbali na kuviendeleza. Viwanda hivyo vinatengeneza bidhaa kama vile nguo, viatu, vifaa vya ujenzi, pembejeo za kilimo, vinywaji, dawa za mifugo na binadamu, samani na vifaa vya kielimu. Malighafi zinazotumika katika uzalishaji wa bidhaa viwandani hutokana na kilimo, ufugaji, na rasilimali za asili zilizopo.

Maendeleo ya viwanda yameongeza kasi ya ukuaji wa sekta ya biashara katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika nchi hizi wapo wafanyabiashara wadogo, wa kati, na wakubwa. Watu binafsi, kampuni, serikali na taasisi zake wamejikita katika kufanya aina mbalimbali za biashara. Biashara hizi zinalenga kukuza uchumi wa wananchi na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ujumla. Bidhaa zinazouzwa ni zile za viwandani, mazao ya chakula na biashara. Huduma zinazotolewa ni afya, mawasiliano, umeme na elimu. Nchi za Afrika Mashariki zimeweka mazingira mazuri ya kufanya biashara baina ya nchi wanachama. Mazingira haya ni pamoja na kupunguza kodi mbalimbali za bidhaa na huduma wanazotoa. Pia, nchi wanachama zimeondoa vikwazo vya kibiashara baina ya nchi na nchi na hivyo kuchochea mzunguko wa bidhaa na muingiliano wa kibiashara.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zinazalisha baadhi ya bidhaa zinazofanana. Baadhi ya bidhaa zinazotengenezwa nchini Tanzania, Kenya, Uganda na Burundi ni pamoja na nguo, viatu, vinywaji, saruji, na bidhaa za vyakula. Pia, nchi hizi hutengeneza vipodozi, rangi, dawa za binadamu, dawa za mifugo na mimea, vifaa tiba, kemikali mfano kastikisoda na tindikali, vifaa vya umeme, bidhaa za plastiki na bidhaa zitokanazo na mazao ya mifugo. Vilevile, nchi ya Rwanda pamoja na kuzalisha bidhaa nyingine pia huzalisha simu za viganjani. Nchi ya Sudani Kusini huzalisha mafuta ghafi kwa wingi. Maendeleo ya viwanda vinavyozalisha bidhaa mbalimbali katika nchi hizi yamechangia kukua kwa sekta ya biashara. Hii imeongeza kiwango cha watu kuajiriwa na kujiajiri. Shughuli za viwanda na biashara zimechangia pia kukua kwa pato la mtu binafsi na taifa kwa ujumla. Hivyo, kukua kwa viwanda kumeongeza soko la malighafi na bidhaa mbalimbali katika nchi za Afrika Mashariki.

**Kazi ya kufanya namba 1**

Tumia vyanzo mbalimbali vya taarifa kama vile vitabu na mtandao, kupata taarifa zifuatazo:

(a) Majina ya viwanda viwili kwa kila nchi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambavyo vinazalisha bidhaa zinazofanana.

(b) (i) Orodhesha aina za malighafi zinazotumika kutengenezea bidhaa hizo.

(ii) Eleza faida zinazotokana na shughuli za viwanda hivyo.

Wasilisha taarifa yako darasani.

### Uchimbaji wa madini

Nchi zilizomo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki zina madini ya aina nyingi. Mfano wa madini yanayopatikana ni: Tanzanaiti, almasi, dhahabu, bati, makaa ya mawe, shaba, chuma, ulanga, chokaa, mafuta, gesi na chumvi. Madini haya yamekuwa yakichimbwa katika maeneo mbalimbali ya nchi hizi. Katika nchi hizi uchimbaji wa madini unatumia vifaa duni kwa wachimbaji wadogo na mashine kubwa na mitambo kwa wachimbaji wakubwa au kampuni. Wachimbaji wakubwa wa madini kwa kiasi kikubwa ni wawekezaji kutoka nje wenye mitaji mikubwa.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kila nchi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki hulinda madini yake ili iweze kunufaika nayo. Mfano, Tanzania imeimarisha ulinzi katika maeneo yanakopatikana madini ya Tanzanaiti kwa kujenga ukuta kuzunguka eneo hilo. Pia, imeanzisha masoko ya ununuaji na uuzaji wa madini kwa kila mkoa ili kuhakikisha kuwa madini hayo hayatoroshwi.

Baadhi ya madini yanayopatikana Tanzania ni dhahabu, Tanzanaiti, bati, almasi, makaa ya mawe, shaba, chuma, ulanga, chokaa, mafuta, gesi na chumvi. Kenya ina madini kama vile dhahabu, magadi, makaa ya mawe na jasi. Madini yanayopatikana nchini Uganda ni pamoja na dhahabu, shaba, chuma, chumvi, mika, mafuta, na chokaa. Nchini Sudani Kusini yanapatikana kwa wingi madini ya chuma, shaba, mafuta, dhahabu, zinki na fedha. Vilevile katika nchi ya Burundi madini ya dhahabu, uraniamu, shaba na chokaa hupatikana kwa wingi. Pia, madini ya dhahabu yanapatikana kwa wingi nchini Rwanda. Hivyo kuna uhusiano mkubwa wa aina za madini yanayochimbwa katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Uchimbaji wa madini huchangia kuinua pato la taifa na ajira kwa wanajamii. Aidha, baadhi ya madini hutumika kama mapambo na malighafi za viwanda. Vilevile, madini hutumika katika shughuli za ujenzi, kutengenezea vifaa vya nyumbani na chanzo cha nishati mfano makaa ya mawe.

### Zoezi la 1

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Orodhesha aina mbili za madini yanayopatikana karibu nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki.
2. Madini gani ambayo hupatikana Tanzania tu?
3. Tofautisha kilimo cha wakulima wadogo na kilimo cha wakulima wakubwa.
4. Bainisha mazao matano ambayo hutumika kama malighafi za kutengeneza bidhaa, kisha taja bidhaa mbili zitokanazo na kila zao.
5. Eleza kwa kifupi faida mbili za kutumia pembejeo za kisasa katika kilimo.

### Ufugaji

Ufugaji ni shughuli nyingine ya kiuchumi ambayo hufanyika katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ufugaji ni shughuli inayohusisha utunzaji wa mifugo kwa lengo la kujipatia chakula au kipato kwa kuuza nyama, ngozi, maziwa, mayai na mbolea. Wanyama mbalimbali hufugwa katika nchi

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 170 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

hizi, pamoja na ufugaji wa samaki na nyuki. Wanyama wanaofugwa kwa wingi nchini Tanzania ni ng'ombe, nguruwe, mbuzi, kondoo, kuku na bata. Samaki na nyuki pia hufugwa Tanzania. Wanyama wanaofugwa kwa wingi katika nchi ya Burundi ni mbuzi, ng'ombe, kuku na bata. Nchini Uganda, wanyama wanaofugwa kwa wingi ni ng'ombe, kuku, mbuzi, bata, farasi, punda na sungura. Samaki na nyuki pia hufugwa nchini humo. Kenya hufuga ngo'mbe, mbuzi, ngamia, kuku, punda na bata kwa wingi. Ufugaji wa samaki na nyuki pia hufanyika. Nchini Rwanda, ng'ombe, mbuzi, kuku na nguruwe hufugwa zaidi. Sudani Kusini hufuga ng'ombe, mbuzi, na kondoo. Hivyo kuna uhusiano mkubwa wa aina ya mifugo inayofugwa katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Ufugaji una faida kubwa katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Faida hizo ni pamoja na upatikanaji wa nyama, maziwa, mayai, ngozi na mazao mengine ya mifugo. Vilevile, upatikanaji wa fedha kwa ngazi ya familia na kuchangia katika pato la taifa linalohusika. Ufugaji katika nchi hizi umechangia ongezeko la kipato na ajira.

**Uvuvi**

Uvuvi ni shughuli ya kiuchumi inayohusisha uvuaji wa samaki kutoka katika bahari, maziwa, mabwawa na mito mikubwa kwa kutumia vifaa maalumu kama nyavu na ndoano. Lengo la uvuvi ni kujipatia chakula au kipato. Katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki shughuli ya uvuvi hufanyika kwenye maeneo kama vile bahari ya Hindi, ziwa Victoria, ziwa Tanganyika, ziwa Nyasa, ziwa Turkana, ziwa Kivu, ziwa Albert na kwenye mabwawa. Baadhi ya vyanzo hivi vya uvuvi vimeunganisha nchi zaidi ya moja. Mfano, ziwa Victoria linapatikana katika nchi za Tanzania, Kenya na Uganda. Pia, ziwa Tanganyika linapatikana katika nchi za Tanzania na Burundi.

Faida za uvuvi katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ni pamoja na upatikanaji wa samaki. Samaki hutumika kama kitoweo ambacho hutupatia protini. Pia, samaki hutupatia mafuta, gundi, ngozi, mapambo na mbolea. Samaki hutupatia malighafi za kutengenezea vyombo vya plastiki na vishikizo vya nguo. Mifupa ya samaki husagwa na kutumika kama chakula cha mifugo. Mafuta ya samaki hutumika kama dawa za binadamu. Uvuvi huimarisha uchumi kwa kuzipatia nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki fedha za kigeni. Mfano, katika nchi ya Tanzania minofu ya samaki aina ya sangara husafirishwa na kuuzwa nje ya nchi hasa katika Bara la Ulaya. Vilevile, shughuli za uvuvi zinatoa ajira kwa wananchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 171 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 2**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Orodhesha maeneo ambayo shughuli za uvuvi hufanyika katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.
2. Bainisha mazao matano ya samaki.
3. Eleza kwa kifupi faida tano za ufugaji katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Utalii**

Utalii ni hali ya mtu au kikundi cha watu kwenda kutembelea maeneo yenye vivutio mbalimbali kwa lengo la kujifunza au kuburudika. Kuna aina mbili za utalii ambazo ni; utalii wa ndani na utalii wa wageni kutoka nje ya nchi. Utalii wa ndani ni kitendo cha watu wa nchi moja kusafiri kutoka katika maeneo yao kwenda maeneo mengine ndani ya nchi yao kwa lengo la kujifunza, kufanya biashara au kuburudika. Utalii wa nje ni kitendo cha watu wa nchi moja kusafiri kutoka maeneo yao kwenda mahali pengine nje ya nchi yao kwa lengo la kujifunza, kufanya biashara au kuburudika.

Shughuli za utalii zinazofanyika katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ni utalii wa michezo, utalii wa makongamano, utalii wa kielimu na utalii wa kibiashara. Utalii pia hufanyika kwa njia ya watu kwenda kupumzika katika maeneo mbalimbali yenye vivutio kama vile fukwe za bahari, mbuga na hifadhi za wanyama. Utalii pia hufanyika kwenye maeneo ya jangwani, maporomoko ya maji na mandhari mbalimbali zinazovutia. Vilevile, utalii hufanyika katika maeneo yaliyohifadhi matukio na vifaa vilivyotumiwa kipindi cha zamani kama vile makumbusho ya taifa na maeneo ya kihistoria. Pia, utalii hufanyika katika maeneo maalumu palipohifadhiwa rasilimali za asili na milima yenye theluji mfano mlima Kilimanjaro.

Karibu nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki zina maeneo yaliyohifadhiwa yenye vivutio vya utalii. Mfano, nchini Tanzania zipo mbuga za wanyama ambazo ni Serengeti, Selous, Ruaha, Mikumi, Kilimanjaro, Katavi, Mkomazi, Tarangire, Udzungwa, Saadani, Mahale, Burigi-Chato, na Gombe. Vilevile, Ngorongoro ni eneo la hifadhi ambalo watalii wa ndani na nje hupenda kutembelea. Vivutio vingine vya utalii nchini Tanzania ni mapori ya akiba mfano Moyowosi na Ugalla. Utalii wa kuangalia mandhari hupendwa pia na watalii wengi. Watalii hutembelea maeneo mbalimbali kama vile kwenye milima, mfano Mlima Kilimanjaro na fukwe za Bahari ya Hindi. Vilevile,

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

yapo maeneo yalipohifadhiwa mambo ya kale kama vile makumbusho ya taifa na nyumba ya utamaduni vilivyopo Dar es Saalam. Pia, yapo maeneo ya kihistoria kama jumba la makumbusho na ngome kongwe yaliyopo Mji Mkongwe Zanzibar, Isimila, Bonde la Oldupai, Kondoa Irangi, na Bagamoyo.

Nchini Kenya kuna vivutio mbalimbali vya utalii kama vile mbuga za wanyama za Tsavo, Sibiloi, Maasai Mara na Ruma. Vilevile, yapo maeneo ya kihistoria, fukwe za bahari ya Hindi maeneo ya Mombasa na Lamu. Utalii wa uvuvi na kupanda milima pia hupendwa sana na watalii nchini Kenya. Katika nchi ya Uganda pia, kuna vivutio mbalimbali vya utalii kama vile mbuga za wanyama za Queen Elizabeth, Mlima Elgon, Semuliki, Ruwenzori na Bonde la Kidepo. Watalii pia hupenda kutembelea maporomoko ya mto Nile yalipo Jinja na maporomoko ya Murchison yaliyopo Masindi.

Nchi ya Rwanda ina utajiri mkubwa wa mimea na wanyama ambao hupatikana katika mbuga ya wanyama ya Akagera. Zipo pia mbuga nyingine kama Nyungwe na Mukura-Gishwati. Wanyama aina ya sokwe pia hupatikana katika Mlima Virunga. Katika nchi za Burundi na Sudani Kusini, shughuli za utalii hazijakua kwa kiwango cha juu kutokana na nchi hizo kukumbwa na changamoto za kisiasa. Pamoja na changamoto hizo, nchi ya Sudani Kusini ina mbuga za wanyama kama vile Nimule, Lantoto, Bandingilo, Shambe na maeneo ya hifadhi kama Fanikang na Juba. Pia, katika nchi ya Burundi upo utalii wa kuangalia ngoma za asili na mbuga za wanyama kama vile Rusizi, Kibira na Ruvubu.

Shughuli za utalii katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zina faida nyingi. Baadhi ya faida hizo ni: kutoa ajira kwa wananchi, kuongeza pato la taifa, kupata fedha za kigeni, kuboreshwa kwa miundombinu, kuimarika kwa shughuli za biashara, uchukuzi na mawasiliano. Pia, shughuli za utalii huhamasisha maendeleo ya sekta nyingine kama vile kilimo na ufugaji katika maeneo yanayopakana na sehemu za vivutio vya utalii. Vilevile, huchangia maendeleo ya sanaa na utamaduni wa jamii za nchi hizi.

FOR ONLINE USE ONLY

### Zoezi la 3

**Jibu swali lifuatalo:**

Orodhesha maeneo matatu ambayo watu wanaweza kutembelea nchini Tanzania ili kujifunza mambo yafuatayo;

(a) Historia ya kale

(b) Mwonekano wa sura ya nchi

(c) Kuhusu wanyama pori

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 4**

**A. Jibu maswali yafuatayo:**

1. Orodhesha bidhaa nne zinazotengenezwa katika viwanda vya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.
2. Eleza faida mbili kwa kila zao lifuatalo:
   (a) pamba
   (b) mahindi
   (c) karafuu
3. Bainisha makundi matatu ya vivutio vya utalii vinavyopatikana katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.
4. Eleza maana ya istilahi zifuatazo:
   (a) utalii
   (b) ufugaji
   (c) uvuvi

**B. Andika KWELI kwa sentensi ya kweli na SI KWELI kwa sentensi isiyo ya kweli katika nafasi uliyopewa.**

5. Mazao ya chakula yanalimwa kwa ajili ya chakula tu. _________
6. Kahawa, pamba, na karafuu ni baadhi ya mazao ya biashara. _________
7. Uchimbaji madini hunufaisha familia za wachimbaji tu Afrika Mashariki. _________
8. Kuongezeka kwa pato la taifa ni moja ya faida ya shughuli za kiuchumi. _________

FOR ONLINE USE ONLY

## Msamiati

Pembejeo — vitu muhimu kwa ajili ya kilimo ikiwa ni pamoja na dawa, mbolea, mbegu, na zana

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Mbili

# Ujasiriamali

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Sita ulijifunza kuhusu makundi ya ujasiriamali, faida za kuwa mjasiriamali biashara, na mambo muhimu ya kuzingatia katika ujasiriamali biashara. Vilevile, ulichambua changamoto zinazoikabili jamii ya Kitanzania katika kutumia fursa zilizopo na namna ya kukabiliana na changamoto hizo. Katika sura hii, utajifunza kuhusu shughuli za ujasiriamali na namna zinavyochangia katika ukuaji wa uchumi, utachambua pia fursa zinazotokana na njia za uchukuzi katika mazingira yanayokuzunguka. Pia, utatathmini athari zinazoweza kusababishwa na njia zisizo halali katika ujasiriamali. Maarifa na ujuzi utakaopata katika sura hii, utakusaidia kutambua fursa zilizopo katika njia za usafiri na kujipatia kipato. Pia, utakusaidia kufuata njia halali katika ujasiriamali biashara ili kuepuka kupata hasara.*



**Fikiri**

1. Kuhusu shughuli za ujasiriamali.
2. Kuhusu shughuli za ujasiriamali zinavyochangia ukuaji wa uzalishaji mali.

## Shughuli za ujasiriamali

Ujasiriamali ni ubunifu unaofanywa na mtu au watu katika kuzitambua fursa zilizopo na kuzitumia kwa kuunda, kutangaza na kuendesha biashara ambazo mara nyingi huwa ni biashara ndogo ili kujipatia kipato. Ubunifu huu unahusisha ujuzi na maarifa ya mtu katika kutatua changamoto zinazoikabili jamii. Katika ujasiriamali shughuli mbalimbali hufanyika kama vile; kilimo, ufugaji, usindikaji wa vyakula, urembo, ushonaji, na biashara. Shughuli za ujasiriamali zinaweza kufanywa na mtu binafsi, kikundi cha watu, kampuni au kwa ubia. Ujasiriamali humsaidia mjasiriamali kupata fedha na kulipa kodi, hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi. Zifuatazo ni baadhi ya shughuli za ujasiriamali na jinsi zinavyochangia ukuaji wa uchumi:



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 175 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kilimo**

Kilimo ni shughuli ya kiuchumi inayohusisha uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Wajasiriamali huchagua mazao yenye faida kubwa, yanayokomaa haraka na yenye soko zuri. Kilimo kinaweza kuwa cha gharama ndogo sana na kupata mavuno kwa muda mfupi. Kwa mfano, kilimo cha mazao ya bustani za mbogamboga kama vile mchicha, spinachi, nyanya, vitunguu, na pilipili. Muda hadi kuvuna ni kati ya wiki tatu hadi miezi mitatu.

**Ufugaji**

Ufugaji ni shughuli nyingine ya uzalishaji mali ambayo mjasiriamali anaweza kuitumia kujiongezea kipato. Mjasiriamali anaweza kufuga mifugo mbalimbali kama ng'ombe, mbuzi, samaki, nyuki, kuku na sungura. Mjasiriamali hutunza mifugo kwa kutumia ubunifu, huipa chakula akizingatia lishe bora au kanuni zote za ufugaji bora kwa viwango vilivyothibitishwa. Juhudi hizi hufanywa na wajasiriamali ili kuweza kupata fursa ya masoko kulingana na ubora wa mifugo hiyo na mazao yake. Ufugaji wenye ubunifu humpatia mjasiriamali mazao yenye ubora kama vile maziwa, nyama, ngozi na asali ambazo anaweza kuziongezea thamani zaidi na kuziuza. Mazao haya yanapouzwa humpatia mfugaji kipato ambacho huchangia kukua kwa uchumi wake binafsi na wa taifa. Kwa kufanya hivi, mjasiriamali anakuwa ameweza kutatua changamoto iliyokuwa ikiikabili jamii yake.

**Ushonaji**

Ushonaji ni stadi inayotumika ama kuunganisha sehemu za kitambaa au kitambaa na kitu kingine, kutengeneza mishono mbalimbali kwa kutumia uzi na sindano. Huu ni ufundi unaotumika tangu zamani kutengeneza vitu mbalimbali kwa kutumia mashine au mikono. Ushonaji wa vitu kama vile, nguo, mashuka, mapazia, viatu na mifuko ya kubebea bidhaa ni baadhi ya shughuli za ujasiriamali. Ushonaji unasaidia kukuza ubunifu. Ubunifu huu humwezesha mjasiriamali kuzalisha bidhaa zenye ubora. Uuzwaji wa bidhaa hizi humwezesha mjasiriamali kujipatia kipato hivyo kukidhi mahitaji yake ya kila siku. Ubunifu katika ushonaji wa bidhaa mbalimbali, unawawezesha wajasiriamali kutengeneza bidhaa bora zinazoweza kushindanishwa kwenye masoko ya bidhaa ndani na nje ya nchi. Mfano, maonesho ya biashara ya kimataifa yanayofanyika kila mwaka katika Viwanja vya Sabasaba, jijini Dar es Salaam, yanahamasisha wajasiriamali wanaojihusisha na ushonaji

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 176 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kubuni bidhaa mbalimbali. Bidhaa hizi huweza kukidhi mahitaji ya soko ambalo hubadilika mara kwa mara kutegemeana na mahitaji ya jamii.

**Biashara**

Biashara ni shughuli inayohusisha uuzaji na ununuaji wa bidhaa au huduma. Wajasiriamali hufanya ubunifu kwa kusambaza au kuongeza thamani ya bidhaa na huduma zinazohitajika katika jamii. Thamani ya bidhaa au huduma inaweza kuongezeka kupitia ubora wake katika uandaaji wake, vifungashio au mazingira bidhaa inapouzwa. Pia, lugha inayovutia wateja, uaminifu, mwonekano wa mtoa huduma na upatikanaji wa bidhaa au huduma inayohusika inaweza kuongeza uuzaji. Lengo kuu la biashara ni kupata faida. Biashara inaweza kufanywa na mtu binafsi, kikundi cha watu, kampuni, au kwa ubia kati ya mtu mmoja na mwingine, jamii moja na nyingine au nchi moja na nyingine. Mjasiriamali hufanya biashara hizi kwa kuzingatia mambo yote muhimu na hujizatiti katika kuongeza thamani na ubora wa bidhaa au huduma zake. Hii humsaidia kupata wateja wengi na faida kubwa zaidi.

**Kazi ya kufanya namba 1**

1. Chunguza fursa moja ya ujasiriamali ambayo inapatikana katika mazingira unayoishi.
2. Eleza jinsi fursa hiyo inavyoweza kuchangia maendeleo katika jamii yako.

**Zoezi la 1**

**Chunguza picha zifuatazo kisha, jibu maswali yanayofuata:**



1



2

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



3



4

1. Eleza shughuli zinazofanyika katika picha namba 2 na 3.
2. Je, shughuli zinazofanyika katika picha hizo, zinasaidiaje maendeleo ya mtu binafsi na ya uchumi wa nchi?
3. Taja bidhaa tatu zitokanazo na shughuli inayofanyika katika picha namba 2.
4. Elezea umuhimu wa shughuli inayoonekana katika picha namba 3 katika kujikwamua kiuchumi kwa wajasiriamali.
5. Picha namba 4 inaonesha shughuli gani ya ujasiriamali? Eleza shughuli hiyo inavyoweza kuleta maendeleo ya uchumi na kupunguza umaskini katika jamii yako.
6. Taja faida tatu zitokanazo na shughuli kwenye picha namba 1.

## Fursa za ujasiriamali zinazotokana na njia za uchukuzi



**Fikiri**

1. Aina za njia za uchukuzi.
2. Fursa za ujasiriamali zinazopatikana kutokana na uwapo wa njia za uchukuzi.

Njia za uchukuzi zimegawanyika katika makundi matatu nazo ni; njia ya nchi kavu, njia ya majini na njia ya angani. Njia za nchi kavu zinajumuisha miundombinu kama barabara, reli na mabomba. Vyombo vya uchukuzi katika nchi kavu ni pamoja na magari, pikipiki, baiskeli, wanyamakazi na

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 178 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

binadamu. Njia za majini hujumuisha bahari, maziwa, mabwawa, mito na mifereji. Vyombo vya uchukuzi majini ni pamoja na meli, boti, mashua, ngalawa, merikebu, jahazi, manowari, nyambizi na mitumbwi. Njia ya anga hutumia ndege kama helikopta na eropleni. Njia hizi zote huweza kutumiwa na wajasiriamali katika kusafirisha abiria na mizigo. Pamoja na kusafirisha mizigo na abiria mjasiriamali anaweza pia kutumia fursa za njia hizi za uchukuzi kufanya biashara mbalimbali. Biashara hizo ni kama vile kuuza vyakula, matunda,vinywaji, mavazi na vifungashio. Pia wajasiriamali hutoa huduma za simu na mawasiliano, huduma za fedha kwa njia ya mitandao, hoteli, nyumba za kulala wageni, na huduma za maliwato. Mjasiriamali anapotoa huduma hizo kwake ni fursa inayompatia kipato. Ufuatao ni ufafanuzi wa baadhi ya fursa zinazotokana na njia za uchukuzi:

**Usafirishaji wa abiria na mizigo:** Mjasiriamali anaweza kubuni na kuboresha namna ya kusafirisha abiria na mizigo kwa njia mbalimbali kama vile; pikipiki, teksi, mabasi, mitumbwi, na boti. Ubunifu huu unaweza kuwa kwa kuboresha chombo anachotumia ili kuvutia wateja, kuongeza idadi ya vyombo vya usafiri au muda wa kutoa huduma na umbali wa kufikisha huduma au bidhaa zake. Usafirishaji unaweza kufanyika ndani ya nchi kutoka mkoa mmoja hadi mwingine, au eneo moja hadi jingine au nje ya nchi. Fursa hii huweza kumuingizia mjasiriamali fedha nyingi na hivyo kuboresha maisha yake na uchumi wa nchi kwa ujumla.

**Hoteli na migahawa:** Hii huweza kufanyika hasa kwenye vituo vya kushusha na kupandisha abiria au kupakia na kupakua mizigo. Wajasiriamali wengi hujishughulisha na shughuli za hoteli na migahawa kando au karibu na vituo vya njia za uchukuzi. Migahawa hii na hoteli hutoa huduma za vyakula na vinywaji. Mara nyingi katika vituo vya usafiri huwa na muingiliano wa watu wengi, hivyo wajasiriamali huweza kujipatia wateja wengi wanaoingia na kutoka katika maeneo hayo. Kwa njia hii, wajasiriamali huweza kujipatia kipato na kuboresha maisha yao. Aidha, ili kuweza kuifanikisha fursa hii mjasiriamali lazima aweke ubunifu, uaminifu, nidhamu, kauli njema na unadhifu katika kuendesha hoteli au mgahawa wake.

**Biashara na huduma ndogondogo:** Njia za uchukuzi zinatoa fursa kwa wajasiriamali kufanya biashara ndogondogo kama vile kuuza vyakula, vinywaji, mavazi, na vifungashio. Wajasiriamali pia hutoa huduma za simu na mawasiliano, huduma za kifedha kwa njia ya mitandao, na huduma za maliwato. Baadhi ya abiria wanaposafiri huwa na mahitaji madogomadogo kama vile vinywaji na viburudisho mbalimbali. Wajasiriamali huwahudumia

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 179 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

na kuwatoza fedha. Wajasiriamali wanapofanya biashara na kutoa huduma hizo hujipatia kipato.

**Zoezi la 2**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja njia tatu za uchukuzi zinazotumiwa na wajasiriamali kusafirisha bidhaa zao.
2. Taja faida anazopata mjasiriamali kupitia njia za uchukuzi.
3. Eleza kwa kifupi fursa tano zitokanazo na njia za uchukuzi.

## Njia zisizo halali katika ujasiriamali



**Fikiri**

1. Maana ya njia zisizo halali katika ujasiriamali.
2. Njia nne zisizo halali katika ujasiriamali.
3. Matokeo ya kufanya ujasiriamali usiofuata njia halali.

Njia zisizo halali katika ujasiriamali ni njia zisizo faa zinazotumiwa na baadhi ya wajasiriamali ili kupata faida kubwa. Pamoja na kwamba ujasiriamali ni uthubutu wa kufanya biashara, uthubutu huo hauruhusu mjasiriamali kufanya biashara kwa kutumia njia ambazo si halali. Ujasiriamali unaotumia njia zisizo halali humsababishia mjasiriamali matatizo. Njia zisizo halali humpatia mjasiriamali fedha haramu ambazo ni hatari kwa maendeleo ya biashara yake. Njia hizo zina athari kubwa kwa mjasiriamali, kwa wateja wake na kwa taifa. Baadhi ya njia zisizo halali katika ujasiriamali ni kama zifuatazo:

(a) *Kukwepa kodi:* Hii ni njia isiyo halali ambapo wajasiriamali huficha maeneo ya uzalishaji wa bidhaa zao na kutoa taarifa za uongo kuhusu aina na ukubwa wa biashara zao. Wajasiriamali wengine hushirikiana na baadhi ya wafanyakazi wenye dhamana ya kukusanya mapato kwa kutoa rushwa ili kukwepa kulipa kodi. Ukwepaji wa kodi

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

unapingwa vikali na nchi zote duniani kwa sababu unalikosesha taifa mapato hivyo kuzorotesha maendeleo ya nchi. Nchi inapokosa mapato yanayotokana na wajasiriamali husababisha kushindwa kutoa huduma muhimu za kijamii kama vile miundombinu na kuleta athari kubwa kijamii, kisiasa na kiuchumi. Nchi nyingi zimeweka sheria kali za kuwaadhibu wajasiriamali wanaokwepa kulipa kodi. Mnunuzi wa bidhaa au huduma yoyote anashauriwa kudai risiti ya manunuzi au malipo yoyote ili kusaidia ukusanyaji wa kodi ya serikali.

*(b)* *Kuuza bidhaa zilizoisha muda wa matumizi:* Baadhi ya wajasiriamali wasio waaminifu, huuza bidhaa ambazo zimekwisha muda wake wa matumizi. Hii ni hatari kwa mlaji kwani huweza kuleta madhara ya kiafya na hata kuweza kusababisha vifo kwa watumiaji. Kwa mfano, mgonjwa anayetumia dawa zilizokwisha muda wake anaweza kupata madhara mwilini au kutokupona ugonjwa unaomsumbua. Pia, dawa zilizokwisha muda wake zinaweza kuwa sumu kwa mlaji. Hivyo, ni muhimu mjasiriamali ahakikishe anauza bidhaa ambazo ziko ndani ya muda wa matumizi. Mtumiaji pia anashauriwa kuchunguza tarehe ya mwisho ya matumizi ya bidhaa yoyote kabla ya kuinunua.

(c) *Kuendesha biashara bila vibali:* Ili biashara iwe halali mjasiriamali anapaswa kuwa na vibali. Vibali hivyo ni kama vile namba ya utambulisho wa mlipa kodi, taarifa ya makadirio ya kodi, leseni ya biashara na vitambulisho vya wajasiriamali wadogo. Vibali vya biashara vinatolewa na serikali kwa mjasiriamali yeyote anapotaka kufanya biashara hapa nchini. Ili mjasiriamali apate vibali vya biashara, anatakiwa kuwa na kitambulisho cha taifa. Baadhi ya wajasiriamali hufanya biashara bila kuwa na vibali kutoka kwenye mamlaka husika. Hali hii husababisha serikali kukosa mapato na hivyo kuzorotesha uchumi wa nchi.

*(d)* *Kufanya udanganyifu kwenye vipimo:* Baadhi ya wajasiriamali hufanya udanganyifu katika vipimo. Mfano, mjasiriamali anaweza kufungasha sukari kwenye kifungashio kinachoonesha uzito wa kilo moja, lakini kwa uhalisia ikipimwa inakuwa haijatimia uzito wa kilo moja. Hali hii inamuathiri mtumiaji kwa kupata bidhaa isiyolingana na thamani ya fedha aliyoitoa huku mjasiriamali akijipatia faida isiyo halali. Ni wajibu wa mjasiriamali kuhakikisha anapeleka kipimo kwa wakala wa vipimo

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 181 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

nchini kwa ajili ya kukaguliwa angalau mara moja kwa mwaka. Pia, mjasiriamali anapaswa kutumia vifungashio vya ujazo halali, mfano kutoweka lumbesa kwenye magunia.

(e) *Kuuza bidhaa zisizo na ubora:* Baadhi ya wajasiriamali huuza bidhaa zisizo na ubora hivyo huleta athari kwa mtumiaji. Mjasiriamali anapaswa kupeleka bidhaa yake shirika la viwango Tanzania (TBS) ili ithibitishwe ubora wake. Kwa kufanya hivyo atapewa leseni ya kutumia alama ya ubora ya TBS. Mjasiriamali anayenunua bidhaa na kuuza kwa wateja wake anapaswa kuhakikisha bidhaa hizo zina ubora uliothibitishwa na TBS.

*(f)* *Kuuza bidhaa haramu:* Katika kufanya ujasiriamali si bidhaa zote ni halali. Baadhi ya wajasiriamali huuza bidhaa haramu kwa lengo la kujipatia kipato. Kwa mfano zipo bidhaa ambazo zimepigwa marufuku nchini kama vile vipodozi vyenye viambato vyenye sumu. Wapo wajasiriamali wasio waadilifu ambao huuza bidhaa hizo na kuleta madhara makubwa ya kiafya kwa watumiaji. Wajasiriamali wanashauriwa kuepuka kujiingiza kwenye biashara haramu.

**Zoezi la 3**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza maana ya vibali vya biashara.
2. Orodhesha njia tano zisizohalali katika ujasiriamali zinazotumiwa na baadhi ya wajasiriamali.
3. Elezea kwa ufupi njia tatu zisizohalali katika ujasiriamali zinazotumiwa na baadhi ya wajasiriamali.

**Athari za njia zisizohalali katika ujasiriamali**

Zipo athari nyingi za kiuchumi, kiafya na kijamii zinazotokana na njia zisizo halali katika ujasiriamali. Athari hizo ni kama ifuatavyo:

(a) *Serikali kukosa mapato*: Sehemu kubwa ya pato la taifa inatokana na kodi. Ukwepaji wa kodi kwa baadhi ya wajasiriamali unakosesha taifa mapato. Hali hii hukwamisha shughuli za maendeleo zinazofanywa na serikali kama vile ujenzi wa miundombinu na kuboresha huduma za kijamii. Wajasiriamali wanapaswa kuwa waadilifu ili kuliletea taifa maendeleo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) *Madhara kwa watumiaji*: Madhara ya kiafya yamekuwa yakiwapata wateja ambao hununua bidhaa zilizokwisha muda wa matumizi kama vile dawa na chakula. Bidhaa hizi huuzwa na wajasiriamali ambao siyo waadilifu na kununuliwa na wateja ambao hawawezi kutambua kwa haraka kasoro za bidhaa hizo. Pia, pamekuwepo na matumizi yasiyokuwa na viwango sahihi kutumiwa na watumiaji. Bidhaa hizo ni kama vile vifaa vya ujenzi, vipodozi, na dawa. Bidhaa hizi zimekuwa na hatari kubwa kwa watumiaji. Kwa mfano, vifaa vya ujenzi visivyokuwa na viwango bora vimesababisha ujenzi wa nyumba zisizokuwa imara na matokeo yake ni kubomoka kwa majengo katika muda mfupi.

(c) *Kufungiwa kwa shughuli za mjasiriamali:* Shughuli ya ujasiriamali huweza kufungwa pale ambapo ukaguzi utafanyika na vyombo husika na kugundua biashara inayofanyika inatumia njia zisizo halali. Pia, shughuli ya ujasiriamali inaweza kufungiwa mara tu inapobainika kuwa imesababisha madhara kwa jamii. Vilevile, mjasiriamali anaweza kuchukuliwa hatua za kisheria na kupewa adhabu kali. Biashara inayotumia njia zisizo halali ni changamoto kwa serikali na inaleta hofu kubwa katika uchumi wa nchi na mazingira. Nchi nyingi ikiwamo Tanzania zimeweka sheria kali zinazolenga kudhibiti wajasiriamali wanaokiuka maadili ya biashara zao kwa kujihusisha na biashara zinazotumia njia zisizo halali. Kufungiwa kwa biashara pia kunaharibu jina la mjasiriamali na kuleta taswira mbaya kwa jamii, ndugu na familia.

**Namna ya kudhibiti njia zisizohalali katika ujasiriamali**

(a) *Kutoa elimu kwa jamii*: Jamiii ielimishwe kuhusu kuzingatia bidhaa zenye viwango. Waepuke kununua na kuuza bidhaa haramu za viwango vya chini na zilizopitwa na wakati. Elimu hii itaisaidia jamii kuangalia kwa umakini tarehe ya kuchotara bidhaa ili kuepuka madhara ya kiafya inayoweza kupata baada ya matumizi ya bidhaa hizo.

(b) *Kutoa elimu kwa wajasiriamali*: Wajasiriamali wapewe elimu juu ya umuhimu wa kufanya biashara kwa kufuata sheria za nchi, na kufanya biashara kwa kutumia njia halali. Elimu hii itawasaidia wajasiriamali kufuata sheria na kanuni za biashara na kuepuka kufanya biashara kwa kutumia njia zisizo halali. Elimu hii pia itawasaidia wajasiriamali kufanya biashara kwa ufanisi na kwa uhuru. Elimu hii itawasaidia kupata

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 183 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

maelekezo na vibali mbalimbali kutoka katika vyombo vya udhibiti vya serikali kabla ya kuanzisha biashara au kusambaza bidhaa.

(c) *Kutunga na kutekeleza sheria za kudhibiti biashara zisizotumia njia halali:* Sheria hizi zitawasaidia wajasiriamali kufanya biashara kwa kutumia njia halali na kuepuka adhabu zitakazotolewa kwa kutofuata taratibu zinazotakiwa kwenye biashara husika. Sheria hizi zitawasaidia wajasiriamali kubuni mbinu za uboreshaji wa biashara kwa kuuza na kununua bidhaa bora. Hali hii itaongeza kipato na kukuza biashara. Wajasiriamali wanaokiuka taratibu na sheria za nchi pamoja na washirika wao wapelekwe katika vyombo vya sheria na kuchukuliwa hatua. Hatua ya kisheria itakuwa ni fundisho kwa wajasiriamali wote na wanunuzi wa bidhaa zinazotokana na biashara inayotumia njia zisizo halali. Adhabu hizi zitawasaidia kubadilika na kutambua umuhimu wa kufanya biashara kwa kutumia njia halali kwa maendeleo ya uchumi wa familia na jamii inayowazunguka.

(d) *Kudhibiti utumiaji wa bidhaa zinazotokana na biashara zinazo tumia njia zisizo halali*: Hali hii itasababisha wajasiriamali ambao wanajihusisha na biashara hizo kukosa wateja na hivyo kuona umuhimu wa kufanya biashara kwa kutumia njia halali ili kujiongezea kipato kwa maendeleo ya familia na taifa. Watumiaji wa bidhaa wakitoa ushirikiano stahiki, itasaidia kukomesha biashara zinazo tumia njia zisizo halali nchini.



**Kazi ya kufanya namba 2**

Shirikiana na wanafunzi wenzako katika vikundi, kujadili yafuatayo:

1. Ni njia zipi zisizo halali katika ujasiriamali zinazoweza kukwamisha maendeleo ya uchumi wa nchi?
2. Nini madhara ya njia hizo katika uchumi na jamii?
3. Jinsi mnavyoweza kudhibiti njia zisizo halali katika ujasiriamali.
4. Kwa nini mnadhani hizo ndiyo njia bora za kudhibiti njia zisizohalali katika ujasiriamali?

Wasilisheni kazi zenu darasani.



MAARIFA YA JAMII STD 7.indd 184 30/07/2021 11:59

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Zoezi la 4

**Jibu maswali yafuatayo:**

**A. Jaza nafasi zilizoachwa wazi**

1. Athari tatu za njia zisizo halali katika ujasiriamali ni;
   (a) ________
   (b) ________
   (c) ________.

**B. Oanisha kifungu cha maneno kutoka safu A na kifungu cha maneno kilichopo safu B kisha andika herufi ya jibu sahihi katika nafasi uliyopewa.**

| Safu A | Jibu | Safu B |
|---|---|---|
| 2. Wataalamu wanaohakiki vipimo vya bidhaa mbalimbali. | | (a) Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) |
| 3. Njia zisizo halali za ujasiriamali | | (b) wakala wa vipimo Tanzania |
| 4. Mamlaka inayoangalia ubora wa bidhaa | | (c) njia mojawapo ya kudhibiti biashara isiyotumia njia halali |
| 5. Wajasiriamali wanaokwepa kulipa kodi ni rahisi kubainika wakati ukaguzi unapofanywa na ___________. | | (d) Shirika la Viwango Tanzania (TBS) |
| 6. Kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kununua bidhaa zenye viwango. | | (e) Huathiri mapato ya serikali |
| | | (f) Wakala wa barabara |
| | | (g) Wakala wa madini Tanzania |
| | | (h) Huleta mapato zaidi serikali kuu |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

7. Eleza maana ya biashara inayotumia njia zisizo halali.

8. Taja makosa manne ya udanganyifu kwenye vipimo yanayoweza kuepukwa na wajasiriamali.

**C. Andika KWELI kwa sentensi ya kweli na SI KWELI kwa sentensi isiyo ya kweli katika nafasi uliyopewa.**

9. Kufanya biashara haramu ni njia halali inayotumiwa na baadhi ya wajasiriamali ili kujiongezea kipato. __________

10. Wajasiriamali wanashauriwa kuepuka kujiingiza kwenye biashara haramu kama vile biashara ya kuuza vipodozi vyenye viambato vyenye sumu. __________

11. Ukwepaji wa kodi kwa baadhi ya wajasiriamali hukosesha taifa mapato. __________

12. Ubora wa bidhaa za wajasiriamali huthibitishwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). __________

13. Namna ya kudhibiti njia zisizohalali katika ujasiriamali ni kutoa elimu kwa wajasiriamali na wananchi kwa ujumla. __________

## Msamiati

Fursa — nafasi ambayo mtu anaweza kuitumia kutekeleza wazo la kibiashara na kujiongezea kipato

Kuchotara — kutofaa kutumika kwa bidhaa kutokana na muda wa matumizi kuisha

FOR ONLINE USE ONLY

Taasisi ya Elimu Tanzania

## Vitabu vingine vya Darasa la Saba






















ISBN 978-9987-09-338-0
9 789987 093380

Maarifa ya Jamii 7 FOR SALECover.indd 1